ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.

14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini

32. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
33. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
34 .Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani

55.Mhe. Mohammed Said Mohammed Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak Nafasi za Wanawake

57.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

58. Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

61.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

62.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

63.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Rashid Seif Suleiman Jimbo la Ziwani

65.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

66.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

67.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

68.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

69.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

70.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

71.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe

74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan Jimbo la Dole

75.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni

76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde

77.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani

78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake
Ndg. Yahya Khamis Hamad	**Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

Kikao cha Nane – Tarehe 10 Aprili, 2012

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Naibu Spika (Ali Abdalla Ali) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 158

Magari Mabovu katika Mabaraza ya Miji ya Chake Chake na Mkoani

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman – Aliuliza:-
Miongoni mwa kazi za Mabaraza ya Miji kwa mujibu wa Sheria Nam. 4 ya 1995 ni kuweka miji katika hali ya usafi. Miji ya Mkoani na Chake Chake ina upungufu wa magari ya kubebea taka. Yaliyopo ni mabovu na hayafanyi kazi vyema kuweka usafi wa miji hiyo.

(a) Mhe. Waziri, Wizara yako ina mpango gani wa kununua magari mapya kwa ajili ya Mabaraza ya Miji hiyo na Miji mingine hapa nchini.
(b) Kwa sasa Wizara yako ina mpango gani wa kuyatengeneza magari hayo ili yasaidie kwa kujishikiza mpaka hapo magari mapya yatakapokuwa tayari.

Mhe.Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi -Alijibu**:-**

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 158 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba Serikali kupitia Mpango wa Kuimarisha Huduma za Mji Zanzibar *(Zanzibar Urban Service Program –ZUSP)*, inatarajia kununua magari matano (5) ya kuzolea taka na maji machafu kwa Mabaraza ya Miji Pemba kabla ya kumalizika mwaka huu wa fedha wa 2011/2012. Jumla ya magari mawili (2) kwa Baraza la Mji Chake Chake, gari moja kwa Baraza la Mji la Mkoani na magari mawili (2) kwa Baraza la Mji Wete. Magari haya tuliyatarajia yangefika nchini mwezi Aprili lakini kwa bahati mbaya yamechelewa kidogo na tunayatarajia wakati wowote yatafika na yale ya Unguja.
b) Mhe. Mwenyekiti, Mabaraza ya Miji na Halmashauri zinaendelea kuzifanyia matengenezo gari zake za kuzolea taka. Baraza la Mji la Chake Chake gari moja tayari imeshafanyiwa matengenezo na imeanza kufanya kazi na gari ya pili inaendelea na matengenezo. Aidha, Baraza la Mji Mkoani linaendelea na kuifanyia matengenezo gari yake moja ya aina ya Isuzu.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Mabaraza yetu

yana magari machache. Je, huoni iko haja ya kuongeza *shift* za kusombea taka ili ziende hata jioni na usiku kwa lengo la kupunguza taka zilizorundikana katika majaa yetu.

Swali (b) je, Mabaraza yana mpango gani wa kupata *trolley* za kuvutia mikono ili kusaidia hayo magari chakavu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba ni vyema tukaongeza *shift* kwa kuzingatia kwamba magari tuliyonayo ni machache na yanaharibika mara kwa mara. Sasa kupata ufanisi ni vizuri tukaongeza *shift* ili kazi ile ya kusomba taka ikafanywa hata nyakati za usiku.

Hilo wizara yetu imelizingatia na miji mingi ukipeleleza usafi unafanywa wakati wa usiku pale mji umetulia kwa hivyo wanapata nafasi nzuri sana alfajiri wewe unaamka mji uko safi. Kwa hivyo na sisi tunazingatia mpango huo tukishatayarisha mazingira huko kwa kutupia taka basi na hili tutalizingatia.

Kuhusu yale magari ya kukokotwa na mkono au *trolley* mradi wa *ZUSP* pia umezingatia kwamba miji yetu ina vichochoro ukizingatia kwamba miji ya Mkoani, Chake Chake na Wete mna vichochoro wakati mwengine magari makubwa hayapiti. Kwa hivyo, katika huu mradi kumeagizwa tayari vi-*trolley* kama yale magari ya zamani ya watu watatu anakuwepo dereva anaingia mbele na wengine wanasukuma sasa yale yanapita katika vichochoro vyote.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, hivi sasa kwa baadhi ya maeneo taka ni malighafi. Je, Mhe. Waziri haoni kwamba wakati umefika sasa kuweza kushirikiana na taasisi ambazo zinaweza kuchukua taka kama ni malighafi na wao wakatusaidia katika shughuli ya usafishaji wa mji wetu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, nakubaliana kabisa na wazo la Mhe. Mwakilishi kwamba ni vyema wizara yetu ikashirikiana na taasisi binafsi na hata vikundi. Kwa kweli tunatoa pongezi za dhati kabisa vikundi hivi vinafanya kazi nzuri vinashirikiana na wizara wanajitolea kwa hiari yao na wengine wanatoa rasilimali zao kuusafisha mji wetu.

Lakini Mhe. Naibu Spika, naomba kwa mara nyengine tena nizidi kusema serikali imeshatangaza kwamba kazi hii tuko tayari sisi wajitokeze watu binafsi makampuni watusaidie na hivyo ndio inavyofanywa sehemu zote ulimwenguni. Kwa hivyo, sisi tumeshatangaza katika hotuba ya bajeti yetu hii tunayokwenda nayo kwamba hili suala tusaidiane na taasisi binafsi.

Bahati nzuri viko vikundi katika Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi, Halmashauri za Mkele kule wao wanafanya, hata sasa hivi mpaka Shehia za Malindi, Shangani nao wameanza utaratibu huu. Kwa kweli tunawapongeza sana lazima tushirikiane sote bega kwa bega kufanikisha suala hili.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, mara kadhaa tumekuwa tukiwaona wataalam wetu wa

Baraza la Manispaa na wataalam wa Wizara wakienda nchi za nje kujifunza matumizi mbadala ya taka ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa nishati. Kwa nini wizara yake na wataalam wake wanashindwa kutumia taka kwa nishati mbadala.

Swali (b) kwa kuwa wataalam wake wameshindwa kutumia taka kwa nishati mbadala, kwa Unguja wameamua kuzitupa taka hizo katika majaa ya Jumbi na kusababisha uchafu mkubwa. Kwa Pemba hawaoni kwamba sasa kuna haja ya taka hizo kuzitupa kule Muambe ambako serikali wameharibu mazingira.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, ni kweli kwamba nchi nyingi taka huwa zinatumiwa kama nishati mbadala na hapa kwetu wazo hilo lilikuja lakini bado halijakaa sawa. Lakini nataka kusema kwamba tayari zimejitokeza kampuni nyengine kwa baadhi ya taka kuzifanyia *recycling* kama kuzichukua wao wakenda wakazisindika kwa matumizi mengine kama chupa za maji, maboksi. Kwa hivyo, tunao wawekezaji kama wawili wameshajitokeza tunaendelea na mazungumzo nao.

Lakini vile vile baada ya ziara ya Mhe. Makamo wa Kwanza wa Rais na ujumbe wake kule India basi wameiona kampuni moja ambayo wanazisindika hizo taka kwa kupata mbolea. Tumepata maelekezo twende tukasome tukaone na vipi Zanzibar tunaweza tukaitumia teknolojia hiyo. Tumo katika mipango ya kukamilisha safari ya vijana wetu waende nao wakasome hilo suala.
Kuhusu kutupa taka Muambe ni kweli kwamba kwa Unguja tunatupa Jumbi lakini Jumbi tumeshahama sasa nafikiri wako pande za Ndijani au Tunguu. Tunajaribu kukimbia mjini humu unajua tena *urbanization* imeshafika mbali. Sasa swali lako kwamba na Muambe vipi kuna mashimo kule. Hilo tumelisikia tutalizingatia tuone kwamba kule mashimo yale yaliyopo yanafukiwa kwa utaratibu maalum ili tuepuke hasa vile vyanzo vya maji.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, kwanza kabla ya kujibiwa swali langu nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwa jitihada anazozichukua na anaendelea nazo hivi majuzi tu amepeleka watoto nchini India kwa matibabu ya maradhi ya moyo. Mhe. Waziri hongera sana. *(Makofi)*

Nam. 14

Wafanyakazi wa Benki ya Damu Pemba

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Wafanyakazi wa Benki ya Damu Pemba ni sita (6) tu na wanafanya kazi Pemba nzima bila ya kuwa na posho, marupurupu pamoja na vikao vya semina, tofauti na wenzao wa Unguja ambao hupatiwa marupurupu, posho na semina na kufanya mishahara yao kuwa mikubwa zaidi.

(a) Mhe. Waziri, kuna sababu zipi zinazopelekea ubaguzi huo.

(b) Inakuwaje wafanyakazi wa Benki ya Damu Pemba maslahi wanayolipwa hayafanani na ya wale wanayolipwa Unguja wakati kazi wanayoifanya ni ya aina moja.

(c) Kwa kuwa wafanyakazi hao hawashughulikiwi kama wale wa Unguja na kwa kuwa wanachama wa Benki ya Damu hawajawahi kupewa semina na motisha yoyote. Je, Serikali haikusudii kuwa na Benki ya Damu yenye ufanisi Pemba.

(d) Huoni kwamba tofauti hizo za kimaslahi kuwa ndio chimbuko la watumishi wa Wizara yako hasa madaktari kukataa wanapopangiwa kwenda kufanya kazi Pemba.

Mhe. Waziri wa Afya - Alijibu**:-**

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 14 lenye kifungu a, b, c na d kwa pamoja kama ifuatavyo:

Mhe. Naibu Spika, Mpango wa Damu Salama ni mradi unaofadhiliwa kwa asilimia 100 na Mfuko wa Rais wa Marekani wa Kuzuia Maambukizi ya Ukimwi *(PEPFAR)* yaani *President Emergency Plan For Aids Relief* kupitia Kituo cha Kukinga Maradhi *(CDC).* Taratibu za mpango huo duniani kote ni kuwa na kituo kimoja cha damu *(Blood Centre)* ambacho huhudumia sehemu kubwa ya jamii kwa kusambaza damu na sehemu za damu zilizotenganishwa katika mabenki ya damu ya hospitali. Kituo Kikuu cha Damu Salama cha Zanzibar kipo Amani Sebleni Unguja na kina wafanyakazi wake, kinashughulika na kazi zote za kukusanya damu.

Kwa mfano, mwezi Oktoba 2010 hadi Novemba 2011 kilikusanya lita 7,965 sawa na asilimia 84 ya mahitaji ya malengo yake na Pemba kilikusanya lita 1,271 sawa na asilimia 16 ya damu inayohitajika malengo yake. Kituo kinahusika na kuzipima damu za Unguja na Pemba maambukizi yote ikiwemo ukimwi (HIV), homa ya ini *(Hepatitis B na C),* maradhi ya Kaswende *(Syphillis)* na maradhi mengine yote kwa kutumia teknolojia maalum, kupima makundi ya damu na kutenganisha sehemu za damu, kusimamia uendeshaji wa huduma katika kituo na kusambaza damu Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile kituo ni kimoja kwa nchi yetu na kwa mazingira yetu ya visiwa yalivyo, kwa ushauri wa Wizara na utaratibu uliopo na wale wanaotufadhili kituo kiliona ipo haja ya kuwa na kiungo *(satellite site)* huko Pemba cha kusambaza huduma zake huko na kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Pemba. *Satellite site* hiyo ambayo iko katika Benki ya Damu ya Hospitali ya Wete inafanya sehemu ndogo tu ya shughuli za damu salama. Kazi za *satellite site* hii ni kukusanya damu kwa ajili ya hospitali za Pemba na baadae kuipeleka Unguja kwa matayarisho yote ya uchunguzi yaliyobaki, kupokea damu na sehemu za damu zilizotenganishwa kutoka Unguja, kuitunza na kuisambaza katika hospitali za Pemba pale inapohitajika.

Kituo hicho cha Pemba kina wafanyakazi saba (7) ambao ni waajiriwa wa Serikali na hivyo wanapata mishahara ya Serikali kama wanavyopata wengine. Lakini pia wafanyakazi hao wanapatiwa posho kutoka fedha za uendeshaji za mfadhili kwa mujibu wa ratiba ya ukusanyaji wa damu. Kutokana na sharti la kuwa na kituo kimoja tu cha damu ambapo ndipo penye kufanyikana kazi zote, wale wanafanya kazi Unguja hupatiwa *top allowance* tofauti na wale wa Pemba ambao kazi yao ni kukusanya na kusambaza tu.

Wafanyakazi hao wa Pemba pia wameshirikishwa katika mafunzo mbali mbali yanayoendeshwa Zanzibar na Tanzania Bara juu ya ukusanyaji wa damu kadri ya nafasi zinapotokea mara wanapopatiwa nafasi ya kuungana na wafanyakazi wenzao wa kituo kikuu kwa mazoezi zaidi ya kazi.

Satellite hiyo ya Pemba imepatiwa vifaa, vitendea kazi na jokofu maalum la kutunzia sehemu ya damu zilizotenganishwa zilizotayarishwa kituo kikuu cha Unguja. Mhe. Naibu Spika, kwa sura hii mradi huu Wizara haioni uhusiano wowote wa mradi kwa suala la kukusanya damu na watumishi kukataa kupangiwa kufanya kazi Pemba.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kuna tofauti kubwa ya ulipaji posho na stahiki nyengine kwa wafanyakazi wa Benki ya Damu iliyoko Pemba.

Je, huoni Mhe. Waziri si kuwabagua Wazanzibari huko na vile vile kuwa wanafanya kazi hatarishi je, huoni kuwa ipo haja ya kuwapatia *risk allowance*.

Swalib (b) kwa kuwa suala la Benki ya Damu ni muhimu kamati ilitembelea Hospitali ya Makunduchi na kuona kwamba kuna tatizo kubwa la suala la umeme. Je, umejipanga vipi kutatua tatizo hilo katika Hospitali ya Makunduchi ili damu ile iwe salama.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, kuhusu tofauti ya allowance ya wale wa Unguja na Pemba nimeeleza kwenye swali langu mama kwamba wafanyakazi wanaofanya kazi Pemba wana kazi mbili, kutunza damu iliyokuwa imeshafanyiwa uchunguzi kituo kikuu cha Unguja na kukusanya damu huko Pemba wakaileta Unguja ikafanyiwa uchunguzi. Kazi zote za kitaalam zinazohusiana na ukusanyaji wa damu zinafanywa Unguja, kwa hivyo wafanyakazi wa Pemba wana kazi mbili kubwa, kupokea damu iliyokuwa imeshafanyiwa uchunguzi wakaisambaza inapohitajika na kukusanya damu Pemba.

Nimeeleza kwamba wamekusanya damu asilimia 16 tu Pemba na utaratibu uliokuwepo kwamba kila wanapokwenda kukusanya damu huko Pemba kila mfanyakazi hulipwa shilingi 15,000/-. Wale wanaofanya kazi Unguja ambao muda wote wapo kazini kufanya kazi wanalipwa tena hawalipwi na serikali wanalipwa na hao wafadhili *top up allowance* kutokana na ule ugumu wa kazi wanazozifanya hapa. Kwa hivyo, tofauti ya kazi ndio inayofanya tofauti ya posho.

Suala la kituo cha Makunduchi na kuwa hakuna umeme hapo walipokwenda wazee kweli kulikuwa na tatizo hili lakini ninachoamini tumeshalishughulikia suala hilo. Suala la umeme sio la kituo cha Makunduchi, suala la umeme ni suala la nchi nzima, mimi nina ushahidi kwamba kila siku nyumbani kwangu nazimiwa umeme saa 1:30 na hiyo ni utaratibu kwa taifa. Lakini suala hilo tumeshalishughulikia na kutunza damu hiyo maana isipotunzwa itaharibika.

Nam. 69

Matumizi ya Kompyuta

Shadya Mohammed Suleiman – Aliuliza:-

Baadhi ya Taasisi za Serikali ziliwahi kutoa maziwa kuwasaidia watumishi wao wanaotumia kompyuta na baadae zilisitisha utaratibu huo. Lakini ziko baadhi ya taasisi ambazo bado zinaendelea na utaratibu huo.

(a) Mhe. Waziri, ni ipi Sera ya Serikali kuhusu suala hilo.
(b) Kwa nini baadhi ya taasisi zimeondoa utaratibu huo.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 69 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Hata hivyo, kabla sijamjibu swali lake naomba kutoa maelezo yafuatayo:

Mhe. Naibu Spika, wakati kompyuta hasa kompyuta za mezani yaani *PC* zilipoanza kuingia kulikuwa na hisia nyingi juu ya mazingira ya kuzitumia yakiwemo chumba cha kompyuta lazima kiwe na vipoza joto *(AC).* Wanaoingia kwenye chumba cha kompyuta wavue viatu, mtumiaji wa kompyuta anywe maziwa ya ng'ombe au maziwa mengine ya unga na kadhalika, baadae ilikuja na kubainika kuwa mengi yao hayakuwa na ulazima.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa serikali ilikuwa inawapa posho la maziwa watumishi wake na wakati wa kuunganisha maposho na mshahara wa msingi *(consolidation)* posho hiyo iliingizwa katika mishahara yao.

Mhe. Naibu Spika, maeneo ya matumizi ya kompyuta sasa yamepanuka sawa takriban kila mfanyakazi anatumia kompyuta, iwe kompyuta kubwa za mezani yaani *PC*, kompyuta ndogo *(lap top),* simu ambazo nyingi zao zina matumizi kama ya kompyuta na wengine wanatumia kompyuta za *internet café* na kwa hivyo kufanya watumiaji wa kompyuta kuwa wengi kwa kiasi ambacho isingewezekana kwa serikali kuwalipa posho watumishi wote husika kufuatia matumizi ya vifaa hivyo.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 69 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali haina utaratibu kuhusu kuwapa maziwa watumiaji wa kompyuta na wala hakuna sharti hilo katika matumizi ya kompyuta.
(b) Baadhi ya taasisi zimeondoa utaratibu huo kutokana na kuwa si rahisi kuwapa maziwa watumishi wote wanaotumia kompyuta ambao takriban ni wengi kuliko wasiotumia na ukweli kwamba wanaopewa posho hiyo hawaitumii kununulia maziwa. Aidha, sio tena mtazamo wa watu kuwa maziwa ni dawa ya kuzuia madhara ya kutumia kompyuta. Zaidi ya haya hakuna sheria inayoelekeza hivyo.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali lake

alizungumzia zaidi juu ya matumizi ya kompyuta kama Mhe Mwakilishi alivyouliza swali lake la msingi.

Lakini mbali ya watumishi wanaotumia kompyuta kuna watumishi ambao hawapati posho za maziwa wanaofanya kazi katika vituo vya kurushia matangazo hasa *Television Zanzibar* ambako kuna mitambo mingi ambapo wanahitaji kupata kitu cha aina hii. Je, Mhe. Waziri hili la wafanyakazi wanaotumia muda wao mwingi katika vyombo vya kurushia matangazo hasa *Television Zanzibar* anasemaje.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, watumishi wa vituo vya redio ambao wanapaswa kupata huduma hii mimi nadhani serikali ina utaratibu wa kuweka *OC* katika kila fungu, kuweka *consolidation* kwa watumishi wa kompyuta haiondoshi kabisa *OC* za vifungu vinavyostahiki kulipwa watumishi katika taasisi zao. Kwa hivyo, kama hilo halipo ni jukumu sasa la wizara na taasisi husika kuweza kulitekeleza hilo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali la msingi na hata swali la nyongeza la Mhe. Salmin Awadh Salmin amejenga hoja kwamba vifungu vya *OC* labda visaidie katika maposho hayo. Lakini ni kawaida ya nchi nyingi duniani kutoa *risk allowance* kwa wafanyakazi wake ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu kama hao wa mitambo ya redio na hata masuala ya mionzi kwenye hospitali zetu.

Je, ni kwa nini serikali hii haiwajali wafanyakazi wake kwa kuwawekea fungu hilo kwa ajili ya matibabu na huduma ya dharura pale ambapo zitatokezea athari za mionzi.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, nimesema kwamba serikali ilipounganisha maposho na mishahara iliondosha baadhi ya maposho mengi kwa watumishi wa umma. Sasa kama hoja Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo inaona umuhimu wa kuweka *risk allowance* kwa watumishi hasa wa vituo vya redio upo ni jukumu la wizara kuleta maombi rasmi serikalini ili serikali iweze kuyazingatia na kuweza kuchukua hatua inayofaa.

Nam. 61

Dakhalia na Nyumba za Walimu

Mhe. Ashura Sharif Ali - Aliuliza:-

Serikali imeandaa mpango mzuri wa kujenga skuli za Sekondari za Wilaya kwa nia ya kuwapatia vijana wetu elimu iliyo bora na inayoendana na wakati. Katika kuhakikisha kwamba tunafikia lengo hilo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga dakhalia pamoja na nyumba za walimu katika skuli hizo ili kuondosha usumbufu kwa walimu na wanafunzi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mheshimiwa Mwakilishi swali lake namba 61 kama hivi ifuatavyo :-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Sekondari inajenga skuli za Sekondari 19 kwa ushirikiano na Benki ya Dunia. Kati ya skuli hizo skuli 8 mbali na kuwa na madarasa, maktaba, maabara tatu na chumba cha Kompyuta zilikusudiwa kuwa na dakhalia za wanafunzi wa wavulana na wasichana na nyumba 10 za walimu. Skuli hizo za Sekondari ni Paje na Mtule Wilaya ya Kusini, Matemwe Wilaya ya Kaskazini B Muwanda Wilaya ya Kaskazini A na Uzini Wilaya ya Kati Unguja. Kwa Upande wa skuli za Pemba ni skuli ya Pandani Wilaya ya Wete, Chwaka – Tumbe Wilaya ya Micheweni, Wawi Wilaya ya Chake Chake, na Kiwani Mauwani Wilaya ya Mkoani Pemba.

Hata hivyo, kutokana na gharama kubwa za ujenzi ukilinganisha na fedha zilizotengwa, baadhi ya majengo yalibidi yapunguzwe katika ujenzi katika awamu hii. Pamoja na majengo yaliyopunguzwa katika skuli hizo ni dakhalia zote mbili za wanawake na wanaume na nyumba saba za walimu kwa kila skuli. Nyumba zilizojengwa ni tatu tu. Skuli hizo zitakapomalizika zitaanza kutumika bila ya kuwa na dakhalia. Hata hivyo, dhamira ya kuanzisha dakhalia katika skuli hizo bado ipo na serikali inaendelea kufanya mazungumzo na Benki ya Dunia, kutafuta uwezekano wa mradi huo kupatiwa fedha za ziada kumalizia kazi ambazo hazikuweza kukamilishwa katika hatua ya kwanza kutokana na uhaba wa fedha. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Asha Bakar Makame: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutuwezesha siku ya leo kuamka katika hali ya afya njema.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo. Mhe.Naibu Waziri atakubaliana na mimi kuwa tunapofanya mambo yetu ni bora tukafanya uchunguzi kwanza na kuhakikisha kwamba mambo tunayoyafanya hayatoleta matatizo. Hilo la kwanza.

Pili, niipongeze sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa dhamira nzuri ya kujenga sekondari hizi. Je, hazitoleta usumbufu kama hayakukamilishwa mambo haya yote ya dakhalia pamoja na nyumba za walimu, itakuwa kazi yetu ilikuwa ni ya bure kuweka magofu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika. Mimi nataka nikubaliane na Mhe. Asha Bakar, mama yangu, kuwa ni kweli kuna ulazima wa serikali kufanya utafiti pindi inapotaka kufanya mambo yake.

Kwa hili Mhe. Naibu Spika, nimuhakikishie Mhe. Asha Bakar mama yangu kwamba tulifanya utafiti wa kutosha. Lililotokea Mhe. Naibu Spika, kama ambavyo nilijibu juzi katika swali kama hili kuwa muda ambao tuliwekeana mkataba wa ujenzi sio muda ambao tulianza kujenga. Kwa hivyo, kipindi hiki gharama za ujenzi zikaongezeka, hivyo yale mahitaji ikabidi yaongezeke, ndio tukashindwa kutimiza azma hii ambayo tulikusudia.

Lakini nataka nimuhakikishie Mhe. Asha Bakar mama yangu pamoja na Baraza lako tukufu kama ambavyo nilijibu kwenye swali langu mama kuwa, dakhalia hizo bado tuna nia ya kuzijenga, kwa sababu skuli hizi 8 ni skuli za wilaya na ni skuli ambazo tunakusudia kuchukua wanafunzi wa wilaya nzima na wale wanafunzi *cream* ndio tunakusudia wasome katika skuli hizo. Nakushukuru Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Kwa sababu skuli hizo kama alivyosema ni skuli za wilaya na kuna baadhi ya skuli ziko mbali kidogo na mji, na tunakusudia kuwapeleka watoto wetu kwa ajili ya kupata elimu. Kwa mfano, skuli inayojengwa Chwaka Tumbe, ambayo ni skuli ya Wilaya ya Micheweni ipo mbali kidogo na mji. Je, atakubaliana na mimi kwamba kuna haja ya makusudi ya kujengewa dakhalia wanafunzi wa pale Tumbe ili wapate kusoma vizuri.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, narudia kusema kama ambavyo nimesema mwanzo kwamba madhali skuli zile ni za wilaya basi wanafunzi wengine ni lazima watakuwa wako mbali. Lakini kwa sasa Mhe. Naibu Spika, zile ambazo ziko tayari kuzifungua, basi tutawachukua wanafunzi ambao wako karibu na maeneo yale tulipojenga skuli zile, mpaka hapo tutakapoanza kujenga dakhalia, basi ndio tutakapowachukua wanafunzi wanaotoka mbali. Naomba tukubaliane hivyo na Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na mimi kwa kunipatia fursa hii ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa serikali imeamua kujenga skuli zile nzuri za kisasa zinazokwenda na wakati. Je, serikali itachukua hatua gani ya kuzijengea skuli zile uzio ili ziweze kuishi katika mazingira bora.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika. Ni kweli Mhe. Naibu Spika, kama alivyosema Mhe. Mjumbe kuwa skuli kuna haja ya kuzijengea uzio. Katika haya mazungumzo yetu ambayo tunaendelea kuzungumza na wenzetu wa *World Bank*, tunakusudia kati ya mambo ambayo tutayafanya katika skuli zile basi moja ni uzio, ukiondoa hiyo dakhalia na nyumba za walimu na jengine tunalotegemea ni uzio Mhe. Naibu Spika.

Nam. 62

Upungufu wa Walimu

Mhe. Ashura Sharif Ali - Aliuliza:-

Walimu katika Taifa lolote duniani ni chachu ya Maendeleo. Kwa upande wa nchi yetu tuna upungufu wa walimu katika skuli nyingi licha ya idadi kubwa ya walimu wanaohitimu kila mwaka katika vyuo vyetu.

(a) Je, Wizara ina mpango gani wa uajiri kwa walimu ambao wameshaomba ajira.

(b) Je, kuna sababu gani zinazokwamisha ajira hizo mpaka leo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 62 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa skuli zetu nyingi zina upungufu wa walimu licha ya kuwepo walimu wengi waliohitimu mafunzo ya ualimu katika vyuo mbali mbali ambao hadi hivi sasa baadhi yao hawajaajiriwa. Hata hivyo, hivi karibuni, wizara yangu imepata kibali kutoka Tume ya Utumishi Serikalini kuajiri walimu 240. Baada ya maelezo hayo, napenda kujibu kama hivi ifuatavyo:-

a) Mhe. Naibu Spika, hivi sasa wizara imeshaanza taratibu za uajiri kwa walimu 240 ambapo tumepata kibali cha uajiri kutoka Tume ya Utumishi. Walimu hao wametangaziwa kwenye redio na wengi wamesharipoti Wizarani Unguja na Pemba na tunakamilisha taratibu tu za ajira.
b) Mhe. Naibu Spika, kuchelewa kuajiriwa kwa walimu hao kumetokana na kuchelewa kupatikana kibali cha uajiri kutoka Tume ya Utumishi Serikalini.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri nimuulize swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri anasema kibali kilichotolewa ni kuajiri walimu 240. Naomba nimuulize je, mahitaji ya nchi sasa hivi ni walimu wangapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, mahitaji ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa hivi sasa ni makubwa. Kwa Pemba peke yake tunahitaji karibu walimu 700, kwa skuli hizi mpya tunahitaji walimu karibu 525 na kama mnakumbuka Wajumbe katika bajeti yetu ambayo tuliisoma hapa, tuliomba kuwaajiri walimu 800. Lakini mpaka sasa hivi Tume ya utumishi imetupa kibali cha kuwaajiri walimu 500 na walimu 240 ni hawa tayari ambao tumeshawaajiri, na tunatarajia kuwaajiri walimu wengine 260 waliobakia. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo. Katika majibu yake mama Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba wamepata kibali cha kuwaajiri walimu kama 500, lakini walimu 240 ndio tayari wameshaajiriwa. Kwa kuwa walimu wengi ni walimu wanawake kuliko walimu wanaume na kwa kuwa hapa kwetu Zanzibar bado tunahitaji sana kuwa na walimu wanaume. Je, Mhe. Naibu Spika, Mhe. Naibu Waziri hao walimu 240 waliowaajiri walimu wangapi ni wanaume.
Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, mchanganuo wa kusema kwamba ni walimu wangapi wanawake na walimu wangapi wanaume, kwa hivi sasa hapa niliposimama nitakuwa sina. Lakini takwimu hizo zipo na Mhe. Mwakilishi nitamletea kwa maandishi, kuwa ni walimu wangapi wanawake na walimu wangapi ni wanaume.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Je, Mhe. Naibu Waziri hivi sasa tuna walimu wangapi wa sekondari kwa Unguja na Pemba, pamoja na msingi ambao wameshaajiriwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa swali hili ni la nne na kanuni inatuongoza kwamba maswali ni matatu tu, lakini kwa maslahi ya wajumbe wa Baraza, naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake.

Mhe. Naibu Spika, walimu ambao wameajiriwa hivi sasa ni walimu 240 na hao ni wa sekondari sio wa msingi.

Nam. 103
Tatizo la Kuzimwa kwa Umeme

Mhe. Asha Bakar Makame – Aliuliza:-

Tatizo la kuzimwa kwa umeme limekuwa sugu katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar na linaendelea kuathiri maisha ya wananchi wa visiwa vyetu.

(a) Maeneo ya Chukwani, Mbweni na Mazizini ni waathirika wakuu wa kuzimwa zimwa ovyo umeme, ni sababu zipi zilizopelekea hali hiyo.
(b) Ni lini hasa wizara yako italimaliza tatizo hilo kwa wananchi wa visiwa hivi hususan wa Shehia ya Chukwani, Mbweni na Mazizini.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 103 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Mhe. Naibu Spika, kwanza kabla ya kumjibu swali hilo napenda kutoa ufafanuzi kwamba umeme hauzimwi ovyo kama alivyoeleza. Usahihi ni kwamba umeme katika maeneo hayo huwa unazimika mara kwa mara. Mhe. Naibu Spika, sababu zinazopelekea kuzimika kwa umeme mara kwa mara katika maeneo hayo ni uchakavu wa miundombinu katika njia hiyo ya umeme na kuzidiwa kwa *transformer* zilizopo.
Mhe. Naibu Spika, wizara yangu kwa kupitia Shirika la Umeme imo katika jitihada za kuliondoa tatizo hilo na hivi sasa kuna miradi mikuu ya kukarabati miundombinu hiyo ya umeme inaendelea, yenye lengo la kuliondoa kabisa tatizo hilo. Miradi hiyo ni pamoja na mradi wa uwekaji wa njia ya pili ya umeme kutoka Bara kuja Unguja wa MCC, mradi wa ukarabati wa miundombinu ya umeme wa JICA na mradi wa ukarabati wa kituo kikuu cha umeme cha Mpendae wa Belgium.

Mhe. Asha Bakar Makame: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza sikuridhika na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, kwa sababu naona misamiati imekuwa mingi. Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a), (b) na (c).

(a) Je, Mhe. Naibu Waziri, wizara ina utaratibu gani wa kuwalipia fidia watu ambao wameharibikiwa na vitu vyao.

(b) Kama vipo ni nani hasa anayehusika na malipo hayo.

(c) Je, atakubaliana na mimi Mhe. Naibu Waziri kwamba sasa hivi kuna haja ya kufanya uchunguzi kwa Unguja nzima ni jinsi gani umeme unavyozima zima, na kama unazima zima ni vyema serikali ikafanya uchunguzi au Shirika la Umeme likafanya uchunguzi kuhakikisha ni sehemu gani na gani inataka *transformer* kubwa na sehemu gani inataka *transformer* ndogo, ili kutowasumbua wananchi kwa kuharibikiwa na vitu vyao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, Shirika la Umeme Zanzibar huwa linamsaidia mwananchi pale anapopata tatizo ambalo limesababishwa na *short* ya umeme, ambapo pengine sio tatizo la *wirering* ni tatizo la *line.* Kwa hivyo, hapo ndio Shirika linamsaidia mteja huyo kwa kile ambacho kilichojitokeza. Kama ni kuungua kwa nyumba huwa inachangia asilimia fulani katika ujenzi wa nyumba hiyo, au chombo chengine chochote.

Mhe. Naibu Spika, anayehusika na suala hilo ni Meneja Mkuu wa Shirika la Umeme. Kwa hivyo, tatizo hilo linapotokea wakati wowote naomba wateja wawasiliane na Meneja wa Shirika la Umeme, kwa ajili ya kufanya uchunguzi katika *shoti* hiyo na kufanyiwa malipo au michango ya hasara ambayo kapata mwananchi.

Mhe. Naibu Spika, tatizo linalosababisha umeme kuzimika mara kwa mara. Nafikiri swali hili nimeshalieleza katika jibu mama, kwamba ni matatizo ya miundombinu. Vile vile linasababishwa na *line* yetu ambayo iko baharini. Kwa sasa hivi ni *line* ambayo imeshakuwa chakavu kiasi ambacho haiwezi kuhimili kuchukuwa *megawatt* zinazostahiki kutumia wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa umekiri kuwa eneo la Chukwani limekabiliwa na uchakavu mkubwa wa ma-*transfomer*. Je, shirika lako ni lini litawaondoshea kadhia hii wananchi wa Chukwani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, shirika limejipanga vizuri na katika jitihada nafikiri wengi mnaziona linasita hapa na pale kwa ajili ya kufanya marekebisho. Vile vile tunaangalia sehemu zile ambazo *transformer* zimezidiwa zaidi, basi tunafanya marekebisho ya kufunga *transformer* kubwa ambazo zinaweza kuyaondoa matatizo hayo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Serikali imefanikiwa kupata majenereta yasiyopungua 32 yenye uwezo wa kuzalisha *megawatt 20.* Je, ni sababu gani za msingi zinazosababisha Zanzibar kukosa umeme karibu saa moja na nusu.

Je, jenereta hizo zimefungwa na zinafanyiwa huduma kwa muda gani na kwa gharama za kiasi gani kwa mwaka.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikiri kwamba majenereta yapo Zanzibar katika Shirika la Umeme Mtoni, majenereta 32. Majenereta yale yapo Zanzibar kwa ajili ya kuongeza nguvu za umeme tunaouchukua kutoka Bara kuja Zanzibar. Lakini kwa sasa hivi kutokana na gharama kubwa za mafuta ya majenereta hayo ndio maana hatuyatumii.

Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Mwakilishi avute subra pale tu tutakapopanga bajeti na hali itakaporidhisha, basi tutayatumia majenereta hayo kwa kuongeza nguvu za umeme Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri aliyoyatoa juu ya suala hili la matatizo yetu ya umeme.

Mhe. Naibu Spika, mimi napenda kuongeza tu kwamba hata kama majenereta yale yatafanya kazi yote, bado tukubaliane kwamba miundombinu na kufikisha umeme katika maeneo imechakaa sana. Kwa hivyo, ni lazima turekebishe waya zetu za umeme tuweke mpya zitakazoweza kuchukua mzigo wa umeme mkubwa ambao unahitajika katika mji huu wa Zanzibar hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika kwa sababu hiyo, ndio maana tuna miradi hii miwili ambayo ameitaja Mhe Naibu Waziri. Mradi wa kwanza ni kurekebisha masuala ya *transformer* kubwa, ndio maana ukipita Welezo tunajenga *transformer* pale kubwa kwa ajili ya Wilaya ya Kati na Kusini kote. Mpendae vile vile tunajenga mradi wa pili *transformer* nyengine kubwa, kwa ajili ya maeneo haya yaliyotajwa ya Mazizini, Chukwani na kwengineko ambako nako kuna matatizo. Lakini JICA wao wanafanya kazi ya mradi wa kusambaza hizo waya mpya ambazo zitasaidia kupunguza kabisa tatizo la umeme na kusema kweli hili suala litaondoka tukimaliza mradi huo, ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Nam. 73
Tatizo la Usafiri wa Baharini

Mhe. Salim Abdalla Hamad – Aliuliza:-

(a) Mhe. Waziri, serikali imejipanga vipi kukabiliana na tatizo la usafiri wa meli baina ya Pemba na Unguja.
(b) Je, ule mpango wa serikali wa kununua meli kubwa ya kusafirishia abiria baina ya visiwa hivyo upo.
(c) Kama serikali bado inao mpango huo utekelezaji wake utafanyika lini.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano – Aliuliza:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 73 lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Naibu Spika, katika kukabiliana na tatizo la usafiri wa meli baina ya Pemba na Unguja, serikali imeanza kuwasiliana na kampuni mbali mbali ziliomo ndani na nje ya

nchi, ambazo yameonesha nia ya kutaka kusaidiana na serikali pamoja na kushirikiana nazo.

Aidha, serikali imetoa ruhusa kwa kampuni hizo kufanya mazungumzo ya kuingia ubia na Shirika la Meli ili kuona uwezekano wa kusaidia kwa pamoja juu ya kugharamia ununuzi wa meli mpya kubwa ya abiria, kwa ajili ya usafiri salama baina ya Unguja na Pemba na sehemu nyengine za bandari ya mwambao wa Afrika ya Mashariki.

(b) Mhe. Naibu Spika, ule mpango wa kununua meli kubwa ya kusafirisha abiria baina ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba bado upo na ni wa lazima kwa serikali yetu.

(c) Mhe. Naibu Spika, taratibu za utekelezaji wa mpango huu bado zinaendelea kama tulivyoeleza katika jibu letu katika kifungu (a).

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru sana kwa kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, matatizo ya usafiri wa baharini baina ya Pemba na Unguja tunayajua ni magumu sana na bado hatujawa na vyombo vya uhakika. Mhe. Naibu Spika, hata juzi tu ile meli tuliyoitegemea ya Serengeti ilibidi ije Unguja kwa *engine* moja ni hatari. Tukizungumza hivi na ikatokea Mwenyezi Mungu akajaalia.

Mhe. Naibu Spika, wakati meli ya MV Mapinduzi imeuzwa na meli ya MV Maendeleo ambayo iko katika hali mbaya na tukasema iuzwe. Kwa nini kwa hatua ya mwanzo serikali haiiuzi hii meli ya pili, ikazalisha fedha za MV Mapinduzi tukapata angalau meli moja kwa kuongeza fedha iliyobakia.

Nasikia wapo wawekezaji kutoka nchi Fulani wamekuja hapa kwa kuwekeza kwa usafiri huo wa baharini na mpaka juzi walikuja, lakini nasikia bado hakujawa na muafaka.

Je, kuna mambo gani mazito ambayo ilibidi serikali isiafikiane na watu hawa tukiangalia umuhimu wa kupata usafiri wa uhakika wa kwenda kule Pemba na Unguja.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Ni kweli maelezo aliyoyatoa Mhe. Muwakilishi kwamba serikali iliuza meli ya MV. Mapinduzi na fedha hizo zipo hazina, kuhusu wazo lake la kusema tuuze Meli yetu ya MV. Maendeleo ili tuchanganye fedha hizo kwa ajili ya ununuzi wa meli ni fikra njema, lakini napenda kumjulisha Mhe. Muwakilishi na Baraza lako tukufu kwamba harama za ununzi wa meli ni gharama kubwa, mimi mwenyewe sitegemei kwamba fedha hizo zilizouziwa meli hiyo na fedha ambazo tutauza meli yetu ya maendeleo zitakizi ununuzi wa meli mpya.

Mhe. Naibu Spika, napenda tena kumhakikishia Mhe. Muwakilishi kwamba serikali ina mipango mzuri itakayothibitisha nia yake ya ununuzi wa meli hiyo mpya kama tulivyoeleza, nikweli Mhe. Naibu Spika, serikali kwa kupitia shirika la Meli kwa usimamizi wa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Katibu Mkuu Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu wameanza mazungumzo na kampuni ya *Farmes International* inayotoka Sudan Mjini Khartoum ambao wameonyesha nia ya kutaka kushirikiana na serikali katika ufumbuzi wa upatikanaji wa meli mpya kubwa kwa ajili ya uchukuzi wa abiria itakayokidhi safari za Unguja na Pemba pamoja na mwambao wa Afrika ya Mashariki.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi kuuliza suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa minara na maboya ni muhimu sana kwa usafiri wa meli hususan katika nyakati za usiku na kwa kuwa mnara wa Matumbilini pale Pemba pamoja na bora linaloingiza meli pale bandarini Mkoani hayafanyi kazi kwa kipindi kirefu jambo ambalo linapelekea *Ma-captain* kuingiza meli pale Mkoani katika hali ya kujaribu na kubahatisha jambo ambalo linasababisha usumbufu mkubwa kiasi ambacho juzi tu meli ya maendeleo iliingia katika ufukwe na kusababisha taharuki kubwa kwa abiria pamoja na familia zao.

a) Je, kuendelea kuyaacha vile vile ule mnara za Matumbini na lile boya ya pale si kuendelea kuhatarisha na kuita ajali nyengine hapa Zanzibar ya meli.
b) Je, kununua meli nyengine pamoja na kutengeneza kwanza ile miundombinu ya usafiri lipi bora kwanza kuanza kufanya.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri jibu suala la (b) kuhusu utaratibu wa maboya tafuta utaratibu mwengine Suala lilikuwa linahusu meli, kwa hivyo la maboya fanya utaratibu mwengine jibu suala (b).

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Ni kweli kwamba Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kwa kupitia usimamizi wa Shirika la Bandari tulifanya mabadiliko makubwa ya msingi katika vifaa hivi vinavyoongoza miendo wa vyombo vya baharini yaani minara pamoja na maboya, vifaa viliopo hivi sasa ni vifaa vinavyotumia mfumo wa gesi katika mfumo huu wa gesi kuna baadhi yao vyombo kama minara ni mfumo ambao ulikuwepo zamani lakini umebadilishwa katika *system* yao.

Ili kuweza kuendana na mahitaji halisi ya vyombo vya hivi sasa, utaratibu uliopo hivi sasa maboya yetu na minara vinaanya kazi vizuri na pale inapotokea hitlafu basi Shirika la Bandari kwa kushirikiana na wataalam wao wamekuwa wakifanya jitihada za haraka ili kukabiliana na matatizo hayo yanayojitokeza.
Napenda nimuhakikishie Mhe. Muwakilishi kama kuna matatizo yoyote yanayohusiana na minara ama maboya, Shirika letu la Bandari lipo tutalifanyia kazi suala hilo mara moja ili kunusuru majanga ya ajali ambayo ambayo yangeweza kutokezeshea.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa safari yake ndefu ya kwenda China mara mbili mfululizo na pia vile vile nimpe pole kwa machofu ya safari. Katika suala la msingi aliposema Mhe. Naibu Waziri aidha serikali imetoa ruhusa kwa kampuni hizo kufanya mazungumza na kuingia katika ubia na Shirika la Meli.
Mhe. Naibu Waziri utakubaliana nami kuwa Shirika la Meli halina uwezo wa kuendesha kitu hivi sasa. Mfano hai walikuwa na meli ya MV. Mapinduzi na MV. Maendeleo na wakati huo hakuna mtu yoyote mwenye biashara na meli hizo zimekufa. Je, kweli patakuwa pana ubia tena hapo wa kuendesha kweli shirika hilo wakati mlipewa meli mbili kuziendesha na wakati huo hakuna ushindani wa kibiashara, meli zipo peke yake na biashara ingalipo meli zote zimekufa hakuna kilichobakia kweli ipo haja ya kubakisha shirika tena hapo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Ni kweli kwamba kwa kipindi kirefu kabla ya serikali kuruhusu mfumo wa soko huria kwa kuwaruhusu wafanya biashara binafsi kuingia katika biashara hii ya usafiri wa vyombo vya baharini, biashara hiyo ilikuwa ikifanywa na chombo chetu cha Shirika la Meli na kweli tulikuwa na vyombo viwilili hivyo. Lakini serikali imeliona hilo na imetafakari na muda huu ninaozungumza tayari Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Miundo mbinu na mawasiliano imeshaandaa *business* Fulani mpya itakayoweza kuhuwisha shirika hili na kuliimarisha ili liendane na uzalishaji ambao utaleta tija kwa wananchi wa Zanzibar.

Hivyo basi napenda kumtoa hofu Mhe. Muwakilishi kwamba matatizo yaliyotokezea serikali imeshayaona na mpango huu inajipanga sasa serikali tutaweza kwenda vizuri pasina kutia hasara serikali wala wananchi wake.

Nam. 48

Migogoro ya ZFA

Mhe. Nassor Salim Ali - Aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni Rais wa Zanzibar katika hotuba yake ya kusherehekea mwaka mmoja toka kuchaguliwa kwake kuwa Rais wa Zanzibar alisikitishwa sana na hali ya migogoro inayoendelea katika michezo hususan chama cha mpira wa miguu hapa Zanzibar.

(a) Je, Wizara imechukua hatua gani kumaliza migogoro hiyo na kuondoa kadhia hiyo ya migogoro ndani ya chama cha mpira wa miguu Zanzibar.

(b) Je, Mhe. Waziri, Wizara yako haioni kuwa kuinyamazia migogoro na malumbano hayo kutaua kabisa mchezo huo hapa Zanzibar.

Mhe.Waziri Naibu wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu:-

Mhe. Spika, Nianze kwa kumuunga mkono muulizaji wa swali hili kwamba Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anasikitishwa sana na migogoro iliyoko katika Chama cha Mpira wa Miguu yaani ZFA lakini pia migogoro ya vyama vya michezo. Aidha, Wizara yangu pia na wananchi wa Zanzibar kwa ujumla hawafurahii hali ya kuwa na migogoro na mizozo isiyokwisha kwa vile inadhoofisha ustawi wa michezo wa mpira wa miguu lakini pia na michezo mengine. Baada ya Kutoa maelezo hayo, sasa naomba kujibu kama ifuatavyo:-

a) Katika kujaribu kumaliza mgogoro hiyo na kuondoa kadhia iliyopo ndani ya chama cha mpira wa miguu,Wizara ya Habari Utamaduni , Utalii na Michezo imechukua hatua kadhaa ikiwa ni pamoja na kukaa na uongozi wa ZFA mara kwa mara ili kuangalia baadhi za kasoro zinazokwamisha utendaji wao na kusababisha migogoro.

Baraza la taifa la Michezo kwa upande wake limekuwa karibú sana na uongozi wa ZFA katika Kutoa ushauri na kupitia mikataba Ambayo ZFA imeingia na wadau wengine. Aidha, kupitia Mrajis wa vyama vya michezo kazi ya kuipitia katiba na kanuni za ZFA inaendelea ili kubaini upungufu wa kisheria unaokwamisha utendaji wa kazi zao na kusababisha migogoro. Wizara yangu pia imechukua hatua za dharura za kuisaidia ZFA katika kutafuta wadhamini wa ligi kuu ya Zanzibar ili kupatikane utulivu katika kuiendesha ligi kuu ya Zanzibar
ambayo kwa kiasi kikubwa imekuwa ikichangia mizozo na migogoro katika uendeshaji wake.

b) Ni kweli kuinyamazia migogoro hiyo ni hatari na kutaweza kudhoofisha na kuua kabisa mchezo huo hapa Zanzibar, lakini kama nilivyoeleza katika jawabu (a) wizara haijakaa kimya, kazi ya kuishughulikia migogoro hiyo inaendelea katika ngazi mbali mbali tena kwa hatua nzuri sana na kwa busara kubwa na kwa kuzingatia sheria, imani yangu ni kwamba mizozo na migogoro hiyo itakwisha na mpira wa miguu utastawi na kuirejeshea nchi yetu jina zuri katika medali ya soka.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ya kukubali kwamba migogoro ndani ya ZFA ipo.

Mhe. Makamo wa Rais ambae alifanya kongamano pale katika hoteli ya Bwawani na yeye alithibitisha migogoro ile.
Je, ndani ya ZFA katika uongozi ule kutakuwa na Katibu ambae atateuliwa na Wizara na mpaka hivi sasa katika uongozi ule hakuna katibu ambae ameteuliwa ambayo ni moja kati ya sababu zinazochangia migogoro ile.

Je, Wizara haioni haya ya kuteua au kuajiri katibu kwa ajili ya kuondoa migogoro ile.

Mhe. Naibu Waziri wa Habarí, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Muwakilishi nakubaliana na wewe lakini kiongozi ambaye amechaguliwa kwa kweli ni kiongozi mzuri na ana ufanisi mzuri sana, nakuomba Mhe. Muwakilishi ikiwa kipindi kilicho pita wewe ulikuwa ni Katibu wa ZFA kwa mashirikiano yetu ya pamoja na Wizara tukiwa tuko pamoja na wewe tukae kitako ili tutoe nasaha na mambo yetu yaende vizuri ya ZFA.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza.

a) Lakini je, ni sababu zipi hasa zinazofanya chama cha Mpira wa Miguu hapa Zanzíbar kuwa na migogoro.
b) Ni lini hasa serikali itawachukulia hatua wale watu ambao wanajifanyia kazi kwenye chama cha Mpira kwa kazi zao binafsi sio kwa kazi za wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habarí, Utamaduni, Utalii na Michezo: Kama nilivyoeleza kwenye swali mama na juzi tu Mhe. Waziri alitoa ufafanuzi mzuri sana kuhusu ZFA kwa kweli tumeshakaa na uongozi na tumeshamaliza mambo yote tumuombe Mwenyezi Mungu tu atujaalie mambo haya yaende vizuri.

Suali lake la Pili Mhe. Mwakilishi haya masuali anayoyauliza tuko pamoja na wewe na wewe ukiwa ni mwanamke na mdau wa vyama vya michezo nakuomba Mhe. Muwakilishi kwa kushirikiana na mimi Naibu Waziri wa Abari mwanamke ili tuwe pamoja kwenye vikao hivyo kuendeleza michezo yetu Zanzíbar.

Mhe. Nassor Salah Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeze.
Kwanza niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibr kwa nia yake nzuri ya kuendeleza michezo ikiwa ni pamoja na huu mchezo wa mpira wa miguu, kwa kuwa ZFA imekuwa na mgogoro endelevu yaani usiomaliza na kwa kuwa fedha nyingi za serikali zinataka kuwekezwa katika kujenga uwanja wa kisasa, pamoja na kukarabati miwanja mingine.

a) Je, kuendelea kuiwacha ZFA kuendelea kugombana huku fedha za serikali tumeshaziwekeza kwenye viwanja na mambo mengine yanayohusi mpira wa miguu si uharibifu wa fedha za walipa kodi.

c) Kwa kuwa uzoefu unaonyesha wazi kwamba wenzetu hapo Tanzania Bara kuna kipindi waliizuia FAT na kuunda kamati maalum inayoshughulikia michezo. Kwa Zanzíbar huu sio wakati muafaka kwa kuwa ZFA hawataki kusikilizana ikaundwa kamati maalum ya kuongoza michezo hii, mpaka pale ZFA watakapojirekebisha.

Mhe. Waziri wa Habarí, Utamaduni, Utalii na Michezo: Masikitiko ambayo Mhe. Rais wa Zanzíbar ambayo aliyataja katika kusherehekea mwaka wake mmoja kwa kuteuliwa kwake, sisi katika Wizara ya Abarrí, Utamaduni, Utalii na Michezo tunachukulia kwamba ni agizo rasmi la kutatua migogoro katika ZFA, hatua ambazo Mhe. Naibu Waziri amezitaja katika suala lake mama ni hatua za uendeshaji wa kujaribu kutatua tatizo hili kwa wale ambao wamepewa majukumu ya kuendesha ZFA ili mpira wa miguu upate ustawi katika nchi yetu.

Ninachomuahidi Mhe. Muwakilishi kwamba kwa Mamlaka ambayo Mhe. Waziri anayeshughulikia michezo amepewa katika sheria na kanuni zake, tutahakikisha kwamba hatua nzito na ngumu zitachukuliwa ikibidi ili tatizo hili liondoke ili kuondoa uwezekano wa Mhe. Rais asije kusikitika tena wakati wa kusherehekea miaka yake miwili tangu kuchaguliwa kwake.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya 2012

(Kusomwa kwa mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili: Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilito Zanzíbar ya mwaka 2012.

Mhe. Spika, utafiti wa kilimo hapa Zanzíbar alianza tokea mwaka 1910 ambapo kwa wakati huo mkazo zaidi ilikuwa ni kuendeleza mazo ya biashara na utafiti wa mifugo, aidha tafiti kwa

wakati huo zilikuwa zikiendeshwa katika kituo cha kilimo Dunga na katika vituo vyengine vya Idara ya Kilimo ambavyo kwa wakati huo vilikuwa vikiitwa Idara ya Zaraa.

Katika mwaka 1933 Kituo cha Utafiti wa Kilimo kilianzishwa kikiwa ni kituo cha kwanza katika Uganda huu wa Afrika ya Mashariki, jukumu Kubwa kwa kituo hiki kilianza kwa uzalishaji wa mazao muhimu ya biashara hususan karafuu na badae kwa uzalishaji mazao muhimu zikiwemo Pili Pili, hiliki, manjano, kakao na kahawa. Utafiti wa mazao ya chakula haukupata msukumo unaostahiki kwa wakati huo kutokana na sera za kiuchumi zilizokuwepo.

Baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964 kituo kiliongeza majukumu ya kufanya tafiti za mazao ya chakula, mkazo zaidi ilikuwa ni kwenye zao la mpunga, mnamo miaka ya 1970 kazi za utafiti zilianza kuimarika kupitia miradi ya maendeleo iliyolenga kujenga uwezo wa kitaalam na kitaasisi katika kubadilisha na changamoto zinazokwamisha maendeleo ya kilimo. Katika kutekeleza azma hiyo sera miongozo na mipango ilitayarishwa ikiwemo mipango mikuu ya utafiti wa kilimo.

Mhe. Naibu Spika, mwaka 1981 utekelezaji wa mipango hiyo ulidhorota kutokana na kukosekana kwa taasisi zenye nguvu za kisheria na za kirasilimali katika kuratibu na kusimamia kazi za utafiti, kutokana na umuhimu huo wa taasisi Serikali ya awamu ya saba imetoa msukumo mkubwa sana kwa sekta ya utafiti wa kilimo hapa Zanzíbar ili kunyanyua hali ya kuanzisha taasisi ya utafiti wa kilimo.

Mhe. Naibu Spika, sababu zilizopelekea kutungwa kwa sheria za taasisi ya Utafiti wa kilimo Zanzíbar ni kama ifuatavyo.

1) Kuipa taasisi uwezo wa kisheria na kiutendaji katika kutoa huduma za utafiti wa mazao ya kilimo kwa lengo la kuongeza tija ili kukuza uchumi na kupunguza umasikini.

2) Kuwepo uwezo wa kisheria taasisi katika kuweka utaratibu wa kuvutia watafiti na kuongeza uwezo wa wataalam katika kufanya tafiti hizo.

Mhe. Spika, Mswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzíbar unapendekeza kuanzishwa kwa vyombo vifuatavyo:

Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzíbar imeanzishwa katika Mswada wa sheria hii kama inavyotajwa katika kifungu cha tatu cha Mswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, pia Baraza la Taasisi na utafiti wa kilimo Zanzíbar. Baraza la Utafiti wa Kilimo litakuwa ni chombo cha juu katika taasisi ambacho kitatoa maelekezo ya utendaji kazi wa taasisi.

Waheshimiwa Wajumbe kamati ya kitaalam ya utafiti wa kilimo inapendekezwa kuanzishwa kwenye Mswada huu kama inavyotajwa katika kufungu Nam. 12 cha Mswada huu ambacho wajumbe wake wanaorodheshwa katika kifungu hicho kidogo cha Pili.

Mhe. Naibu Spika, mambo mengine muhimu yanayozingatiwa katika Mswada wa Sheria hii ni haya yafuatayo:

- Kufanya uteuzi wa Mkurugenzi wa Taasisi
- Kufanya Uteuzi wa Ofisi Mkuu wa Utafiti wa Kilimo

Mhe. Naibu Spika, Mswada wa Sheria katika kifungu Nam. 11 inaelezea Uteuzi wa Osifi ya Mkuu wa Utafiti wa Kilimo ambaye atakuwa pia Msaidizi Mkuu wa Mkurugenzi katika kazi za utafiti katika taasisi hiyo.

Mhe. Naibu Spika, Mswada wa Sheria na Taasisi ya Kilimo Zanzíbar katika kifungu Nam. 15 kimeweka utaratibu unaohusiana na ufunguzi na ugunduzi endapo iwapo ugunduzi huo wowote utakaofanyika basi kwa maslahi ya umma, baraza litakuwa na utaratibu wa kununua, kuuza au kuchukua kutika kwa mgunduzi huyo.

Mhe. Naibu Spika, Mswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzíbar katika kifungu Nam. 24 na 25 inaweka makosa yanayohusiana na ukiukwaji wa sheria pamoja na adhabu zake.

Waheshimiwa Wajumbe natumai mmepata wasaa wa kupitia Mswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzíbar na tunatarajia kupata Maoni na michango kutoka kwennu na hatimae kuupitisha mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, na waheshimiwa wajumbe naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Salmin Awadh Salmin: (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo): Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo, kuhusu Mswada wa Sheria wa Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mhe. Spika, naomba nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mwenyeenzi Mungu kwa kutuwezesha kutufikisha hapa tukiendelea kuitumia neema yake ya uhai.Tumuombe Mwenyeezi Mungu aendelee kutujalia afya njema na maisha marefu.

Nikushukuru wewe Mheshimwa Spika kwa kunipatia nafasi hii ya mwanzo ili niweze kutoa maoni kwa niaba ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo yanayohusiana na Mswada uliombele yetu wa sheria ya kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo pamoja na mambo mengine yanayohusika na hayo.

Mhe. Spika**,** Naomba nitumie nafasi hii kumpongeza kwa dhati Mhe Mohamedraza Hassanali kwa kupata ridhaa ya Wananchi wa Jimbo la Uzini kwenye uchaguzi mdogo uliofanyika hivi karibuni.Tunamkaribisha katika utumishi huu wa uwakilishi wa wananchi tukimuombea kila la kheri, ujasiri na moyo wa subra.Tukimuahidi mashirikiano kutoka kwa wajumbe wote.

Mhe. Naibu Spika, niruhusu vile vile nitumie nafasi hii uliyonipa kwa kuwashukuru sana Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ambao kwa umoja wetu, tulishirikiana katika kuupitia mswada huu kifungu kwa kifungu.

Mhe. Naibu Spika, naomba niwataje Waheshimiwa hao kwa majina kama ifuatavyo:

1. Mhe. Salmin Awadh Salmin - Mwenyekiti
2. Mhe. Abdallah Mohamed Ali - Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Mahmoud Mohamed Mussa - Mjumbe
4. Mhe. Rufai Said Rufai - Mjumbe
5. Mhe. Raya Suleiman Hamad - Mjumbe
6. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma - Mjumbe
7. Mhe. Bikame Yussuf Hamad - Mjumbe
8. Ndg. Amour Mohammed Amour - Katibu
9. Ndg. Shemsa Maabad Mohamed - Katibu

Mhe. Naibu Spika, napenda nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshiwa Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe. Suleiman Othman Nyanga kwa kuwasilisha vyema Mswada huu katika Kamati yetu. Aidha na watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na wasaidizi wake kwa kuipa mashirikiano makubwa Kamati wakati ilipokuwa ikijadili maswada huu.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar kihistoria ndio Nchi ya mwanzo kwa ukanda wa Afrika Mashariki kuanzisha shughuli za utafiti unaohusu kilimo na mifugo.Umaarufu huu kwa wakati huo uliinua sana jina la Kizimbani likitajika kwa shughuli hiyo, na wataalamu wengi kutoka pembe nyingi Barani mwa Afrika wamezitumia tafiti zilizofanyika katika kituo hicho.

Mhe. Naibu Spika, hadhi na bahati hiyo tulioipata, kwa kweli haikuweza kuendelezwa kikamilifu, kwani tangu dhana hiyo ya utafiti ilipoanzishwa na laiti ingelitafsiriwa kivitendo, leo hii tungekuwa na Taasisi yenye hadhi ya chuo kikuu.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile bado tuna lengo la kukuza uchumi wetu kupitia kilimo, basi suala la kuwa na chombo kama hichi ni muhimu sana. Bila ya shaka huu utakuwa ni ufumbuzi sahihi wa kukabiliana na changamoto zinazoikabili sekta ya kilimo

Mhe. Naibu Spika, tunaelewa kwamba eneo la ardhi yetu inayofaa kwa kilimo ni dogo, ambalo bila ya kulimwa kitaalamu basi suala la kujiinua kiuchumi kwa kutegemea kilimo litakuwa kama ndoto.Utafiti wa aina za udongo, aina za mbegu au mimea inayotaka kuoteshwa ndio utakaotoa majibu ya matumizi bora na sahihi ya rasilimali hiyo ya ardhi.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa 1981, Mpango Mkuu wa Utafiti *(Agricultural Research Master Plan)* ulitayarishwa. Hata hivyo mpango huo ulizorota kutokana na kukosekana kwa taasisi yenye nguvu ya kisheria na kirasilimali katika suala zima la kuratibu na kusimamia kazi za kiutafiti.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu inakubaliana kwa kiasi kikubwa juu ya sababu za msingi zinazopelekea haja ya kutunga sheria ya uanzishwaji wa Sheria ya utafiti wa kilimo Zanzibar.Kwa kuamini kwamba Sheria hiyo itaweza kuipa Taasisi nguvu za kiutendaji katika lengo lake la kutoa huduma za kiutafiti wa mazao ya kilimo ili kuongeza tija kwa wakulima.Aidha kwa uwezo huo huo taasisi hiyo inayoanzishwa inaweza kujenga mvuto kwa

watafiti na kuongeza uwezo wao kwa kuweka utaratibu mzuri wa ugunduzi, na hivyo maslahi ya mgunduzi yatalindwa.

Mhe. Naibu Spika, Uongozi wa Taasisi hiyo unajumuisha na kuundwa kwa Baraza la Taasisi, ambalo litakuwa ni chombo cha juu kitakachotoa maelekezo ya utendaji kama yalivyoelekezwa kwenye kifungu cha sita cha sheria inayokusudiwa kutungwa. Sambamba na hilo, kifungu cha kumi na mbili cha mswada huu kinaanzisha Kamati itakayojulikana kama Kamati ya kitaalamu ya Taasisi ya Utafiti wa kilimo. Majukumu na kazi za vyombo pamoja na yale ya Mkurugenzi wa Taasisi yameelezwa wazi kwenye mswada huu. Kwa hiyo basi; kamati yetu inasisitiza utekelezaji mzuri wa majukumu hayo, ili baadae kusije kuwa na mgongano utakaosababishwa na chombo kimoja kufanya kazi ya mwengine.

Mhe. Naibu Spika, mara nyingi tumekuwa tukilalamika juu ya kukimbiwa na wataalamu wetu wazalendo, ambapo wale wanaobakia hatuwatunzi katika stahiki yao.Kamati yetu inaiomba serikali iwaangalie kwa jicho la rehema wataalamu wetu ili waendelee kuwa na moyo wa kuutumia ujuzi wao kwa faida ya Nchi yetu.Aidha kwa mnasaba huo huo, Serikali haina budi kutenga fungu la fedha kwa ajili ya mafunzo ya wataalamu hao, ili ujuzi wao uwe unaendana na wakati na mazingira yaliyopo.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha kumi na sita kifungu kidogo cha pili cha mswada huu, kinampa nafasi Waziri kutoa idhini kwa Taasisi kuweza kumlipa mtaalamu, mgunduzi aliyefanya ugunduzi au ubunifu wakati wa kutekeleza kazi za utafiti, kulipwa bahashishi au mrabaha kwa kazi hiyo aliyoifanya.Tunachokiomba jambo hili litakapo tokezea, basi lifanyike kama ambavyo sheria imeeleza.Aidha malipo hayo yawe katika kiwango kinacholingana na kazi yenyewe, ili kiweze kushajihisha wataalamu waweze kuwa wagunduzi na wabunifu wazuri.Kwa maana hiyo basi, ni vyema Taasisi ikatenga fungu kwa madhumuni hayo, ili itakapotokezea haja hiyo kusiwe na urasimu wa kulifanikisha suala hilo la malipo.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu imekubaliana na Mhe.Waziri kufanyika kwa baadhi ya marekebisho ambayo mengine ni makosa ya uandishi *(spelling mistakes)*, kuongeza kijifungu kidogo cha 24 (2) (d) ambapo awali kifungu cha 24 (2) (c) ndicho kilichokuwa ni cha mwisho, aidha kwenye jadweli linalohusu Wizara zinazohusika na mambo ya kilimo zimeongezwa wizara nyengine tatu kama tulivyoziainisha katika marekebisho ya Mswada waliokabidhiwa Wajumbe.

Mhe. Naibu Spika, kamati yetu imeuunga mkono mswada huu na tunawaomba Wajumbe wenzetu waujadili na wauchangie hatimae waukubali ili iwe ni sheria. Mhe naibu Spika, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Magomeni naunga mkono mswada huu. Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia fursa hii kueleza machache kuhusu Mswada uliopo mbele yetu. Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kutufikisha siku hii ya leo tukiwa hai. Maana baada ya kumaliza wiki nzima leo tumekuja hapa Barazani tukiwa hai tena bila ya kukamatwa mkono. Hii ni neema kubwa aliyotujaalia Mwenyezi Mungu na inabidi tumshukuru.

Mara baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu nadhani nitakuwa mchache wa fadhila kama sikuitumia fursa hii na wewe kukushukuru kwa kunipatia fursa angalau kutia *nyalio* kuhusu hii hoja iliyokuwepo mbele yetu. Kabla ya kwenda kwenye hoja naomba uniruhusu nitoe mkono wa pole, kwa wale waliokuwepo katika tasnia hii ya sanaa kwa kumpoteza ngwiji katika mambo ya sanaa Charles Kanumba, Mwenyezi Mungu amlipe kwa mujibu wa matendo yake.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo haya mafupi, naomba moja kwa moja sasa niende katika hoja. Mhe. Naibu Spika, Mswada uliokuwepo mbele yetu ni wa Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo. Kwanza naomba nitumie fursa hii kuishukuru serikali kwa kuweza kuleta Mswada huu mbele yetu, kama kuna jambo linalohitajika sasa hivi katika nchi yetu ni hii taasisi ambayo itafanya tafiti katika masuala ya kilimo, kwa kweli mimi nimefarijika sana.

Mhe. Naibu Spika, hapo siku za nyuma tulikuwa tunasikia tu nadharia za kilimo kupitia kwa wanasiasa, "siasa ni kilimo", "ujamaa na kujitegemea". Maneno mengi tu lakini ni ya kisiasa, hatuoni maendeleo yake. Hapa Zanzibar tuliletewa nadharia ya Ngoro na Bwana Aboud Jumbe Mwinyi, Mwenyezi Mungu ampe maisha marefu. Alikuwa ana nadharia nzuri ya kulima muhogo kwa ngoro, lakini wataalamu hawakufanya tafiti kumsaidia yule mzee, matokeo yake ngoro imefeli, hatukupata maendeleo yoyote.

Mwanasiasa huyo huyo Bwana Aboud Jumbe hapa akaja na nadharia ya kilimo cha mipira, mashamba ya mikarafuu tukaikata kule Pemba, tukapanda mipira na kweli hadi leo hii mipira ipo lakini tija inayopatikana katika mashamba yale ni ndogo sana, kiasi ambacho haisaidii wakulima wala taifa letu hili. Kwa hivyo nadhani kuja kwa taasisi hii tena naomba waheshimiwa Wawakilishi sote tuiunge mkono hoja hii, ianzishwe hii taasisi kusudi iweze kutukomboa. Tunaambiwa kwamba kilimo ndio uti wa mgongo wa nchi yetu. Ikiwa uti wa mgongo unauma hauna tiba jamani kweli utaweza kutembea, utaweza kwenda kazini? Mimi naamini ikianzishwa taasisi hii itakuwa ni daktari wa kutibu "uti wa mgongo wa taifa hili" yaani hichi kilimo.

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba katika taifa letu tulikuwa tunataja nadharia ya kilimo, lakini ukiiangalia bajeti ya nchi ilikuwa haitengwi kuhusiana na mambo ya utafiti ilikuwa hakuna. Mataifa mengi yaliyoendelea katika ulimwengu basi yalianzia uchumi wake kupitia kilimo, kwa mfano, Marekani, Japani, waliendelea mpaka sasa wamekuwa na viwanda vya kimataifa, lakini walipita kwenye kilimo. Katika karne ya 17, 18, Wamarekani na Wajapani waliongoza katika soko la dunia kwa kuuza mchele. Lakini 20% ya *total budget* ya nchi zao ilikuwa inapelekwa katika tafiti, kabisa Mheshimiwa.

Nakumbuka pale Wajapani walikuwa wakiitwa *Japanism Pishori* katika soko la dunia kwa wingi katika *Century* ya 10, lakini walikuwa wanafanya tafiti. Kwa mfano, katika ule Mji wa *Korosawa* pale Japani wana taaluma katika kuangalia uzalishaji wa mchele kwa *per unit area*, walifanya utafiti. Bwana mmoja anaitwa *Gibberella Fujikoroi* katika mwaka wa 1728, katika tafiti zake aliona katika mji wa Korosawa pale Japani, aligundua kwa *Gibberellin plant hormones*, inaitwa Gibberellin. Huyu Gibberellin ni *derivative name* ya huyu Gibberella Fujikoroi yaani kampa jina kutokana na jina lake yeye mtafiti.

Baada ya kumgundua *phytohormone* wenye miti wakaanza kumu *apply* katika sehemu ya miche ya mipunga, mbegu moja unayoipanda katika mpunga mche wake unapotoka ikiwa utamuweka Gibberellin huyo, basi itatoa viji *tectives* wanaitwa *circuse* nyingi sana yaani mche mmoja unaweza ukatoa miche mingi na ukapata mpunga mwingi katika *unit area* ndogo.

Hawa Wajapani wakaongoza sana kwa kuzalisha mchele, kwa sababu 20% ya bajeti yao waliingiza huko. Lakini sisi tumo katika mikarafuu na minazi, tangu miaka 60 tunategemea mkarafuu na mnazi kwa kuleta maslahi ya nchi. Mkarafuu uliopo hivi sasa ni ule ule wa karne ya 18 mpaka wanawake sasa hawawezi tena kupanda kwa sababu imekwenda juu sana. Ni tatizo kwenda kuchuma karafuu.

Mimi naamini kama ingalikuwa fedha inatumika kwenye tafiti, naamini wataalamu wangekwisha kuufanyia utafiti mkaruu huu badala ya kwenda juu ukawa unatoa matawi mengi katika sehemu za chini, na matokeo yake uzalishaji ukawa mkubwa katika nchi.Lakini sisi Bwana Aboud Jumbe alipoona unakwenda juu akaleta *dia-betes.* Wataalamu wakamuachia tu mwanasiasa, tena yule ni mwalimu katika fani ya elimu ya viumbe, tangu lini na mambo haya ya kilimo, akaleta *dai-betes*, hapa mikarafuu tukaanza kuipiga shoka ukenda juu unaambiwa utibu, unapigwa shoka na lami kidogo, eti ndio matibabu.

Wataalamu hawana chombo cha kufanyia kazi, hakuna bajeti inayotengwa katika nchi kwa ajili ya tafiti, matokeo yake ukiangalia wizara ya kilimo kama ni *dampo* la wataalamu sasa hivi, wengine wameanza kutukimbia Mhe. Naibu Spika. Naamini kuwepo kwa chombo hiki kitawafanya wataalamu wa wizara ya kilimo ambao sasa tunao wengi, wakaweza kutufanyia tafiti na matokeo yake kweli kilimo kikapata tiba na kuwa kweli ni uti wa mgongo wa uchumi wetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi naamini kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar si tatizo la bajeti linalowakwaza, lakini ni ubakhili. Hii serikali bakhili kweli kweli, hii SMZ ni bakhili sana na ubakhili bila ya malengo ni tatizo Mhe. Naibu Spika, ubakhili bila ya malengo haufai.

Mhe. Naibu Spika, kuna kabila moja pale Pemba hawa watu ni mabakhili sana, ni kabila la Kiarabu sitaki niliseme kwa sababu naweza nikakosa mke pale. Hawa ni mabakhili sana lakini walikuwa na malengo, ubakhili wao walikuwa kuna roda na bichwa la nguru, ikifika wakati wa mchana zinakatwa tungule, vitunguu, vinawekwa kwenye sufuria, linateremshwa kwa roda bichwa la nguru, linachemka halafu linapandishwa tena juu watu wanatoelea harufu ya nguru linapandishwa tena juu, halafu linapandishwa tena juu. Lakini walikuwa wana malengo.

Hivi sasa mji wa ChakeChake ndio wanaomiliki ghorofa nyingi kubwa, *Show rooms* pale Dar-es-Salaam zile kubwa kubwa zinamilikiwa na wao. Hivi sasa hivi ukija hapa Chukwani, kabila hilo ndilo linamiliki nyumba kubwa kubwa. Kwa sababu walikuwa wana malengo walifanya ubakhili hivi sasa wameshapata wanatumia. Sisi ubakhili wetu hauna malengo. Tutaendelea kula nguru mpaka lini, sisi kama Zanzibar jamani. Serikali yetu kila siku haikui ni kokoto, kokoto ndiyo iliyokuwa haikui. Mimi nadhani hivi sasa tu *turn mind* zetu, Mswada huu utakapokuja naamini kilimo kinaweza kutukomboa.

Pale Kibokwa, pamoja na bonde la mpunga la vitongoji kama tutalitumilia kwa kilimo cha utafitii basi litalisha Zanzibar nzima pamoja na kusafirisha. Ni lazima tutumie fedha katika hili, ili kuona kwamba katika nchi yetu bonde la Mfubaa la pale Vitongoji nakuhakikishia ikiwa tutawapelekea watafiti, basi Mfubaa tu liliopo Vitongoji litalisha Zanzibar nzima. SMZ wametuletea mpango wa Mapinduzi ya kilimo, unatudanganya kila siku Mhe. Naibu Spika.

Hivi sasa mapinduzi ya kilimo wakulima hawajalimiwa mpaka sasa hivi ninavyokwambia. Mapinduzi ya kilimo hiyo nerika haipatikani Vitongoji, watu hawajalimiwa, Furaha, Uwandani watu hawajalimiwa katika jimbo la Wawi, mapinduzi ya kilimo hayo yako wapi Mheshimiwa. Mimi imani yangu kwamba tukiupitisha Mswada huu haya mapinduzi ya kilimo ambayo tunayapitisha hapa basi inaweza yakapatikana kweli mapinduzi ya kilimo.

Mhe. Naibu Spika, tukijaaliwa wiki ijayo niende nikaishtaki Wizara ya Kilimo, kwa sababu wamechukua pesa za wakulima hawajalimiwa mpaka sasa hivi. Watu wa Machomane, jirani zake Mohammed Aboud, Mahakamani tutakwenda kuishtaki Wizara ya Kilimo, kwa sababu wameshindwa kutuletea mapinduzi ya kilimo hawajatulimia, hatuna dawa za magugu, dawa za magugu hazipatikani, tuendelee kuwaacha tu, tutakwenda Mahakamani.

Mhe. Naibu Spika, mimi naamini katika hili ikiwa tutafanya *scientific agricultural system* ndani ya nchi yetu, basi mkarafuu unaweza ukakidhi haja, mnazi unaweza ukakidhi haja, Mzee Aboud Jumbe alijitahidi sana lazima tumsifu. Alileta *high breed* ya minazi kwamba hii *East African tall* tuikate yote.

Alikuwa asaidiwe yule mzee, yeye keshaleta miche chotara ile ya minazi, na hii *East African tall* ipo lakini *life span* yake ni ndogo, hakusaidiwa. Matokeo yake ile chotara imekufa, sasa bado tunayo ile ile minazi mirefu ambayo nayo vile vile inatutoka. Nadhani tutakapoleta hili basi suala zima la ukombozi wa kilimo utasaidiwa na utafiti huu, na tija itapatikana nzuri katika nchi yetu.

Mhe. Spika, sasa niende katika ukurasa wa 16 na 17 katika suala la ufafanuzi. Anasema utafiti wa kilimo maana yake ni utafiti wa kitaalamu unaohusiana na kilimo na mazingira, unaojumuisha uchapishaji na usambazaji wa zana na tafiti. Tunaomba sana tuupitishe huu Mswada, tena tusiwe na wasi wasi tuupitisheni kusudi taasisi ianze, kama kuna tatizo linahitajiwa kufanyiwa utafiti katika nchi hii lifanyiwe. Kuna tatizo kubwa linalolikumba nchi yetu basi ni mazingira, tena ya aina zote. Kuna mazingira ya aina tatu.

- Kuna mazingira ya maji
- Kuna mazingira ya ardhi
- Kuna mazingira ya hewa.

Mazingira haya yote yana matatizo.Wana siasa wanaachiwa wanafanya wanavyotaka pamoja na wafanyabiashara katika nchi hii, kwa sababu hapana tafiti zinazofanywa juu ya mazingira. Hivi sasa pale kwetu Wawi Mhe. Naibu Spika, pamejengwa kiwanda cha makonyo. Kweli pale panatoka waasisi kina biti Vihimu, Mhe. Mohammed Aboud anatoka pale, Zaidi Yakuti anatoka pale. Sisi tuliwashauri kwamba hichi kiwanda tukijengeeni Makaani karibu na pwani. Basi wakaingia wana siasa pale wakasema kijengwe pale. Kwa sababu hapakuwa na chombo wakaachiwa wanasiasa. Kikajengwa kiwanda pale, hivi sasa ni tatizo kubwa kwa afya za

wananchi. Mazingira ya hewa ni mabaya sana. Hivi sasa kama uzalishaji wa mafuta ya makonyo ukifanywa pale, kama utaweka ndoo basi kuanzia usiku mpaka asubuhi ukija kuna ukungu mkubwa kwenye ndoo ya maji. Sasa yakiingia kwenye mapafu je, hilo ni tatizo kubwa.

Mimi nadhani tuipitisheni taasisi hii ili maamuzi ya wanasiasa pamoja na wanafanyabiashara yasifanyike, yafanywe maamuzi ya kitaalamu. Nadhani ikija hii huenda kiwanda cha makonyo Mhe. Mohammed Aboud akakubali tukipeleke Makaame kule, ili kusudi wananchi wasiathirike na mazingira hayo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani ni kukosekana kwa chombo madhubuti, kumesababisha hata mfumo wetu wa maji machafu kuwa tatizo.Mfano hivi sasa kuna baadhi ya maeneo *sewage system* zimetupwa tu baharini. Hoteli juzi tulisema zinajengwa ndani ya bahari jambo ambalo mazingira ya bahari yanaharibika sana. Sasa ndani ya Mswada huu kumezungumzwa katika ukurasa wa 18 ibara ya 5 kifungu kidogo cha 1(b).Kifungu hicho kinasema "kazi na uwezo wa taasisi, kufanya utafiti na kutumia utafiti wa kilimo kwenye mazao na mazingira, mifugo, misitu, uvuvi, ardhi, maji, wadudu, maradhi na aina zote zinazohusiana na mambo hayo na mfumo wa viumbe na mazingira".
Sasa ninachotaka kuzungumza ni mfumo wa viumbe na mazingira. Mheshimiwa ndani ya mazingira kuna kutegemeana kwa chakula baina ya viumbe. Sasa wewe unaharibu mazingira ya maji kwa kujenga hoteli ndani ya maji. Inaelekeza *sewage system* ndani ya maji, sasa maji ukiweka takataka pale ukimwaga sumu, wanakula samaki, samaki wanaathirika na sisi tunakula samaki, tunaathirika sasa kule *inter dependence of food,* jambo ambalo kuna ule mnyororo wa chakula. Tatizo Mheshimiwa tumekosa sio tu hichi chombo lakini kwa sababu sheria ipo ya kusimamia hizi sheria zetu kuhusu ujenzi.

Mimi naamini kama chombo hiki kama kitakuja, basi hili tatizo la uharibufu wa mazingira ya maji kupitia *sewage system* litaondoka. Nashauri tufanyeni mambo ya kuyatibu maji yetu, kabla ya kuyapeleka kule. Watu wengi ukiwapima sasa hivi wana matatizo ya *pressure*, kumbe ni kuchezea changu waliokwisha athirika, tunakula dagaa lililoathirika, tunapata mambo kama haya. Naamini ikija hii taasisi basi kutakuwa na udhibiti wa mambo haya ya mazingira.

Mhe. Naibu Spika, serikali nayo inasababisha kuharibu mazingira. Juzi hapa tulipata taarifa kutoka kwa Mhe. Waziri Baraza lililopita kwamba ameua kunguru laki 5. Sasa unapoua kunguru laki 5 kimazingira ni tatizo, wanasema wanafanya *dropping* kuharibu mazingira. Ilikuwa wale watumiwe sio *chemical means* katika kuwaua, wajaribu kupeleka *natural enemy,* maadui wawaue ili wa- *balance* ile biological *equilibrium* katika eneo. Wamewaua wadudu wale lakini hapa Unguja Mjini hapalimwi, lakini ingelikuwa tuna mashamba basi nakuhakikishia tungepata tatizo jengine la wadudu wanaoshambulia mazao ya mpunga.

Jengine ni kwamba utafiti wa kilimo unahitajika sana hususan katika upandaji wa miti. Tumeshajihishwa na serikali tupande miti ili kulinda mazingira. Lakini hakuna utafiti uliofanywa. Matokeo yake tumepanda mivinje na mikaratusi. Hapa juzi nilisikitika sana Mhe. Waziri alivyokuwa anajibu kwamba haina madhara, lakini kitaalamu mivinje ina *high transpiration rate,* inafyonza maji kwa wingi kwenye ardhi na kuyatupa katika hewa kwa njia inayoitwa *transpiration*. Sasa ukitwambia haina matatizo, sisi wana taaluma tunapata shida sana, unatwambia mivinje haina matatizo, wakati wenzetu Bara wanaanza kuikata mikaratusi katika

vyanzo vya maji wewe unatwambia hivi. Mimi nadhani mambo kama haya yanaweza tukapata nafauu.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kuwaomba wenzangu kwamba mswada huu ni mzuri na utakuwa mkombozi wetu na kama uti wa mgongo wetu ndio kilimo na sasa hivi ni kwamba uti wa mgongo unaumwa, hivyo dawa pekee ya uti wa mgongo huu ni kupata taasisi itakayofanya tafiti za kilimo kuhusu mazao yetu yakaweza kupatikana. Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwamba hivi sasa kutokana na kukosekana hili yale mapinduzi ya kilimo yamefeli moja kwa moja, hakuna nerika, hakuna watu wa kulimiwa wala hakuna mbegu iliyopatikana katika maeneo yetu. Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja mia kwa mia.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii yakuweza kutoa mawazo yangu katika kuanzishwa Mswada huu wa Sheria ya Utafiti wa Kilimo. Mhe. Naibu Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu Subhana Wataala aliyenijaalia kuwa katika hali ya uzima na afya njema nikasimama mbele ya Baraza lako tukufu kutoa mawazo yangu. Pia nikushukuru na wewe uliyenipa nafasi hii kwa kutoa mawazo yangu katika taasisi hii itakayoanzishwa ya utafiti wa kilimo.

Mhe. Naibu Spika, kufanya utafiti juu ya kila jambo hapa ulimwenguni ni jambo zuri sana na huleta faida kwa wanadamu kujua jinsi Mwenyezi Mungu alivyoumba dunia na kuweka mambo kwa mpangilio mzuri sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa muda mrefu nchi yetu imekuwa ikifanya utafiti katika mambo mbali mbali juu ya ardhi na kujikita zaidi kwenye kilimo na ufugaji. Lakini bado bahari na fukwe zetu hapa Zanzibar hazijafanyiwa utafiti yakinifu hasa uvuvi pamoja na mazingira ya nchi na baharini ikiwemo miamba, matumbawe na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, mimi katika mswada huu niende moja kwa moja kwenye kifungu cha 5 (1a-c) naomba kunukuu.

Mhe. Naibu Spika, mimi katika mswada huu niende moja kwa moja kwenye kifungu cha 5 (1a-c) naomba kunukuu.

Kifungu cha 5 (1a).

(a) Kuendeleza, na kukuza kazi ya utafiti wa kilimo Zanzibar.
(b) Kufanya utafiti na kutumia utafiti wa kilimo kwenye mazao, mazingira, mifugo, misitu, uvuvi, ardhi, maji, wadudu, maradhi na aina zote zinazohusiana na mambo hayo na mfumo wa viumbe na mazingira.
(c) Kufanya na kutumia utafiti wa kilimo utakaozidisha uzalishaji kwa kutumia usimamizi wa kisayansi katika mazao, mazingira, wanyama, misitu, uvuvi, ardhi, maji na kuendeleza teknolojia inayofaa ikijumuisha aina mpya na udhibiti wa wadudu na maradhi.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme kuanzishwa kwa taasisi hii ni jambo jema sana kwa sababu bila ya kufanya utafiti utakuwa huwezi kujua jambo, lakini ukifanya utafiti utayagundua mengi

na utaweza kuyafanyia kazi. Lakini kama nilivyosema naomba kila palipotajwa neno kilimo basi na uvuvi utajwe. Mhe. Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu ya msingi kwani hizi shughuli za kilimo zinategemea na mambo ya uvuvi vile vile, watu wakishalima wanategemea kula samaki kwa wingi basi ni jambo jema panapotajwa neno kilimo pakatajwa na uvuvi, kwani hii ni wizara husika.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli jambo hili ni zuri na sisi tunaliunga mkono kwa nguvu zote na nawashauri Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuichangie na tukiipitisha sheria hii ambayo itakuwa na manufaa kwa wananchi wetu wote. Mhe. Naibu Spika, kama alivyozungumza mtanguliaji aliyepita kuwa pamoja na ardhi yetu ndogo, lakini kama itafanyiwa utafiti basi kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tunaweza tukapata mambo mengi ya kilimo.

Kama vile upande wa Mashariki kule kisiwani Kojani kuna sehemu inaitwa Ng'ambwa watu wengi wanalima, lakini jambo likiwa halijafanyiwa utafiti na wakaelekezwa wananchi wanaofanya mambo ya kilimo. Mhe. Naibu Spika, tunaomba sheria hii itakapopitishwa hapa utafiti uwe ni yakinifu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nikiendelea na mchango wangu huu kuna mambo ya uvuvi, mambo ya uvuvi kwa kweli ni vyema yakafanyiwa utafiti wa kina kwani jambo hili limekuwa ni kikwazo sana kwa wadau wetu ambao ni wavuvi huwa wanapata tabu sana. Kama litafanyiwa utafiti basi huenda mambo yakawa mazuri kwa wananchi wetu wanaofanya kazi hii ya uvuvi. Kwa nini niseme hivyo? Kwani zipo sheria zetu hapa za uvuvi lakini ukiangalia sana pamoja na nia nzuri ya serikali kumkomboa mvuvi kwa vyombo vya kisasa, ni kwamba bado kuna vikwazo vinamkwamisha mvuvi.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu leo imekuja sheria hii tunaomba sheria hii ijikite sana kufanya utafiti ndani ya bahari tena uende vizuri kabisa. Mimi pia ninashauri katika mambo haya ya uvuvi basi yafanyiwe utafiti wa kina kwa sababu tukitaja neno nyavu, ni kwamba ziko za aina nyingi, ziko nyavu za macho madogo, ziko nyavu za macho makubwa, ziko za kuvulia samaki wa aina mbali mbali kwani kila samaki ana mtego wake wa kuvuliwa. Lakini pale sisi huwa tunasema tunaharibu mazingira na hatujui ni mazingira ya aina gani yanayoharibiwa.

Kwa mfano, mimi naweza kusoma hapa lakini ikawa macho yangu hayaoni vizuri hivyo nikachukua miwani ya macho yakanisaidia kwa kusoma. Lakini leo mvuvi akichukua kioo cha kuzamia anaambiwa anaharibu mazingira, hivyo anaharibu mazingira ya aina gani tunaomba utafiti ufanywe wa kina.

Mhe. Naibu Spika, mvuvi akichukua kiatu cha kuogelea anaambiwa anaharibu mazingira ni lazima tupate utafiti wa kina kwa sababu kioo kinamsaidia mvuvi kufanya kazi zake anapokuwa baharini kwa kuona kila kitu ndani ya bahari. Mhe. Naibu Spika, lakini baada ya muda kioo hiki kinakuwa haramu kwa mvuvi, lakini kwa mtalii ni halali basi tunaomba ufanywe utafiti wa kina.

Mhe. Naibu Spika, pia kuhusu viatu vya kuogelea huwa vinamsaidia mvuvi katika shughuli zake pamoja na kumkinga na samaki wakali wa baharini. Lakini leo ukiziachilia hizi nyayo huwa vinangara ndani ya bahari vibaya sana inakuwa ni chambo cha samaki unaweza ukapigwa dharuba moja tu na imeshatokezea hivyo. Mhe. Naibu Spika, alikuwepo Mkojani wetu mmoja

kipindi kilichopita pale Misali alikuwa anavizia kutafuta samaki basi alikatwa na papa vibaya sana na hatimae alipoteza maisha. Kwa hivyo, kwa vile sheria hii imeundwa tunaomba ifanye utafiti wa kina kabisa ili wajue mazingira yaliyokuwa baharini.

Mhe. Naibu Spika, mimi nasema kwamba bado wavuvi wana hali ngumu hawafanyi kazi zao kwa umakini kutokana na sheria jinsi inavyowabana, lakini kwa vile umekuja utafiti basi utafiti huo uje kufanywa kwa kina. Mhe. Naibu Spika, ukiangalia hapa katika ukurasa wa 19 katika kifungu cha 5 (j-k).

(j) Kuwapatia wakulima taarifa muhimu za shughuli zao za kilimo ili waweze kufanya kazi zao kwa umakini na ubora.

Mhe. Naibu Spika, unaona hapo mkulima anaambiwa hivyo lakini mvuvi hajalengwa sijui ni sababu zipi zinazosababisha mvuvi asilengwe na hizi zinategemeana kabisa unapolima lazima na wavuvi wawepo na nchi yetu ni ya kisiwa, hivyo wavuvi kuondoka ni ajabu sana. Kwa mfano, hapa tumepiga marufuku mifuko ya plastiki isitumiwe lakini tumeleta mifuko mbadala japokuwa ni bei mbaya. Leo unamwambia mvuvi usitumie chombo hiki na wala hujampa mbadala hivyo itakuwa bado hujamtendea haki, na kama hujamtendea haki ni sawa sawa na kusema kama uvuvi Zanzibar hakuna. Lakini ukimwambia leo acha hiki na ufanye hiki basi itakuwa umeshamtendea haki, akifanya vyenginevyo itakuwa ni kosa na atachukuliwa hatua za kisheria zilizoanishwa.

Mhe. Naibu Spika, tunapozungumzia chupa ya *oxygen* ni kwamba inamuwezesha mvuvi kupata pumzi anapofanya kazi zake za uvuvi, lakini leo mvuvi yule anaambiwa chupa ya *oxygen*, lakini mtalii akija hapa chupa hiyo hiyo ya *oxygen* anaitumia. Kwa hivyo, hii sheria ni kwa wazalendo tu wageni haiwakumbi? Tunaomba Mhe. Naibu Waziri ufanywe utafiti wa kina na utafiti yakinifu ili kila mtu ajue kupata haki zake za kimsingi hasa kwa wazalendo.

Mhe. Naibu Spika, mvuvi huyu huyu anapotumia mchokonoo anaambiwa asivuwe, hivi pweza utamvua kwa kitu gani. Mhe. Naibu Spika, kule kwetu Kojani tunauita uchomo au njoro hiyo ndio silaha ya pweza anayovuliwa, hivi ni sawa sawa na kupiga marufuku kama pweza asivuliwe. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu pweza anapozama lazima ukamvue kwa kutumia mchokonoo ndio atatoka, lazima tupate utafiti yakinifu tutayajua haya mambo na tutayawekea sheria ambazo ni nzuri.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli jambo hili ni zuri kama nilivyosema lakini lifanyiwe utafiti wa kutosha, na atoke muasisi aliyekuwa hahusiani na mambo ya serikali lakini awe katika mambo ya kilimo kwa ajili ya kufanyia utafiti jambo hili. Mimi nasema hawa watafiti wawe wawili, awepo wa kilimo na awepo wa uvuvi. Mhe. Naibu Spika, mimi nashauri katika hapa tunayo jumuiya nzuri ya maendeleo ya wavuvi wa Kojani atoe kinara awepo katika mambo haya ili atakapokwenda katika *field* kule awe ni mtu wa mwanzo kuzamia na kufanya huo utafiti. Lakini leo tunakaa mezani tu tunasema jambo hili ni haramu na wala kumbe hatujalifanyia utafiti, na tukifanyiwa utafiti kila mmoja atapata haki yake.

Mhe. Naibu Spika, sheria hii mimi naiombea Mungu ipite na ikishapita sheria hii wananchi wetu watakuwa na faraja sana. Mhe. Naibu Spika, kama nilivyoeleza mwanzo kama kitu chochote

unataka kukifanyia utafiti basi utakijua na ukishakijua utakifanyia kazi iliyo makini na ya kupata tija kabisa.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba kueleza kwa sababu hapa wavuvi hawawajui wavuvi ni nani, lakini unapoujua uvuvi wenzangu wengi katika Baraza hili hawajui mvuvi ni nani? Lakini mimi najua kwa sababu kazi hiyo nimeshaifanya Mhe. Naibu Spika, leo unamzuia mtu kuvua dema. Mhe. Naibu Spika, uvuvi wa dema ni uvuvi wa asili utakuja kutuonesha dema ya macho madogo, lakini hutooneshi dema ambayo inatakiwa ivuliwe zipo na zinavua samaki ambao wanatakiwa, lakini ni kwamba hatuelekezwi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nasema bado elimu ya kutosha haijatolewa kwa wavuvi isipokuwa sheria hizi zinakandamiza sana wavuvi. Mhe. Naibu Spika, nchi yetu hii ya Zanzibar ni visiwa vyenye wavuvi wengi sana basi mambo haya ya kivuvi yatakuwepo mpaka dunia itaondoka, isipokuwa tupange sheria nzuri zenye kuwapa uhuru wavuvi na kuhifadhi mazingira yetu yasichafuke. Lakini leo tunakaa tu tnasema kitu hiki hakifai wala hatuleti.

Mhe. Naibu Spika, kama tutafanya hivyo basi tutafikia katika shughuli za maendeleo na Zanzibar itapiga hatua nzuri sana kwa sababu tunao wavuvi wazuri. Mhe. Naibu Spika, pia tujue kuanzia leo kama wavuvi wetu ni wadogo wadogo, sio wavuvi wa bahari kuu. Leo mtu anakwenda kumvua pweza unasema hebu tuelezeni huyu pweza anaanza vipi na anakuwa vipi mpaka kufikia kuvuliwa.

Mhe. Naibu Spika, leo unazikuta nyavu za macho makubwa zimetiwa jiwe mimi najua kwamba nyavu kwa kuitia maboya matupu haivuwi, lazima nyavu itiwe na mawe japo moja moja ili iweze kugawa maji kwani haifiki chini. Ndio maana wenzetu wale wanatia maboya kama vile kisima cha roda nilivyokiona kama anaangalia chini kwa kile kioo na nyavu kama inakwenda katika matumbawe anavuta anapandisha nyavu yake haifiki chini. Kwa hivyo, naomba utafiti ufanywe na kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu basi Jumuiya ya Maendeleo ya watu wa Kojani aingizwe ili watu wakenda kwenye *field* waone jinsi wavuvi wanavyokuwa na hatima yake tutapata wavuvi waliokuwa wazuri kabisa.

Mhe. Naibu Spika, mimi sitaki nizungumze mengi lakini nasema hayo ili yafuatiliwe na nashauri tena kwa mara nyengine kila penye neno kilimo basi na uvuvi uwepo, kwa sababu haya mambo yanategemeana. Mhe. Naibu Spika, baada ya kuzungumza haya nasema nikipata changamoto nzuri basi nitaunga hoja mia juu ya mia, ahsante sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kuweza kunipa nafasi asubuhi ya leo kuweza kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Utafiti wa Kilimo. Kwanza niipongeze sana kamati kwa maelezo yake mazuri na kuelekeza yale ambayo waliyoyaona yaweza kufanyiwa na wizara husika. Pili, nimekaa hapo kwa muda mdogo nilikuwa najiuliza

Mhe. Naibu Spika, nini maana ya utafiti, halafu nikajiuliza je tuko makini au basi tu ionekane kama mswada huu umeletwa hapa tuupigie kofi halafu tuondoke. Mhe. Naibu Spika, hapa nikawa najiuliza kama tuko makini na jambo hili kwa sababu kwa hiyo dhana ambayo naijua mimi maana ya utafiti huu ni moja katika kuikomboa Zanzibar kuondokana na umasikini. Hilo mimi sina tatizo nalo nimekubaliana mia kwa mia.

Mhe. Naibu Spika, upande mwengine huwa nina wasi wasi sana kwa sheria zetu hatuzilindi, sisi tunakuwa tunazileta hapa tunaziunga mkono asilimia kwa asilimia, lakini baadae hatuzilindi. Hii mimi nitasema na nitaendelea kusema mpaka nitaondoka kwenye Baraza sitorudi nyuma nitalisema ukweli, kwa sababu ukweli mara nyingi sana ndio unaouma kuliko vitendo.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar tunaelewa kwamba ina rasilimali nyingi sana za kuwatajirisha wananchi wetu, hivyo tumeamua leo kuleta sheria hii ya utafiti lakini kwanza tujiulize wataalamu tunao? Mhe. Naibu Spika, wataalamu wako wapi na wameshakimbia, mtaalamu leo unakwenda kumpa shilingi 200,000 mshahara hivyo kweli atakaa kweli hapa.

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba serikali inamsomesha kwa jitihada zake zote hatimae leo anakuja hapa tunamdharau, pengine tunakwenda kumsomesha awe mtafiti wa mihogo tunamuondoa kule tunakwenda kumuweka katika kituo cha matrekta, hivyo tunafanya nini Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, kama tuko makini mimi nitaunga mkono la kama tumeuleta tu hapa masihara yamalize sawa, lakini sitounga mkono nikapata dhambi mimi hata siku moja.

Mhe. Naibu Spika watu wetu sasa hivi wamekubali kabisa katika masuala ya kilimo kwani sio kitu cha mchezo nina ujuzi nalo suala hilo, na laiti ingekuwa huko nyuma huu utafiti wetu tunaupa nguvu kwa sababu utafiti nina hakika upo, hapa tumekuja kutunga sheria tu baadhi ya mambo ili tuweze kuwapa nguvu. Lakini huko nyuma utafiti upo lakini haukuendelezwa Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, kwa wakulima wetu sasa hivi kuna sehemu nyingi wamekosa kulima na kama juzi tu wananchi wangu wa Jimbo la Kitope wamekosa mabonde ya kulima kwenye miwa kule wamenyanganywa hawakupewa, ndio mambo. Lakini ingelikuwa utafiti upo wale wakulima waliokosa mabonde yale ya Kitope na Mahonda basi mimi ningeamini kama utafiti ungefanya kazi sasa hivi wale wasingesikitika kwa sababu wamekwenda kulima chini ya minazi na maeneo tunayo. Lakini ni kwamba chombo hiki hakikukua ndio kwanza tunataka kukiimarisha basi hatukuchelewa, tumeambiwa kuna mbegu ya nerika.

Mhe. Naibu Spika, imezungumzwa tu mbegu hiyo lakini sehemu nyengine bado haijafika, na tumeambiwa kwa utafiti wa hapa na pale nerika wamefanya kazi kwa dakika tu, unaweza kuipanda pahali popote hata chini ya upenu wa nyumba yako inaweza ikafanya kazi. Lakini yale niliyokwambieni kuwa hatuko makini na mambo kama haya bado matatizo haya yapo. Mhe. Naibu Spika, mimi ndio nikawa na wasi wasi huo kama kweli tunakusudia kufanya kitengo hiki basi tuwe makini kabisa ili tuweze kuwagomboa wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, kwenye ukurasa huu wa 18 kwenye kifungu cha (d) kuingia katika mikataba ya shughuli yoyote nyengine na kufanya au kuagiza kufanywa mambo au jambo ambalo chombo kinachojitegemea kisheria kinaweza kufanya au kuagiza kufanywa. Mhe. Naibu Spika, mimi hapa nakubaliana nacho kifungu hiki sina tatizo nalo hivyo tuwape mamlaka hayo.

Mhe. Naibu Spika, kuna mambo mengi wanakuwa wanayaona lakini sheria inakuwa inawakwaza wanashindwa kuelewa, lakini tuikubali na tuwape kweli tusifanye mchezo tuwaruhusu waendelee kufanya shughuli zao, isiwe tena waziri au katibu hilo hakuna. Mhe.

Naibu Spika, mimi naamini kuna sheria ambazo zimewapa mamlaka watu kama hawa, haya naona kama marejeo yale kwa yale lakini kidogo kijifungu kile nimekisahau lakini sheria hii ipo ya kuweza kuingia mikataba na sekta nyengine kwa kuweza kufanya suala ambalo wao wameliona litawatilia tija au kufanya mambo mengine zaidi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nasema tuwe makini na kifungu hiki mimi nakubaliana nacho lakini kisiwe na vikwazo hadi vikwazo tuwape moja kwa moja kwa mujibu ambavyo tunachokipitisha hapa ili wakubalike moja kwa moja.

Mhe. Naibu Spika, mimi nakubaliana nazo kazi na uwezo wa taasisi na hasa hapa kifungu cha (b) kufanya utafiti na kutumia utafiti wa kilimo kwenye mazao, mazingira, mifugo, misitu, uvuvi, ardhi, maji, wadudu, maradhi na aina zote zinazohusiana na mambo hayo na mfumo wa viumbe na mazingira.

Mhe. Naibu Spika, ni kwamba sheria tumeitunga sisi na baadhi ya wanasheria wengine wanasema tafsiri ya sheria inakuwa na upana mrefu, unaweza ukaitamka lugha wewe ukasema ni sawa kumbe mwenzako akaja akasema sio sawa kabisa, umekosea kitu. Lakini Mhe. Naibu Spika, mwenzangu alisema suala la uvuvi hapa kuhusu wazamiaji wa chupa, hebu mimi naomba nisaidiwe kuna wazamiaji hawa ambao wazungu wanaokwenda kuzamia chini kwenda kuangalia mazingira na mambo mengine.

Je, hawa sheria hii inawagusa na kuna hawa ambao tunaambiwa wanakwenda kuvua kwa kuzamia na wao sheria inawagusa sasa hapa inakuwa akili yangu inanichanganya kuwa yule anavaa chupa na viatu na huyu naye anavaa chupa na viatu, hebu tuangalie hii mipaka ili katika utafitu wetu kama laiti ingelikuwa huko nyuma utafiti umefanyika lakini haukuwa na hadithi wala haukuwa na maelezo wa kuwaelezea hawa wavuvi wetu. Kwa mfano, watafiti kama wangekuwa wamefanya utafiti mzuri wa kisayansi hasa juu ya mambo ya bahari basi wangeelewa kuwa maeneo fulani kuna samaki wengi, lakini hicho kitu hakuna. Mhe. Naibu Spika, hebu tuamke katika utafiti wetu tuende kwenye mipaka ya bahari yetu tujue kwamba Wazanzibari tunadai mipaka yetu ya bahari.

Mhe. Naibu Spika, kuna mambo ni muhimu sana Wazanzibari kupata kujua. Mhe. Naibu Spika, mimi nimeshapitwa na wakati lakini tuna hawa tunaowazaa sasa hivi watataka kujua hatma yao ikoje, leo hatujui mipaka yetu ya bahari. Kwa hivyo, mimi ningeomba tuelezwe mipaka yetu ili kuweka sehemu zile ambazo wapi samaki wapo. Mhe. Naibu Spika, rasilimali hii ya samaki wapo wengi baharini lakini wananchi wetu wanapata tabu sana baharini.
Mhe. Naibu Spika, ni kwamba utafiti huu mimi naungana nao mkono, lakini tuwe wa kweli. Mhe. Naibu Spika, twende kwenye misitu, misitu yetu sasa hivi Zanzibar inateketea kwa makusudi kwa utafiti wangu msitu uliobakia sasa hivi ni Pongwe Kiwengwa na kule Pemba ni Ngezi tumemaliza kazi. Na hii inakuja kwa sababu kutokana na kutokuelimisha watu utafiti wetu haukuwa endelevu kwa sababu ingekuwa endelevu na sheria ipo kali sana na sisi viongozi tusiingie katika sheria basi tungefika pahali.

Lakini na sisi tujiseme maana yake mimi husema ukweli huku na huku nipo, leo ukikamata gari ya kuni mbichi za msitu wa Kiwengwa unapigiwa simu ya waziri iwache hiyo gari yangu. He!

Sasa wewe si ndiye unayetunga sheria hapa, nimenuniwa mimi humu sisemi uongo kwa sababu watu wengi nimewazuia gari zao za kukata misitu basi wamenuna, lakini ndio mambo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nawaambia humu tusinuniane tukimalize nje tuulizane hali vizuri kwa sababu mimi huko ndio kwenye kazi yangu hii sina kazi nyengine kama sio hapa na niwasemee hapa wananchi, niwalinde hapa. Kwa hivyo, tukifika pahala sheria hizi tunazitunga wenyewe halafu sisi wenyewe tunanuniana itakuwa hatufiki pahala na wala hatutotenda haki au msituletee miswada saa.

Mhe. Naibu Spika, misitu inateketea jamani hii ni hatari viongozi tuondokane na kazi hizi za hatari za kupeleka magari yetu kwenye mwitu. Mimi ningeomba hapa tufanye utafiti wa kina kabisa hali halisi ilivyo, mimi nakubaliana nayo sheria ya msitu bado ni nyepesi, na wataalamu wangu bado kidogo hivyo tuwaengeze wataalamu, tuwaelimishe wananchi mfuko wa fedha ziongezwe zaidi, Idara husika tuipe mamlaka ya kutafuta fedha kwa kuendesha masuala haya tusiwaingilie, tuwape uhuru kabisa ili waweze kufanya kazi zao kwa uaminifu kabisa ndipo kazi itakwenda. Lakini pakiwa na vikwazo, saini hii haipatikani mpaka uende kwa katibu au ipite kwa waziri, ipite kwa naibu katibu hatufiki pahali.Hilo Mhe. Naibu Spika, tukikubaliana hapa basi tuachie moja kwa moja ili waendelee na shughuli zao.

Mhe. Naibu Spika, kufanya majaribio kifungu cha (c) hiki mimi nakubaliana nacho. Lakini hivi karibuni kulikuwa na maradhi mengi ya mihogo lakini sijasikia serikali ikatoa kauli yake kuhusiana na hawa wadudu. Kwa sababu angalau ingekuwa wanaelimisha kuwa wadudu hawa wanasababishwa na jambo fulani, wananchi tahadharini sana na tatizo hili, basi mimi naamini Mheshimiwa ingekuwa mambo mazuri, lakini mpaka leo bado maharibiko ya mihogo yapo, nendeni kwenye mabonde tunamlaza na njaa mkulima masikini, tunachelewa Mhe.Naibu Spika kutoa tamko, serikali nalo hili tulione.

Mhe. Waziri hili tulione tuwe safi sana katika kuwatangazia wakulima wetu lazima tutoe taarifa ya haraka haraka kuwa tumeingiliwa na maradhi ya aina Fulani, na yanasabishwa na msitu, mti fulani au nyakati fulani. Basi mimi naamini tutakuwa sahihi na utafiti wetu utakuwa sawa kabisa.

Nikiendelea hapa hapa Mhe. Naibu Spika, zamani tulikuwa na vikundi kule mashamba sijui walikuwa wanaita *DABEC* wale, Mhe. Waziri utanisaidia hilo utapokuja kunijibu, hawa walikuwa wana-*deal* na utibabu wa mikarafuu na walikuwa ni watafiti wa mikarafuu. Sasa ndio maana wakati wa kipindi kile utakuta mikarafuu mingi, mihiliki mingi, lakini serikali imejikunuta imewaondoa wale ata sijui wameishia wapi, tusiwe wabakhili jamani tutumie hizi fedha za wavuja jasho kwa kuwasaidia katika vitu kama hivi kuwaondolea umasikini, tunakuwa tunaona tabu sijui kwa nini.

Mhe. Naibu Spika, mwenye fedha leo hayupo lakini atapata salamu zangu, nasema kuwa zile fedha zinazokusanywa za kodi wawape hao mawaziri watimize zile ahadi zao kwenye bajeti zao, ndio hatari yake sasa inakuwa kama hivi sasa, wanakuwa wanashindwa kufikisha yale malengo kwa sababu fedha hamna tunasema kila siku uchumi uko nyuma, sasa leo tunaongeza misaada ya utafiti, tunaongeza na mambo mengine sijui uchumi huo tutaukuta wapi sisi.Kwa sababu kitengo hiki itabidi wataalamu walipwe, wawe kila baada ya muda fulani wanabadilika wanakwenda nje kuangalia mazingira ya wenzetu kutuletea huku.

Mheshimiwa nilikwenda China. China angalia wenzetu utafiti wao, kuna sehemu nyengine ambazo hazistahiki kupandwa tungule, lakini wanapanda tungule kwenye nyumba, kwenye mabweni, au kwenye mahanga.Utakuta sehemu nyengine watu wanapanda tungule, viazi, na mambo mengi sana, sasa hili nalo tuliangalie vizuri sana utafiti ni kitu muhimu sana, utafiti ni mkombozi wa umasikini katika kisiwa cha Zanzibar ni lazima tuheshimu sana.

Mhe. Naibu Spika, tunasema kuna kitu ardhi, ardhi tuseme hamna tena sasa hivi tumeikosea *is too late*. Ardhi tumeikosea mimi sijui niseme ardhi ya kulima iko wapi sasa hivi, niseme ardhi ya utafiti iko wapi, tumekosea.Kwa upole zaidi nazungumza, kwa sababu suala hili limeniuma sana kuwa ardhi hatuna ya kulima na leo tunaunda chombo hiki kikubwa sana kwenye Baraza hili tukufu kabisa chini ya dhamana yako Mhe. Naibu Spika, na mswada huu pengine utapitishwa kwenye dhamana yako ni kitu ambacho kinatia huzuni sana. Watu wamevamia sana, leo raha kama hiyo inaletwa ya kuletwa wataalamu waje kutufanyia utafiti wa kila leo kuondoa umasikini kwa njia ya kilimo, lakini tumechelewa hatuna ardhi.

Lakini nasema bado hatujawa na masikitiko makubwa. Nilikwenda nchi moja sehemu fulani hivi nimeisahau, nchi hiyo ina majabali ni China lakini kidogo sehemu imenitoka. Mhe.Naibu Spika, wanachukua udongo wanakwenda kusambaza, kwa mfano nichukulie eneo la Matemwe kule ni jiwe tupu tu, basi unachukua dongo unajaza mle watu wanaendelea kupanda.Sasa tutumie utafiti wetu, watafiti hawa hii sheria ikipita nalo hilo moja waliangalie ndio ardhi zilizobakia kwenye mawe mawe tu, ukija ukanda ule wa Makunduchi kule ndio mama! Ni ukanda mkubwa sana wa jiwe tupu. Binadamu kapewa akili na maarifa kuliko mnyama, naamini watafiti hawa watapoletwa pale, moja katika *study* yao waangalie hiyo ili kuweza kutafuta kifusi, udongo ili ile ardhi iliyobakia tena tuiokoe tulime.

Mhe. Naibu Spika, mimi nakubaliana na mswada huu sina tatizo nao, lakini kukubaliana kwangu mimi aje kuniambia Mhe.Waziri Mheshimiwa ulipokuwa ukichangia kuna maeneo ambayo uliyaeleza wewe haya kwa hivyo, mimi nakuunga mkono kwa asilimia mia moja, atanambia yeye Mhe.Waziri halafu ndio mimi nikubaliane nao.

Mhe.Naibu Spika, mimi nakuwa na tahadhari sana sasa hivi katika miswada hii, nina imani kubwa sana kuwa tutunge sheria twende tukaifanyie kazi, tunatunga sheria Mheshimiwa hatwendi kufanya kazi, hili linaniuma sana tena linaniuma kweli.

Juzi hapa tulizungumza samahani Mhe Naibu Spika, tulipiga kelele suala la Mswada wa Sheria ya Utalii leo wako kibao bado huko, ndio maana Kenya wanasema Serikali ya Zanzibar tumeitia kwenye kiganja hapa, au tumesema nini hapa? Sio lengo Mhe.Naibu Spika, samahani unajua jazba inakuja saa nyengine ule uchungu wa roho.Sasa hili ndio wasiwasi wangu mimi nikawa nasema kitu kinachoniuma kuwa tunatunga sheria lakini hatuzitekelezi.

Mimi nilifikiri wizara zinazohusika zitafanya kazi lakini hazikwenda huko kunakohusika, wanatuacha tunapiga debe tu wanatuona wenda wazimu tukizungumza hapa hapana, tunataka sheria inayotungwa hapa jamani mawaziri shukeni chini mwende kule mkaone, lakini hawashuki wanangojea mpaka waitwe na Rais wende kule na *document* zao wanakwenda kumdanganya, aaa hapo nimeuliwa sana bango kitita.

Mimi hapa nalia sana, Wallah ingekuwa laiti Mhe.Naibu Spika, nilisema siku moja kuwa Mhe.Rais anionjeshe uwaziri sasa siutaki tena, wala sisemi tena lugha hiyo.Siutaki tena Mhe. Naibu Spika, hata kidogo roho yangu safi kabisa bora niweko huku huku juu. Jukumu kubwa nimeligundua, na swahiba wangu mmoja kanambia jukumu kubwa sasa sitaki.

Kwa hivyo, jamani ninachoombea kuwa mawaziri tukizungumza hapa twendeni huko chini tukaangalie hali ngumu.Mkenya anasema hivi hivi Serikali ya Zanzibar nimeiweka kwenye kiganja hapa, kwenye hoteli huko *Blue Bay* huko yanazungumzwa wanatamba kabisa. Sasa hili ndio tatizo lake, *message* imefika.

Mhe.Naibu Spika, ahsante sana nitaunga mkono baada ya kumuona Mhe. Waziri ataponijibu maswali yangu mazuri nitampa kwa asilimia mia moja, lakini wananchi wa Jimbo la Kitope sasa hivi wakali sana, neno si neno wananiletea ujumbe kunambia Mheshimiwa usingempa yule hatutaki hilo, na mimi nawasikiliza na wao ndio kibarua hiki wamenileta hapa siwezi kuwakatalia. Ahsante sana.

Mhe. Shawana Bukheti Hassan: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii ya leo na mimi niweze kutoa mchango wangu katika mswada huu ulioko mbele yetu. Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniamsha salama na kuweza kusimama kwenye Baraza lako hili tukufu.

Lakini hapo hapo Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza waziri mpya wa Wizara hii ya Kilimo na Maliasili kwa uteuzi alioupata hivi karibuni, na Mwenyezi Mungu amjaalie, amuwezeshe kushika nafasi hii na aweze kukidhi haja za Wazanzibari kama tunavyotegemea.

Mhe.Naibu Spika, niungane na wenzangu kusema kuwa mswada huu ulioletwa kwetu ni mzuri, kwa sababu suala la utafiti ni suala zuri na ndilo suala linalotoa utatuzi wa masuala mbali mbali. Suala la utafiti katika nchi yetu kwa yale yaliyoorodheshwa katika mswada huu ni sawa sawa na mgonjwa ambaye kenda hospitali unamtafutia vipimo halafu ujue tiba yake ni nini. Kwa hivyo, mimi napongeza sana mswada huu umeletwa kwetu na nadhani sote tutaupitisha ili hii azma iliyokusudiwa humu kwa mustakabali wa wakulima na nchi yetu uweze kufikiwa.

Mhe.Naibu Spika, mimi kidogo niseme kwamba, kama kulikuweko na chombo hiki, sasa hivi ndio tunakihalalisha basi ni sawa, lakini kama kilikuwa hakipo chombo hiki kwa kweli tumechelewa. Kwa sababu wananchi wetu, wakulima wetu, walikuwa wanatarajia jambo hili la utafiti katika masuala yote yaliyoelezwa humu yawe yameandaliwa mapema, na kila wanalolifanya liwe linafanyika kwa uhakika na ile azma ya kuweza kumuokoa mkulima na kusema kilimo ni uti wa mgongo ilikuwa iweze kufikiwa. Lakini kama ni bahati mbaya kilikuwa hakiko chombo hiki kabisa hapo niseme kuwa tumechelewa, lakini kama kilikuwepo leo tunakipitisha kisheria basi nadhani tuendelee nacho vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli nataka kusema kwamba chombo hiki kitapopitishwa na kikaweza kufanya kazi zake, tutawasaidia sana wananchi wetu katika masuala mengi yanayowakwaza katika kujipatia mapato. Ijapokuwa wataalamu hasa wanasema kuwa kilimo hasa hakiko katika

kupunguza au kuweza kuongeza mapato ya nchi, lakini yanasaidia sana kuwapunguzia masikini katika kujikwamua kwenye masuala mbali mbali ambayo yanawakwaza.

Sasa hivi tuna mambo mengi hapa kwetu Zanzibar ambapo wananchi wetu, vijana wetu, ingekuwa masuala hayo yamefanyiwa utafiti mapema, sasa hivi nadhani tungekuwa mbali. Mpaka hivi sasa Mhe.Naibu Spika, utakuta vijana wetu wanakaa vijiweni hawana shughuli hasa za kufanya, na wengine si kwa kuwa wanataka na wengine tunajitahidi kuwawezesha vijana hao hasa wa vijijini ambao elimu yao pengine hailingani na kuweza kupata ajira, lakini wanaweza kujiajiri wenyewe katika masuala mazima haya ya kilimo. Mhe. Naibu Spika, utakuta vijana hao hata uwape mtaji wa kwenda kufanya shughuli za kilimo hasa mambo ya mbogamboga ni wachache sana wanaofanikiwa, wengi hawafanikiwi na mpaka hivi sasa tuna hoteli nyingi hapa, tuna watalii wengi wanakuja, lakini bado vijana wetu hawawezi kufaidika katika suala hili kutokana na kuwa hawana uwezo wa kuweza kujua kitu gani wakifanye vipi au wapange na washughulikie vipi waweze kufaidika.

Kwa mfano Mhe. Naibu Spika, sasa hivi kunaletwa mbogamboga nyingi kutoka Tanzania Bara, kunaletwa kabichi, karoti, pilipili mboga na mengineyo ambayo mimi hapa sikuweza kuyakumbuka, hata matikiti pia yanaletwa tena gari kwa gari. Sasa nikawa nakaa najiuliza kwani hivi vitu hapa sisi hatuwezi, vijana wetu wakaweza kupanda tukawahamasisha wakaweza kuimarisha mazao haya na kuweza kuuza kwenye hoteli yetu na tukajipatia faida na vijana kujikomboa na umasikini?

Lakini utakuta jibu hakuna, wanaofaidika ni wachache, wataopanda tikiti maji anakaa siku mbili tatu limeshatumbuliwa na wadudu, basi mara ya pili haliwi tena keshavunjika moyo. Anayelima pilipili mboga utakuta majani yashanyauka basi pilipili mboga pale haziji tena haendelei, anayelima tungule na mambo mengine halikadhalika hali ndio hiyo hiyo. Sababu ni nini? Hakuna utafiti.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, tunaomba sana hayo waliyoeleza wenzetu katika mswada huu basi yafanyiwe kazi kama walivyotangulia wenzetu, kupitisha mswada kwenye Baraza letu ni sehemu moja lakini kutekeleza ni sehemu ya pili. Kwa hivyo, sheria hizi tunazozipitisha hapa zifanyiwe kazi, na humu katika mswada mmeelezwa katika suala zima la kusema kuwa tafiti zitazofanywa baadae zitakuja kuwasilishwa kwa wananchi wenyewe wale wanaohusika na utafiti ule waliofanyiwa katika eneo lao. Kwa hivyo hili tunaliomba lifanyike.

Kuna mjumbe mmoja hapa kazungumzia kuhusu suala la wataalamu. Mimi kwa mtazamo wangu Wizara ya Kilimo ina wataalamu wengi sana na tulifikia mahali tukaona kuwa Wizara ya Kilimo ina wataalamu wengi kuliko hata wizara nyengine, lakini wataalamu wao hawaonekani nini wanachokifanya ndicho wanacholalamikia wananchi na watu wetu kwa jumla na wakulima wetu. Wataalamu hao, wanalima wananchi wetu utasikia kuna mabwana shamba, mabibi shamba lakini mimi sijawaona wanapangiwa wapi, sijui wanapangiwa huku mjini Kikwajuni huko kuimarisha asumini na mawardi, lakini kule vijijini hatuwaoni, watu wanalima vilimo tofauti vya kujikwamua kimaisha lakini hali halisi inavyoonekana watu hawafaidiki.

Watu walijaribu kulima kilimo cha uyoga, lakini utakuta ni wachache waliofaidika na wengine wamevunjika moyo na pesa zimetumika nyingi mno.Hapa Unguja watu wamelima eneo la

Kinduni, kule Pemba sehemu za Wete, lakini sasa hivi utawakuta hawauendelezi mradi ule lakini maeneo ya kuuza yapo, hoteli tunazo. Kwa hivyo, mimi ningeliomba sana kwa upande wa kilimo wenzetu mjitahidi sana, kwa hayo mliyoyaeleza humu basi myafanyie kazi, lakini matokeo ya haya basi yawafikie wahusika yasiishie tu kukaa humo mnamokaa utafiti umefanyika unaishia mezani, kwenye makabrasha makubwa makubwa utafiti uko hivi basi mnaishia wenyewe kwa wenyewe huko kwa huko, uwafikie wahusika.

Mhe.Naibu Spika, wale wanaoitwa mabibi shamba na mabwana shamba na wengine wote basi wateremshiwe ili wawafikishie wananchi na kuwaambia jamani utafiti uliofanywa katika eneo lenu mpaka sasa hivi zao hili na hili hapa haliwezi kuja, lakini kama kuja tumieni hiki na hiki mtafaidika.Hilo lilikuwa la kwanza Mhe. Naibu Spika.

Lakini la pili, mimi bado nina wasi wasi katika kutekeleza hasa huu mswada wenyewe, kwa sababu naona umejifunga funga katika maeneo mengi, wizara nyingi pamoja na Wizara ya Fedha ipo, Tawala za Mikoa.Lakini wasiwasi wangu kuwa sasa hivi huu mswada unawasilishwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili, lakini wamejumuisha na mambo ya uvuvi, mifugo na maeneo mengine. Kwa zamani ni sahihi kwa kuwa kilimo, mifugo, mazingira, uvuvi yote ilikuwa ni wizara moja, kwa utekelezaji wake kimtazamo wangu mimi ilikuwa ni rahisi, sasa hivi itakuwa wizara zimo nyingi. Mimi wasiwasi wangu hakutotokea migongano katika utekelezaji wa jambo hili? Sasa labda Mhe.Waziri aje atusaidie kututoa wasiwasi katika suala zima la utekelezaji wa jambo hili.

Jengine niseme tu kuwa humu kuna Wizara ya Fedha katika jadweli imesema nao watakuwa wahusika katika suala hili.Ni sawa lakini kwa kweli mambo yetu mengi yanakwama kutokana na fedha ambazo huwa zinahitajika.

Mhe.Naibu Spika, suala la utafiti kama tunavyosema ni zuri na litatusaidia, lakini lazima tujue utafiti una gharama zake na wengi wanasema kuwa kila jambo zuri lina gharama na utafiti una gharama, basi kama Wizara ya Fedha ndio wamo humu na wao katika kulisimamia hili jambo, basi wajitahidi kadiri ya uwezo wao kuhakikisha kuwa hizi pesa zinapatikana ili haya malengo yaliyokusudiwa yaweze kukamilika na kutekelezeka, vyenginevyo yatakuwa ndio yale wanayosema wenzangu tunakuja hapa tunapitisha miswada, tunazungumza kwa nia moja lakini katika utekelezaji hamna kitu.

Sasa vitu kama hivi itakuwa vinavunja moyo Mhe. Naibu Spika, matokeo yake inakuwa kazi kumbana waziri masuala mbali mbali, kwa nini utafiti mpaka leo hili halijafanyika.Lakini kutokana na yale ambayo tunayapanga matokeo yake hayakamiliki kama vile mategemeo ya wananchi na wakulima kwa ujumla wanavyotegemea. Kwa hivyo, tunawaomba sana wahusika wote, hasa Waziri wa Fedha basi wajikite vizuri katika kutenga hizo fedha kuona hili jambo linafanywa kama lilivyokusudiwa.

Mhe.Naibu Spika, kama nilivyosema kuwa utafiti ni mzuri kwa sababu hata usafi wa mji, wafugaji wetu nao wanajitahidi katika masuala ya kufuga ng'ombe wa kisasa, mbuzi wa kisasa, kuku, lakini matokeo yake utakuta tunakwama au wafugaji wetu wanakwama. Utakuta wafugaji wa ng'ombe wa maziwa asilimia kubwa Mhe. Naibu Spika, wanajitahidi watu kuchukua ng'ombe lakini ng'ombe hao wengi wanaopata hasara kuliko wale wanaopata faida, ng'ombe

wanakufa. Sasa na hili nalo liangaliwe, katika utafiti huu kuona hali halisi tunaiwekaje, mazingira gani tuwasaidie wenzetu kuona katika hali hii ya hili tulilokusudia kujikwamua katika mazingira ya umasikini basi wanajikwamua kweli. Watu wengi wanapewa ng'ombe, hawa wenzetu wa *TASAF* mashirika mengi wanasaidia lakini hali ndio hiyo.

Jengine Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani kama nilivyosema kuhusu masuala haya ya utafiti hasa huu wa ng'ombe ukifanywa vizuri, nadhani tunaweza kurudia kule tulikotokea. Hapa nakumbuka tulifikia mahali sisi hapa Zanzibar tukawa tunatoa siagi zetu, maziwa tunakunywa, hata lile swali lililoulizwa asubuhi la maziwa nadhani pia lisingekuwa kikwazo kikubwa, watu wangeweza kununua maziwa tena yalikuwa bei nafuu tu, yanauzwa mle kwenye vibanda vya maziwa, raha mustarehe kila mtu anakunywa maziwa watu wote wanafaidika.

Siagi zile *blue band* zinazokuja kutoka nje tulikuwa tunatengeneza hapa hapa kwetu. Sasa imekuwa sisi ni soko tu la watu, tununue tuje hapa basi watu waje kwenye soko wauze vitu vyao sisi hatuna hata kimoja ambacho kinatusaidia hapa kwetu.Na kwa mtoto kuila siagi nyumbani mashaka kweli kweli na siku zile ilikuwa nafuu, nyumbani ukitaka hata kipaketi kidogo tu cha siagi unapata mtoto anaweza kujisaidia, lakini sasa hivi umekuwa mtihani.

Kwa hivyo, mimi ningeliomba jamani huu utafiti uende vizuri na baada ya kutiwa saini kama tutangojea bajeti au vipi, lakini kama hizo fedha zitatiwa baada ya bajeti zitatengwa, basi hapa tukijaaliwa muda si mrefu, ikiwa si robo mwaka basi nusu mwaka tuwe tunaletewa hizo tafiti zilizofanywa zimefanywaje, zimefikia vipi, na zinaendeleaje na zimetusaidia vipi sisi wananchi wa hapa Zanzibar.

Mhe.Naibu Spika, nije kidogo tu kwenye mswada huu ukurasa nambari 17 sehemu ya ufafanuzi kuna neno ''Afisa Utafiti na Mkuu wa Kilimo''. Mhe.Naibu Spika, mimi ningeomba atusaidie aliyewasilisha mswada huu afisa huyu hakutajwa kiwango chake cha elimu wakati Mkurugenzi ametajwa kiwango chake cha elimu. Sasa hapa mimi ningeomba tusaidiwe kuweza kujua na yeye atakuwa na sifa gani katika hili? Hilo la kwanza.

La pili, Mhe.Naibu Spika, ukurasa huo huo na kama sio Mhe.Waziri ataangalia vizuri ataweza kunipatia ufafanuzi. Kuna neno "Zao la Kilimo lililopandishwa au Zao la Mwitu".Mimi hapa sijafahamu, Kiswahili fasihi ni nini? Kupandishwa, kupanda au kupandikiza mimi ndio najua, sasa hiyo kupandishwa mimi najua mara nyingi kupandishwa huwa ni wanyama, sasa hili zao inakuwaje na tafsiri hii.

Mhe.Naibu Spika, jengine ni kusisitiza tu katika suala zima la kuweza kupata utafiti wakulima wetu kuweza kupatiwa taaluma kama nilivyokwishaeleza hapo mwanzo.

Mwisho kabisa Mhe.Naibu Spika, nimalizie tu kwa kuulizia kuhusu utafiti unaofanywa pale katika Chuo cha Kilimo cha Kizimbani. Je, utakuwa na uhusiano gani au kutakuwa na mashirikiano gani na utafiti huu wa kitengo hiki kinachotaka kuanzishwa. Naona ni hayo tu Mhe. Naibu Spika, mengine nadhani watachangia wenzangu lakini imani yangu kwa yale ambayo nimeyaeleza katika mswada huu, wenzetu wanaohusika kuanzia waziri na wataalamu wake na wote wanaohusika kwenye mswada huu basi tungeomba wayafanyie kazi kikamilifu ili yale malengo tuliyoyakusudia yaweze kufikiwa.

Baada ya hayo Mhe.Naibu Spika, nakushukuru tena kwa mara nyengine na naunga mkono hoja kwa sababu na mimi niko katika eneo kubwa la kilimo, ili wakulima wangu kule waweze kufaidika. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza nianz nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima na kuweza kufika kutekeleza shughuli zetu tulizojipangia kwa siku ya leo katika Baraza lako hili tukufu. Mhe. Naibu Spika, pili nikushukuru kwa kunipa nafasi ili kwa umuhimu wa mswada huu nami nizungumze machache.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwa kuwasilisha sheria hii ambayo ijapokuwa tunasema imechelewa, imechelewa sana naweza kuthubutu kusema kama mgonjwa ambaye maradhi yashamthakilisha na nyuma hakufanya *checking* ya mwili wake, lakini sasa hivi kishakuwa yuko taabani kwa maradhi anaanza kutibiwa hajui atibiwe wapi. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, haidhuru umechelewa huu mswada lakini ni mswada mzuri wa sheria nami nasema naunga mkono mswada huu kabla sijazungumza chochote. Kwa sababu ni mswada ambao utatusaidia sana katika shughuli zetu zote ambazo zimetajwa katika sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nianze kwa kusema kwamba tuliambiwa kwamba kuna mapinduzi ya kilimo, nimuunge mkono Mhe. Saleh Nassor Juma aliyesema kwamba mapinduzi ya kilimo kweli yamefeli tena yamefeli kweli kweli. Mhe. Naibu Spika, sasa hivi wakulima wa mpunga hawajui wafanye nini waliokuwepo Cheju na sehemu zote. Hivi sasa kuna wakulima wengi ambao hawana mbolea hawajui waipate wapi.

Mhe. Naibu Spika, nadhani katika bajeti iliyopita tuliifurahia sana na tukaipigia makofi vizuri jinsi ya punguzo kubwa lililokuwepo la dawa. Lakini hivi sasa dawa Cheju wanauziwa kuanzia shilingi 18,000/- mpaka 20,000/- na hawajui waipate wapi na wakati umefika huu wa kulima, wananchi wanalia hawajui wafanye nini.

Kwa hivyo, hii hali ionekane kwamba wakati ule tulipongeza sana tukampigia makofi Waziri sote tulifurahi kwa hali tuliyoiona na kweli wananchi walivuna sana mpunga kwa sababu hawa mabwana shamba walikuwa karibu na wakulima. Lakini inaonekana kipindi hichi wamewaacha mkono, mbali ya kuwa matrekta vile vile yalichelewa kusogea, pia na hawa wahusika wamewatupa mkono wakulima.

Kwa hivyo, ni lazima wakulima waonekane wasikilizwe kilio chao. Nina imani kwa haya yote kwa mswada huu tukiupitisha basi hali itakuwa nzuri ambayo itatuunganisha na wakulima wetu ili tuwaondoshee mzigo mkubwa walionao. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri akimaliza Baraza hili apite katika mashamba ya kilimo awaone wakulima hivi sasa wanavyochacharika.

Mhe. Naibu Spika, nadhani katika huu utafiti tulikuwa tukiuzungumzia sana katika vikao vingi vikija habari za kilimo basi inazungumzwa habari ya utafiti. Kwa hivyo, nakumbuka Baraza la Saba mimi nilizungumza juu ya watafiti jamani hawa wataalam washuke. Kuna suala zima lililoingia hivi sasa jinsi wakulima wanavyojishughulisha, mkulima yeyote anajua kwamba uajiri

wake ni kujishughulisha katika kilimo, anajiajiri na anatupa nguvu zake zote na kila mbinu anatafuta vipi atavuna vizuri na vipi atakuwa na mazao mazuri.

Mhe. Naibu Spika, nilisema katika Baraza la Saba lililopita kwamba wakulima wengi tumechukua mataka tunakwenda kumwaga katika mashamba yetu, lakini pia yale mataka tuliyokwenda kumwaga sisi tunamwaga tu katika mashamba hakuna utafiti wowote wala hakuna utaalam wowote, sisi tunamwaga tunalima tunangojea kuvuna. Sasa hapa palikuwa panataka patoke taaluma kwa wakulima je, mataka haya tunayomwaga tu baada ya kumwaga kweli kile tunachokipanda tutafanikisha na kile tunachokipanda je, hakina madhara kwetu.

Mhe. Naibu Spika, siku moja mimi niko Mjumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii tulikwenda Tanzania Bara nikamuuliza mtaalam mmoja ile wasi wasi wangu kwa sababu na mimi ni mmoja katika waliomwaga mataka. Sasa baada ya kumwaga mataka nimepanda, nini athari yake niliyoiona, migomba yote ile imekufa. Akanambia kwamba baada ya kumwaga mataka yale ukae muda wa mwaka mzima tena hapo ndio upande.

Sasa sisi hatuna utaalam ule baada ya kumwaga tumepanda na baada ya kupanda taathira tumeiona. Vitatoka vitu muhogo tuuchukue mimi na Mhe. Asha Bakari Makame hatuuwezi, hilo utasema ni fanikio moja kwa mkulima atasema muhogo umetoka mzuri lakini unalika, hauliki muhogo ule.

Ukilima kiazi kikuu mimi na Mhe. Asha kukichukua hatukiwezi kinalika, hakiliki. Kwa hivyo, sheria hii ikipitishwa itatusaidia na naomba hawa watafiti wasikae juu ya meza maofisini washuke kwa wakulima. Mhe. Naibu Spika, mimi nimefurahi sana kwa taasisi hii kuundwa ili ipate kutusaidia.

Mhe. Naibu Spika, tuje katika mifugo amezungumzia Mhe. Shawana Bukheti Hassan hapa juzi nimesikia katika mawio wanasema watu wa Wambaa wameletewa ng'ombe wa kufuga kutoka nje, ng'ombe wale baada ya kufika hapa tu wamefariki tatizo liko pale pale na wamesema kwamba kutokana na mazingira, hali ya hewa. Laitani kama pangelikuwa na utafiti wa kutosha basi ingelijulikana athari hii kabla. Kwa hivyo, pia naomba na hapa tuwe na utafiti wa kutosha katika hali kama hii. Watu wetu wanajitahidi sana kujikwamua katika hali ya umaskini kwa kila njia na kwa kila mbinu na wafadhili nao wanajitahidi lakini bila ya kujua kuna athari gani na matatizo gani kwa kweli hili ni tatizo. Kwa hivyo, mswada huu utatusaidia kufanyiwa utafiti katika hali zote hizi ili kupata tija ambayo itatusaidia kimaisha.

Mhe. Naibu Spika, jengine tuje katika utafiti sehemu ya uvuvi. Mhe. Naibu Spika, mtaalam hapa wa uvuvi ambae yeye ni fani yake amezungumza vizuri sana, nayo kuwe na utafiti wa kutosha. Leo mvuvi ajira yake iko katika uvuvi unapomwambia asiende pwani umeshamuua, asiende kuvua kwa nyavu ambazo haziruhusiwi umeshamuua.

Nadhani huu utafiti uwe wa makini, leo kuna ugomvi watu wa Marumbi na Chwaka, hapo nyuma waliwahi kuuana, hili ni tatizo. Pia naomba katika kila sehemu ambazo kunahitaji utafiti kuwe na utafiti wa kina na utafiti ambao utaondosha migogoro yote. Kwa sababu migogoro inachangiwa kwamba pia hapakuwa na utafiti wa kina.

Mhe. Naibu Spika, nadhani kama walivyosema wenzangu kwamba kutunga sheria ni jambo moja, utekelezaji wa sheria hiyo ni jambo jengine. Kwa hivyo, sheria tunazozitunga zisikae katika makabati tu lakini zifanyiwe kazi na zitumike.

Mhe. Naibu Spika, mimi nathubutu kusema kwamba ikiwa sheria hii tutaitumia ipasavyo basi utafiti utatusaidia mambo mengi. Kwa sababu hata hicho kilimo tulichokuwa tukilima mimi nakumbuka zamani mpunga wetu mbegu zetu hasa watu walikuwa wakiipa kipaumbele *super*, unaipakua hapa basi nyumba kumi zinapata habari leo Bi Mtumwa kapika *super* nini. Lakini hata mipunga yetu ya sasa tunayopika wala hujui kama mtu kapika mpunga mpya.

Mhe. Naibu Spika, mimi tangu mdogo nimelelewa na wazee wangu basi tuko kwenye kilimo tunahama Ndijani tunahamia Cheju mpaka tunamaliza kulima tunajua mpunga unanukia vipi. Kwa hivyo, tujue kitu gani kinachosababisha mipunga ya sasa kwamba unakula wali mpya haunukii hata kidogo.

Mhe. Naibu Spika, Mwenyezi Mungu amrehemu babu yangu siku moja nilimuuliza kwa nini huu mpunga wa sasa haunukii, akanambia babu mpunga wa sasa unatiwa madawa mengi, lakini mpunga wa zamani tulikuwa hatutii madawa mengi. Ikaniingia akilini mimi kwamba mpunga nimeuvuna leo naupika ndani hauna tofauti na mapembe haunukii hata kidogo.

Kwa hivyo, mimi nadhani pia tupite nyanja hizo za kufanya utafiti kitu gani kinachotufanya kwamba mpunga wetu mpya tunauvuna sasa hivi hauna harufu wala ladha hata kidogo. Mhe. Naibu Spika, hili ni jambo zuri sana na tusisitize tu kwamba sheria hii itumike ipasavyo na wataalam wetu wawe karibu na wakulima ili kuwapa nguvu.

Mhe. Naibu Spika, pia kufanya utafiti katika maji. Mhe. Naibu Spika, njoo Jumbi panapo jaa la taka, pale pametupwa taka kwa muda mrefu na jaa lile pale pana vianzio vya maji. Kwa hivyo, utafiti huu unataka uwe nao kwa hali ya nguvu ya kweli kwa sababu maji yale wanatumia binaadam, sijui maji yale kama yako salama kwa binaadam. Sasa pia itatusaidia kufanyiwa utafiti katika sehemu zote za maji ambazo maji yale yako katika sehemu hatarishi.

Kwa mfano, kama hapo Jumbi ambako pamemwaga taka kwa muda mrefu sana labda sasa hivi tena wananchi wamegoma pasimwage taka tu, lakini muda mwingi taka zipo pale inaonesha maji ya pale yanataka kuangaliwa kila wakati na kufanyiwa utafiti ili wananchi wasiathirike afya zao.

Mhe. Naibu Spika, nina imani sheria hii itatusaidia wakulima, itawasaidia sana wafugaji, wavuvi na kupata ardhi iliyo nzuri baada ya kufanyiwa utafiti ili tujikwamue wananchi wote katika sehemu hii ya kilimo ambayo ni uti wa mgongo. Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo, mimi naunga mkono mswada huu mia kwa mia.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii nimpongeze Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye ni miongoni mwa kutilia mkazo mambo ya kilimo na utafiti.

Mhe. Naibu Spika, ni hivi karibuni tu Rais wa Zanzibar alifanya utafiti wa kilimo cha mpunga na tukaona kwenye televisheni jinsi gani alivyokwenda kuzindua na mpunga *mashaallah*. Sasa

nimesema nianze kwa hili Mhe. Naibu Spika, niipongeze wizara na serikali kwa jumla kwa kuleta mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu ni muhimu kabisa katika nchi hii. Mimi naweza kusema kama tunavyosema kwamba kilimo ni uti wa mgongo, basi na huu mswada ni uti wa mgongo katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, niungane na baadhi ya wenzangu kwamba katika Wizara yenye wataalam wengi ni Wizara ya Kilimo na Maliasili, nathubutu kusema kwamba ina wataalam wengi na wenye ujuzi.

Sasa naiomba serikali kwamba mswada huu ni wa utafiti. Tatizo tulilonalo Mhe. Naibu Spika, ni kwamba tunatunga miswada tunaiweka ni sheria lakini baadae sasa kutunga na kupitisha ni kitu mbali na kutekelezwa ni kitu mbali. Niombe kwamba tusifanye mchezo kwa sababu ukiangalia fedha nyingi sana zinatakiwa katika mswada huu kwa utafiti na kutafuta wataalam wenye ujuzi.

Mhe. Naibu Spika, niombe sana wenzangu walijaribu kusema kwamba yanapokamilika mambo haya basi tuwaombe wataalam wetu wasikae maofisini, kwa kweli wahakikishe kwamba wanakwenda vijijini.

Mhe. Naibu Spika, jengine niseme kwamba katika utafiti huu tunapochangia baadhi ya wakati hapa katika michango yetu kwenye bajeti huwa tunazungumza mambo mengi sana ambayo tunaichangia Wizara hii ya Kilimo na Maliasili lakini hayachukuliwi hatua. Mimi nasema kwamba hebu watafiti wakae kitako mikoa yetu ni mitano tu na kesho kutwa tutakuwa na mikoa miwili mingine iwe wa sita. Ni sababu zipi ambazo zinatupa kwamba hatuwezi kufanya utafiti wa kila mkoa. Katika Mkoa wa Kaskazini Pemba tuseme mfano katika shehia zake na juzi nilizungumza suala hilo, ni kitu gani ambacho kama tutatupa nguvu zetu panapaswa kupandwa nini na nini.

Hebu tufanye utafiti huu tutenge maeneo ya kilimo mbali, tutenge maeneo ya ujenzi mbali, tutenge maeneo ya utalii mbali, tukifanya masihara kisiwa hichi basi wakulima wetu watakuwa hawana pahala pakulima. Maeneo mengi sana ya kilimo tumeyachukua tumeyafanya ni makaazi, maeneo mengi sana tumeyachukua tumeyafanya ya utalii. Haidhuru utalii unatuletea asilimia 80 ya pato la Zanzibar lakini je, tumejisahau kwamba na sisi wenyewe tunataka chakula.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia katika kisiwa cha Zanzibar maeneo yote takriban hata haya ya maweni tukiweza kuyatumia basi mpaka *in island*. Wewe chukua kijiti chako kizike ujue kitachipua. Sasa na mimi naomba huu utafiti uwe utafiti wa kweli, usiwe utafiti wa kupitisha mswada huu baadae makabrasha yakakaa ndani ya madroo.

Mhe. Naibu Spika, nazungumzia haya kwa sababu huko nyuma alikuwepo Mhe. Adam Mwakanjuki palifanywa utafiti mzuri wa migomba ikawa migomba tunawania hata mimi mwenyewe nilikwenda nikachukua lakini tatizo lake umekwishia wapi utafiti ule wa migomba wa kuzalisha sijui kwa chupa si mtaalam mimi. Tatizo lake tumesahau hata hatujui tena, hilo ndio tatizo letu tulilonalo tunafanya kitu kwa hasara kubwa lakini mategemeo yake ni madogo na hatuwezi tukaendeleza jambo lile.

Naiomba sana serikali hebu tubadilike na suala hili tutakuwa tunalisema lazima tubadilike. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais mwenyewe anasema tubadilike nchi yetu ndogo hii, hawa wataalam wetu wawabadilishe wakulima. Kama mswada unavyosema utafuatilia sehemu mbali mbali, umeeleza mambo muhimu sana mswada huu. Mhe. Naibu Spika, kama mambo haya tutayachukulia tutayavalia njuga basi ni imani yangu kwamba Mzanzibari atajilisha mwenyewe. Lakini je, tunaweza? Ni imani yangu Wazanzibari wanaweza la msingi ni kuwasaidia.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu pia unaweza ukasaidia vijana wetu wengi sana wakapata ajira kwa sababu kuna mkopo hapa, lakini namna ya kuwashajihisha sasa na kuwaweka pamoja kimikoa, kiwilaya au kimajimbo ili kuhakikisha lengo la mswada huu linafanikiwa. Mimi naomba sana Mhe. Naibu Spika, narudia tena hebu tubadilike na wakulima wetu hawana ubishi. Lakini nirudie kama wenzangu walivyosema wataalam tusikae maofisini wale wanaohusika waende kule kwa wakulima. Kila wilaya, kila mkoa ina wataalam wa kilimo, lakini tuulize wangali wanaokwenda kuwasaidia wakulima kule vijijini.

Mhe. Naibu Spika, ni imani yangu kwamba kwanza mswada huu utasaidia sana katika nchi yetu. Mimi nashangaa zamani bibi yangu mzaa baba alikuwa mkulima mzuri tu Mwenyezi Mungu amrehemu aliko, alikuwa analima shamba lake lakini ana kijisehemu analima pishori hii ambayo sasa hivi ndio tunaiita *basmati*. Mhe. Naibu Spika, pishori ilikuwa inalimwa Zanzibar, niungane mkono na mwenzangu Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak amezungumza hapa. Leo mchele unaokuja nchi hii hata kunukia haunukii maana yake tunaambiwa sijui huu ndio mchele mzuri, mapembe ndio kabisa na ndio maana yakaitwa mapembe kwa sababu likikupiga pembe ndio limekupiga tu.

Lakini leo tunasahau tulikotoka na haya yote ni kutokujali jinsi gani mwananchi wetu anasaidiwa katika shughuli za kilimo. Si pishori tu, lakini zamani mimi muhogo najua hii hii Wizara ya Kilimo na Maliasili ilikuwa inafanya utafiti mahogo yanafanywa maonesho hogo mimi na Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak hatuuchukui lakini leo yote yale yamepotea.

Mhe. Naibu Spika, naiomba sana serikali dhamira ya mswada huu ni dhamira nzuri sana kwa wananchi wake. Naomba tuifanyie kazi kwa bidii wataalam wetu hawa wa utafiti wakishakumaliza shughuli zao basi kwa kweli wasaidie.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nilisema nichangie hapa na pale lakini kuna baadhi ya vifungu katika mswada huu naomba nichangie kifungu cha 3 (2) (a) imeelezwa huku kushtaki na kushtakiwa. Naomba sheria ni msumeno tuhakikishe wananchi wetu katika suala hili isije ikawa ndio kisingizio cha kuwa kila wakati ni makesi ya kushtakiwa.

Mhe. Naibu Spika, pia (b) kupata fedha kwa njia ya mkopo. Hili ni suala gumu lakini kama likitekelezwa ni rahisi kwa sababu tumeona katika wizara mbali mbali mikopo inavyokopeshwa tusije tukawa na ubinafsi. Mhe. Naibu Spika, naomba sana zifuatwe taratibu kwa mujibu wa sheria ambazo mkulima ataweza kukopeshwa fedha zile kwa ajili ya kujiendeleza.

Mhe. Naibu Spika, kuna kifungu cha 4 (2) kuna kitu muhuri hapa. Mhe. Naibu Spika, naomba kunukuu “Muhuri wa Taasisi utakuwa umetumika ipasavyo ikiwa umeambatana na saini ya Mkurugenzi.” Hapa sina tatizo. Lakini “au mtu mwengine yeyote aliyepewa mamlaka kwa niaba

yake.” Sasa hapa tunaanza Mhe. Naibu Spika, mimi hili nataka Mhe. Waziri aje anifafanulie maana yake muhuri ni kitu muhimu na hasa kwa ajili ya shughuli hizi ambazo tunazitarajia. Sitokuwa tayari kupewa mtu mwengine muhuri ule kutumia kwa sababu tunaelewana jinsi gani muhuri ule unaweza ukatumika vibaya. Naomba sana Mhe. Waziri hapa aje anieleze masuala mazuri.

Lakini pia kifungu cha 5 (b) kuainisha uzalishaji sera, soko, vikwazo vya utengenezaji na matumizi kwenye kilimo na maliasili au kutayarisha mipango.Watafiti mimi nakubaliana nao sana hawa, lakini je tuseme hii sera inaendana na sasa. Kuna huku mbele nimetia kitu sera, je inakubalika, na sasa hiyo sera ya kilimo ambayo toka hiyo ya utafiti inakubalika na sasa hivi wakati wa sayansi na teknolojia, hakuna marekebisho yoyote katika sera hii. Naomba sana wizara itafiti vizuri kama sera hii inakwenda sambamba na mswada huu.

Mhe.Naibu Spika, kwa vile na mimi nilisema nichangie tu hapa na pale katika mswada huu. Hivi kweli Zanzibar tungule, maana kuna wenzetu wanaita nyanya, tungule zitoke Bara, mabilingani yatoke Bara, vitu vidogo vidogo vitoke Bara, kabeji na karoti. Kweli jamani tunashindwa sisi hapa, wakati zamani sana vilikuwa vinalimwa kwa wingi vitu hivyo, kuna watu maalumu walikuwa wanalima, hata hakuna msimu ukaambiwa leo hakuna tungule wala nini. Hata zile kotimiri, wakati wa enzi hizo Wahindi walikuwa wengi sana hapa Zanzibar, pilipili. Lakini leo mpaka pilipili zinatoka Tanzania Bara. Hivi tujiulizeni kweli jamani hatuwezi vitu vidogo vidogo kama hivi kuvilima.

Marehemu Karume alikuwa anakuambia bustani yako hebu panda vitu kidogo, kama michungwa, miembe midogo midogo, kotimiri, figili, pilipili na kadhalika, unapanda kwenye nyumba yako mwenyewe hununui ndio iwe bustani yako, hebu tujaribu na sisi bustani zetu ziwe vitu kama hivyo, maua panda nje, lakini mule ndani ya uzio ambapo nyumba yako kama ina uzio basi panda vitu vidogo vidogo.

Mimi ukija kwangu Mhe. Naibu Spika, huwezi hata kuingia kwa migomba, ipo karibu karibu na ninashukuru *Alhamdulillah* napata humo, nyumba nzima nimeieneza migomba na hakuna mti hata mmoja niliokuwa sina, basi mibirimbi ndio haisemeki maana Mpemba kwa mbirimbi huna la kumwambia. Kwa hivyo, tujaribu na sisi wenyewe kuchukua mifano ya kupanda vitu vidogo vidogo katika nyumba zetu, ili tuepushe angalau ile senti ya kununulia pilipili au bilingani uifanyie kazi nyengine.

Mhe.Naibu Spika, baada ya kuchangia, nitoe tena pongezi kwa serikali kwamba mswada huu kama tutaufanyia kazi ipasavyo, basi ni imani yangu utaweza kusaidia wananchi wa Zanzibar ili kuhakikisha tunaondokana na upungufu wa vitu vidogo vidogo hata yale mambo makubwa. Kwa hivyo, Mhe.Naibu Spika, naomba niunge mkono mswada huu kwa asilimia mia juu ya mia ahsanate sana.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi kwa mchana huu wa leo kuchangia mswada huu. Mhe. Naibu Spika, kwanza nampongeza Mhe.Waziri kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Kilimo na Maliasili, naamini waziri huyu atakuwa ni mahiri kwa wananchi wake katika kufuatilia hasa shughuli zake za kilimo. Vile vile Mhe. Naibu Spika, nimpongeze Mhe.Waziri kwa kuleta mswada huu Barazani, ili kuweza kuuchangia

na kuwatetea wananchi kwa ujumla. Mhe.Naibu Spika, mswada huu wa kilimo naamini ni mswada mzuri ambao katika kufanyiwa tafiti zake utatuinua katika nchi yetu. Kwanza Mhe. Naibu Spika, kilimo kama si kilimo, kama si uvuvi, kama si maji, kama si ardhi na mambo mengine basi naamini nchi hii haitokuwa nchi iliyokuwa iko makini.

Mhe. Naibu Spika, niende katika kifungu cha 5(b) ambacho kinasema, kufanya utafiti na kutumia utafiti wa kilimo kwenye mazao, mazingira, mifugo, misitu, uvuvi, ardhi, maji, wadudu, maradhi na aina zote zinazohusiana na mambo hayo na mfumo wa viumbe na mazingira. Mhe. Naibu Spika, katika kufanya utafiti wa kilimo au mazingira, kwanza ningeomba zaidi ifanyiwe utafiti ardhi, kwa sababu Mhe. Naibu Spika, ardhi hivi sasa imekuwa ni chakavu, tangu napata fahamu zangu za kuzaliwa, watu wanalima tangu mazao yanapatikana mpaka mazao hayapatikani.

Mhe. Naibu Spika, ningeomba na ardhi ifanyiwe utafiti. Vile vile Mhe. Naibu Spika, tufanye utafiti wa mbegu zetu. Mbegu hizi hazilingani aidha na ardhi yenyewe, au pengine wakulima wenyewe wanakuwa hawajui jinsi ya kuzitumia hizi mbegu.

Mhe. Naibu Spika, nije katika kifungu cha 5(f) naomba kunukuu,

Kifungu cha 5(f)

> "Kuanzisha vituo maalumu vya utafiti, vituo vidogo, maeneo ya miradi na mashamba kwenye maeneo tofauti ya mahusiano ya viumbe na mazingira ya nchi ya kufanyiwa utafiti kwenye maeneo ya kilimo yenye matatizo;

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana na Mhe. Waziri kwamba kufanya utafiti katika maeneo kama hayo. Vile vile Mhe. Naibu Spika, kuanzishwe vituo vya utafiti wa wataalamu katika maeneo ya kila shehia zenye miradi ili kuondoa usumbufu kwa wakulima wetu na wananchi kwa jumla.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye kifungu cha 5(c) kinasema,
Kifungu cha 5(c)

> "Kufanya na kutumia utafiti wa kilimo utakaozidisha uzalishaji kwa kutumia usimamizi wa kisayansi katika mazao, mazingira, wanyama, misitu, uvuvi, ardhi, maji na kuendeleza teknolojia inayofaa, ikijumuisha aina mpya na udhibiti wa wadudu na maradhi;

Mhe. Naibu Spika, kufanya utafiti wa vitu kama hivi na pia kufanywe utafiti kwa wavuvi. Mhe. Naibu Spika, wavuvi wetu na wao huingia katika bahari ambazo wengine wanavua katika bahari inayostahiki na wengine huvua katika bahari ambazo hazistahiki, huvua wengine maji makubwa na wengine maji madogo.

Vile vile huharibu mazingira. Mhe. Naibu Spika, wapo wavuvi ambao hutoka mbali na nchi kama yetu sisi na huingia katika nchi kama hii na wakifika Mhe. Naibu Spika, huvua mpaka uvuvi ambao haustahiki. Suala hili liangaliwe zaidi.

Mhe. Naibu Spika, katika kuangalia suala hili la uvuvi wa maji makubwa, pia waangaliwe na wavuvi ambao wanavua maji madogo, kwa sababu wale wavuvi wanaovua maji madogo

hutegemea ule uvuvi wa samaki wadogo ili wapate kijio na watoto. Vile vile hutegemea uvuvi huo wa samaki wadogo ambao utawanufaisha na wao wenyewe kuendeleza maisha yao. Suala hili pia liangaliwe zaidi.

Mhe. Naibu Spika, kuwapatia wakulima wetu zana za kilimo, kwa sababu zana hizi zimekuwa ni ndogo mno, basi ni vizuri kuwasaidia ili waepukane na kijembe kongoroka. Wananchi wetu Mhe. Naibu Spika, wameshachoka kulima na kijembe hiki cha mkono ambacho kinachosha na kinaumiza sana. Tangu nipate fahamu zangu wananchi hawa wanachezea kijembe mpaka hii leo.

Mhe. Naibu Spika, hebu tuwaangalie wananchi wetu jinsi kilimo wanachokilima, wasaidiwe kwa kupatiwa pembejeo za kilimo na kuwasaidia masuala mengine.

Mhe. Naibu Spika, mwisho naomba yale maeneo ya kilimo ambayo hayatoi tija, basi kiondoshwe kilimo kile ili kupanda kilimo kinachotoa tija kwa nchi yetu hii, ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipatia fursa hii ili niweze kuungana na wenzangu kuuchangia mswada huu muhimu. Vile vile Mhe. Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kutuletea mswada huu ambao unahusu utafiti.

Mhe. Naibu Spika, nianze kuuchangia mswada huu kwa sababu ni mswada muhimu na unatugusa sote, yaani sisi viongozi na wananchi kwa jumla, kwa sababu wengi humu tunahusika na mambo ya kilimo tunalima.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu kama nilivyosema ni muhimu kwetu kufanyiwa utafiti juu ya kilimo, ardhi yenyewe, mifugo, uvuvi na mengineyo yanayohusiana na hayo. Mhe. Naibu Spika, mimi nianze kwa kilimo kwa sababu hasara kubwa sana wanapata wananchi wetu katika kilimo kwa vile wanalima bila ya kuwa na utafiti wowote, wanapanda mimea yao bila ya kufanyiwa uchunguzi, hivyo wakulima huvunjika moyo au hukata tamaa kwa ajili ya mapato madogo wanayo yapata katika kilimo chao. Kwa hivyo, baada ya kujitokeza mswada huu ambao utaweza kufanya utafiti na ukaweza kutusaidia wananchi kuona sasa nakwenda kulima muhogo pale unapostahiki kulimwa muhogo, au nakwenda kupanda mpunga pale unapostahiki kupanda mpunga, basi ni jambo ambalo litaweza kutusaidia sana.

Mhe. Naibu Spika, pia kumeelezwa kwamba kutafanyika utafiti hata wadudu ambao wanaathiri sana mazao yetu. Mhe. Naibu Spika, mimi nipongeze zaidi juu ya hili kwa sababu niseme wakulima wanajitahidi lakini wanapoteza nguvu nyingi wanapopatwa na athari kama hizi.

Kwa mfano, wakulima wa mpunga huingiliwa na viwavi wakati mwengine na mpunga wote ukaathiriwa bila ya kujua nini chanzo cha tatizo hili au vipi tuweze kukabiliana na tatizo hili. Kwa hivyo, utakapofanywa utafiti huu tutaweza kufaidika sana wakulima na kuweza kupata mazao ambayo yataweza kutukwamua.

Mhe. Naibu Spika, lakini utafiti katika mazao, pia suala hili nilipongeze ambapo litafanywa na kuweza kutukwamua na kutupunguzia ukali wa maisha. Wananchi wengine wamejitolea wana

vilimo vyao mbali mbali wana miembe, michungwa na mazao mengine pia. Lakini utakuta unakuja kuingia msimu basi embe zile zinaingiliwa na mafunza na hatimae hasara kubwa inatokea bila ya kujulikana nini chanzo cha tatizo lile au vipi sisi tuweze kukabiliana nalo.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wa nchi hii wengi pia ni wafugaji. Mhe. Naibu Spika, wafugaji na wao ni watu ambao wanakata tamaa kutokana na ufugaji ambao hauna uhakika. Vile vile mifugo inapata maradhi mbali mbali na bila ya kupata ushauri mzuri ambao unaweza kuwasaidia wafugaji ili wakaweza kupiga hatua na wao wakaweza kujikwamua katika umaskini.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, kupatikana kwa mswada huu kama utafanya kazi kikweli, kuweza kufanya utafiti juu ya ufugaji, kuweza kufanya utafiti juu ya wakulima na kufanya utafiti kwa wavuvi basi naamini tunaweza tukafikia pahala pazuri na tukapunguza ukali wa maisha. Mhe. Naibu Spika, ardhi yetu ni ndogo, kama ardhi yetu ni ndogo basi inapaswa hasa kuwa na utafiti wa kina ili tuweze kwenda vizuri katika kuitumia ardhi hiyo.

Mhe. Naibu Spika, mimi kama walivyoendelea wenzangu hapa kusema kwamba mswada huu pamoja na kuwa umechelewa, lakini kwa kuwa kazi ipo inaendelea basi hatujachelewa, mradi tujipange vizuri ili tuweze kuona utafiti huu unatuletea mafanikio makubwa.

Mhe. Naibu Spika, utafiti huu utakapofanya kazi zake kisawa sawa na wakaweza kushirikishwa wale viongozi wetu ambao wanatusimamia katika wilaya zetu, basi naamini tunaweza tukapiga hatua moja kubwa, kwani ndani ya wilaya wenzangu wametangulia kusema hapa kuna mabibi shamba na mabwana shamba, hutuachia sisi tukalima bila ya kupata ushauri kutoka kwao, ndipo pale tunapokata tamaa kwa sababu tunakula hasara katika kilimo chetu, hivyo tumezowea kulima kilimo chetu cha zamani ambacho sio cha kitaalamu na wakati huu tunakwenda kitaalamu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kufanywa utafiti huu na ukaweza kutuwekea bayana kama walivyoeleza wenyewe katika huu mswada, kwamba baada ya kufanywa utafiti katika sehemu zile, wenyewe watapewa yale matokeo ya utafiti ambayo yamefanywa. Kwa hivyo, naamini tukishirikiana na maofisa wetu wa kilimo ambao tunao basi naamini tunaweza tukafikia pahala pamoja pazuri sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilitaka nichangie kidogo juu ya mswada huu na kwa kuwa ni mswada ambao una manufaa makubwa kwetu na tukiweza kuufanyia kazi vizuri, basi utaweza kuleta tija kwetu. Basi na mimi naungana na wenzangu kuunga mkono mswada huu uweze kuchangiwa na wajumbe wenzetu wote na kuupitisha bila ya matatizo, kwa moyo safi ili tukijua kufanya hivi ni kuwakomboa wananchi wetu waweze kufanikiwa katika sekta zao mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache na mimi naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja, ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Naibu Spika, na mimi nachukua nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuweza kuchangia katika suala zima la mswada wetu huu ambao umetukabili hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu kusema kweli ni mzuri, na tutapata nafasi kubwa ya kuweza kuuchangia kwa kirefu, ili mswada huu baadae uweze kuleta faida kwa wananchi wetu. Katika maelezo ya mswada huu ni kwamba una madhumuni ya kuwa tayari umeshatunga sheria itakayoweza kuanzisha taasisi ya utafiti wa kilimo hapa Zanzibar, jambo ambalo ni zuri, jambo ambalo sio geni na ni jambo ambalo tulikuwa nalo kwa muda mrefu, isipokuwa hivi sasa tunataka kuliboresha zaidi au kuliweka katika hali nzuri.

Mhe. Naibu Spika, katika mswada huu pia umeelezea habari ya mfumo, kwamba utakuwepo mfumo mzuri wa utafiti pamoja na usimamizi mzuri. Hilo ni jambo muhimu kwamba, katika utafiti ikiwa tunahitaji kufanya suala hili ni lazima tuweke utaratibu mzuri, pamoja na usimamizi mzuri katika suala zima la tafiti zote za kilimo pamoja na maliasili.

Mhe. Naibu Spika, taasisi hizi zinaonesha kwamba zitapewa uwezo wa kisheria pamoja na kiutendaji. Hatuwezi kuweka taasisi bila ya kuwa na sheria, sheria ni lazima ziwepo, ili tuone hali ya utendaji utakuwa vipi. Kwa hivyo, tunamshukuru Mhe. Waziri kwamba kaweza kufikiria kuweka hii sheria, ili kuweza kudhibiti mambo yote pamoja na mambo ya utendaji.

Mhe. Naibu Spika, katika suala zima hili tunahitaji katika mswada huu wa utafiti, tunahitaji kuwa na rasilimali watu. Lakini tuelewe tu kwamba rasilimali watu kwa mujibu wa majimbo yetu 50 ni lazima tuwe na rasilimali watu kwa majimbo yetu yote 50, ili kuweza kutosheleza mahitaji ya utafiti huo.Kwa sababu hivi sasa naamini kuna upungufu mkubwa sana wa rasilimali watu katika utendaji wa shughuli hizi za utafiti.

Mhe. Naibu Spika, tunahitaji kwa vyovyote vile kubadili hali ya kilimo chetu, na kilimo hakiwezi kuwa kizuri bila kwanza kufanya utafiti.Utafiti ni jambo muhimu sana, katika nchi zote zilizokuwa zimeendelea, basi suala la utafiti limewekwa mbele hasa katika suala la kilimo kwa sababu binadamu ni chakula, na chakula ndio binadamu wenyewe.

Bila ya kula, bila ya kupata maji na bila ya kuweka mazingira mazuri, basi binadamu hatoweza kuishi. Huwezi kuishi bila ya maji, na huwezi kuishi bila ya chakula na chakula kiwe bora, kizuri na kingi.Sasa bila ya kufanya utafiti katika masuala haya, basi nadhani hatuwezi kufanikiwa. Kwa nini mpaka hii leo kuwa utafiti wetu, tumewahi kufanya miaka ya nyuma, lakini bado haujatosheleza katika kiwango ambacho kinahitajiwa.

Mhe.Naibu Spika, kwa hivyo, tunahitaji kubadili mwenendo wetu mzima wa kilimo, kiwe na lengo la utafiti. Mimi nataka niseme kwamba utafiti haukuanza leo, umeanza zamani na tulikuwa na vituo kwa Pemba na Unguja, tukiviita vituo maalum ambavyo vinafanyia utafiti.

Lakini kwa bahati mbaya, sijui ni kwa utaratibu gani ambao tena baadae ulibadilika na ikawa wizara hii haikushughulikia tena mambo ya utafiti. Kwa sababu tulikuwa tunapata maradhi ya namna kwa namna. Kwa mfano, katika migomba kulikuwa na maradhi ambayo yanaitwa *sagatoa* kitu kama hichi. Maradhi haya yalikuwa yameenea katika migomba, na ilikuwa migomba mingi inaanza kufa na ilikuja wakati ing'olewe migomba yote, kila inayopandwa inakufa tena vile vile. Kwa hivyo, inaonesha kwamba utafiti haukuweza kudumishwa, ili kuona kwamba maradhi ya migomba yamepotea.

Mhe. Naibu Spika, si hayo tu hata ukitizama katika miti yetu ya michungwa, baadhi ya miti mingi midogo midogo utakuta wadudu ni wengi na hapajafanywa utafiti wowote. Kwa hivyo, lengo la mswada huu ni kutaka kuweka udhibiti wa maradhi.Maradhi yapo ya kutosha, tumeona maradhi ya migomba, mihogo, mboga mbali mbali, miembe na pia tumeona maradhi katika matunda mbali mbali katika nchi hii.

Mhe.Naibu Spika, mimi naipa heko wizara kwa kuweza kuliona hilo suala na kuweza kulifanyia utafiti wa hali ya juu, ili kukomesha matatizo haya. Tuelewe kwamba kadiri maradhi yatakavyoongezeka katika miti yetu na wanyama wetu, basi tujue kwamba ni upungufu wa uzalishaji. Kila maradhi yakiwa mengi na uzalishaji unakuwa ni mdogo. Kwa hali hii wizara ijikite katika kudhibiti na kuhifadhi maradhi haya. Tutakapodhibiti na kuhifadhi maradhi haya, basi ndio kusema kwamba tutaongeza tija katika uzalishaji. Tuna mipunga baadhi ya wakati inapata hujuma ya wadudu, hivyo tunahitaji kudhibiti mipunga yetu ili isiharibiwe, na kuweza kuongeza uzalishaji na tija iweze kupatikana.

Mhe. Naibu Spika, katika wizara ambayo imebahatika, tunaweza kusema ni Wizara ya Kilimo na Maliasili, kwa sababu wizara hii ina wataalamu wa kutosha na wenye elimu ya juu. Lakini hali halisi inavyojitokeza pamoja na kuwa sifa hii ipo, lakini bado mapungufu yapo makubwa sana.

Mimi nafikiri tujiandae tuone hali halisi ya wananchi wetu, kwa sababu wanaopata shida ni wananchi wetu. Kwa hivyo hawa wataalamu waliopo na wengine watakaoweza kupatikana, waweze kusambazwa katika maeneo yetu yote ya kilimo, ili tuweze kufanikiwa katika suala hili. Hivyo, kama tuna wataalamu wa kutosha basi wagaiwe kwa mujibu wa majimbo yetu tuliyonayo.

Mhe.Naibu Spika, tunahitaji kuwa na nyenzo za kufanyia kazi, pamoja na kuwa tutakuwa na wataalamu wa kutosha, lakini inawezekana wataalamu hawa washindwe kufanya kazi zao katika maeneo tuliyoyataja. Kwa hivyo, nafikiri hapa wizara itaweza kusimamia vizuri shughuli zake za kuona kwamba wanapata nyenzo za kutosha, ili waweze kukabili matatizo haya ya utafiti pamoja na kudhibiti maradhi ya ndani ya nchi.

Mhe.Naibu Spika, mimi naamini kwamba katika utafiti huu bila shaka utagaiwa kwa muda maalum.Labda wanaweza kupanga kwamba tuweze kufanya utafiti wa muda mfupi na utafiti wa muda mrefu.Suala hili utakuta ni muhimu sana kwa wizara hii kuweza kupanga mipango mizuri, yaani mipango ya muda mfupi na mipango ya muda mrefu kwa mujibu ya rasilimali watu alionao.
Mhe.Naibu Spika, sasa tuelewe kwamba katika dunia ya leo hatuwezi kuishi kama watu wa pangoni. Watu wa pangoni walikuwa hawana elimu ya kutosha na walikuwa wanaishi katika maisha yao wenyewe walivyotaka kuishi.Lakini kwa dunia hii ya leo ambayo tunaidhibiti kwenye vidole vyetu, dunia ambayo ina mtandao wake mkubwa sana, hatuwezi tukaishi katika dunia hii ikawa na sisi tusijue lile tunalolifanya.Tunahitaji katika wizara hii kwa sababu ni wizara ambayo wananchi wanaitegemea kwa wingi, hususan katika suala zima la kilimo.

Sasa kama wizara hii haitoweza kufanya jambo likajulikana, na likaweza kuleta tija katika nchi hii, basi utafiti wa maradhi ambayo yametuzunguka, ambapo tulifanya kwa mara ya kwanza tumeona maradhi yalikuwepo halafu yakaachiliwa mbali, ikasemekana kwamba hakuna fedha za

kutosha kuondoa maradhi hayo.Kwa hivyo, ni muhimu kwa dunia ya leo kwamba kama wananchi tunataka tuwasaidie katika kujikomboa kwenye kilimo, basi uzalishaji uwe mkubwa, basi tunahitaji utafiti ufanywe kwa kina, ili matatizo madogo madogo yaondoke.

Kwa hivyo, katika suala la utafiti tunahitaji kuonesha taaluma yetu nzuri ambayo tumejifunza, wataalamu wetu walionao ni lazima wajikite katika dunia ya leo ya sayansi na teknolojia, ili kuweza kudhibiti mambo yote kwa mujibu wa hali ilivyo.

Mhe. Naibu Spika, katika suala zima ni lazima tufanye utafiti ambao ni wa shirikishi, sio Wizara ya Kilimo na Maliasili peke yake ifanye jambo peke yake. Tunahitaji kuwashirikisha wananchi ili wajue nini linawahitaji kufanya.

Mambo kama haya Mhe. Naibu Spika ni muhimu sana, sio kwamba tunatengeneza miswada na kuweka miswada ya sheria, baadae ikishapita kwa Rais inarudi tena kama ni sheria na baadae inatupiliwa mbali ndani ya makabrasha, na makabrasha hayo yanawekwa ndani ya makabati tunamaliza leo leo, halafu baadae hilo suala zima tunaliacha njiani.

Mhe. Naibu Spika, haya tunayozungumza wananchi wanayasikia na wanajua kwamba sasa hivi Wizara ya Kilimo na Maliasili, imejikita kabisa katika kuleta maendeleo nchini mwetu na kuwasaidia wananchi katika kujikomboa. Kwa hivyo, utafiti ni lazima ufanywe, na wananchi wajue kwamba kweli utafiti unafanywa, wananchi lazima washirikishwe, wananchi lazima wapewe misaada ya kila aina. Ni lazima wizara hii ishirikiane kikamilifu na wananchi kama suala hili linatakiwa lifanikiwe, basi ni lazima waelimishwe wananchi katika suala zima la maradhi tuliyonayo.

Mhe. Naibu Spika, utafiti huu ni mzuri sana kama utaanza na fedha zipo za kutosha katika utafiti huo, kwa sababu utafiti unahitaji fedha ni lazima Wizara ya Kilimo na Maliasili ijitahidi katika kuweka fedha zake kwa wingi, ili kuweza kufanikisha suala hili la utafiti.

Kwa mfano, tukiingia katika suala la chakula, basi bila shaka chakula tunahitaji kujua kama ni mpunga, kama ni mihogo na kama ni viazi. Hujuma ya wadudu ni suala muhimu sana, ni lazima ihakikishe katika suala zima la chakula, basi maradhi haya yanaondoka na tunapata chakula kwa wingi na tija inapatikana na lengo lililokusudiwa linafikiwa.

Mhe. Naibu Spika, tukiingia katika masuala ya matunda ambayo ni suala muhimu sana kwa binadamu. *An orange a day keeps a doctor away* au sivyo, tunahitaji tuwe na uzalishaji wa matunda kwa wingi, kwa sababu huwezi kula vyakula vya *carbon hydrates*, ukala vyakula vya *protein* bila ya kupata matunda haiwezekani, itakuwa *balance diet* haijapatikana. Kwa hivyo ni lazima tuwe na matunda kwa wingi. Suala hili ni muhimu katika wizara hii, ili kuhakikisha kwamba tunazalisha matunda kwa wingi kwa maslahi ya wananchi wetu. Mhe. Naibu Spika, kama matunda haya yameingiliwa na wadudu ni juu ya wizara hii kuhakikisha kwamba inafufua.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano kule kwetu tulikuwa na *Matangatuani Agricultural Station* ya kudhibiti maradhi, pamoja na kuwasaidia wananchi katika kilimo.Ile *station* ipo, lakini hakuna linaloendelea. Hakuna nyenzo, hakuna dawa wala hakuna kitu chochote.Kwa hivyo, tunahitaji wizara hii sio kuzungumza tu, lakini kuna mambo mengi yanahitajika.Ikiwa ni masuala ya

matunda basi tuhakikishe kwamba matunda tunayo kwa wingi na yameanza kudhibitiwa na wadudu ambao wanaathiri.
Mhe.Naibu Spika, tukija kwenye suala la wanyama, kama tunataka uzalishaji kwa wingi basi ni lazima tuhakikishe kwamba ng'ombe wetu na kuku wetu tunawaweka katika hali nzuri.Tuache wale ng'ombe wa zamani, *tradition cows* ambao wanazalisha lita moja na nusu ya maziwa. Sisi sasa tunakusudia kuweka ng'ombe ambao ni *multipurpose* kwa dhamira ya kuwa tunachinja na tunatoa maziwa, hiyo ndio *multipurpose* ya kufuga wanyama.

Sasa kama tutapata wanyama wenye dhamira hiyo ya kuchinja na kupata maziwa, basi wizara ijikite katika suala hili kwamba tunao wanyama wa kutosha kwa mujibu wa idadi ya watu tulionao nchini.Tunahitaji idadi kubwa ya wanyama ili tupate nyama ya kutosha. Lakini Mhe. Naibu Spika, wakati huo huo wizara hii inahitaji kuhifadhi wadudu ambao wanaathiri wanyama hawa. Kama ikiwa ni *tradition cows* tunaendelea nao mpaka leo, basi ng'ombe wetu wa asili ambao uzalishaji wake ni mdogo bado hatujafanya kitu. Ni lazima wizara hii ijikite katika kuhakikisha kwamba inaleta ng'ombe wa kisasa, ambao wanahitaji kutunzwa kwa hali ya juu, wana maradhi ambayo yanawaathiri kama maradhi ya kupe, kwa hivyo ni lazima wahifadhiwe na wananchi wapatiwe dawa za kutosha.

Mhe. Naibu Spika, katika suala hili kama tunahitaji kuongeza nyama pamoja na maziwa, ni lazima tupate dawa za kuweza kuwasaidia wanyama hawa. Kwa hivyo, ninalomuambia Mhe. Waziri ni kwamba tunahitaji kuweka bei nafuu ya dawa kama tunataka uzalishaji mzuri na tunahitaji kupata nyama kwa ajili ya afya zetu, tunahitaji kupata dawa na dawa hizi ziwe kwa bei nafuu, kwa sababu dawa za wanyama ni ghali sana.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo nahitaji kuzungumza ni suala la misitu. Mhe. Naibu Spika, misitu ni suala muhimu sana katika nchi yetu, tunahitaji kuwa na misitu mingi ili kuweza kuleta mvua ambayo ndio itakayosaidia kilimo, bila ya misitu basi mvua inaweza ikatukimbia. *Barren world* haina maana, *semi-arid land* hazina maana haziwezi kuleta mvua. Ni lazima kata mti panda mti hili ni suala muhimu sana, tukiongeza idadi ya miti tutaweza kupata uzalishaji wa mbao, tutaweza kupata kivuli na wanyama wetu wanaweza kustirika katika vivuli.

Kwa hivyo, suala la misitu ni muhimu sana na ni suala la kuweza kusimamiwa na kama kuna maradhi ya miti iweze kufuatiliwa na utafiti huu. Mhe. Naibu Spika, mimi naona katika mambo mawili, jambo moja itakuwa ni msitu na jambo la pili itakuwa ni vitu ambavyo tunavyoviotesha. Tunaotesha mpunga, mihogo, viazi, majimbi na kila kitu tunaotesha. Kwa hivyo, kuna sehemu mbili hapa. Kuna sehemu moja ya kuangalia kwenye misitu na kuna sehemu moja ambayo sisi wenyewe tunataka tuvioteshe vyakula vile. Hivyo, ni suala la kuangalia utafiti wa hali ya juu, hasa katika masuala ya maradhi.
Mhe. Naibu Spika, tuna suala la uvuvi katika nchi hii. Samaki tunao wa kutosha na kwa wingi lakini hawajafanyiwa utafiti. Kuna samaki ambao sasa hivi wana umri zaidi ya miaka mia katika bahari hawajaweza kuvuliwa, wanachokifanya wananchi wetu ni mama kanipa mzima, uwezo wake wa kuvua ni samaki wadogo wadogo, ingawa ni muhimu vile vile kwa maskini ambaye anaweza kumnunua. Lakini hata hivyo maskini atakula hao wadogo wadogo na yeye wale wakubwa anawahitaji kula ili ajenge afya yake. Kwa hivyo, bado tunao samaki wa kutosha.

Mhe. Naibu Spika, kilimo sasa hivi kimepewa mzigo mkubwa sana, kimeingizwa mpaka katika sehemu hizo, ni *world range* kwa kweli imetembea Wizara ya Kilimo na Maliasili. Kwa hivyo, hii ni kazi kubwa kuhakikisha upande wake kwamba tunapata samaki wa kutosha kwa ajili ya kujenga afya zetu na kuweza kusisitiza kwamba tuweze kupata boti kubwa kubwa, ili kuweza kuvua kwa wingi tule samaki kwa wingi, chakula kidogo samaki wengi, chakula cha samaki kiwe kingi kuliko wali wetu tunaokula au muhogo wetu.

Unaonaje pale unapoliweka jichwa la samaki kwenye muhogo, huku kuna *carbohydrate* ambayo haina nguvu, muhogo una *temporary energy* ambayo nguvu zake ni ndogo, hauna nguvu sana ile ni *starch, carbohydrate* nguvu zake ni *temporary energy* ni ya muda mfupi.Lakini ukiongeza kichwa la samaki au vichwa viwili ya samaki juu ya muhogo basi unaongeza *energy* ya kutosha.Kwa hivyo, tunasema uvuvi utatusaidia tuweze kupata kuongeza idadi yetu ya nguvu za mwili.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe malizia.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Namalizia Mhe.Naibu Spika, la mwisho, nasema kwamba nahitaji kumwambia Mhe. Waziri tuangalie *situation* yote ya kilimo ni nani hasa ambaye anafanya kilimo, hebu tuangalie ni wanaume au ni wanawake. Mimi ninachohisi hapa ni kwamba wanawake ndio wanaokwenda katika sehemu za kilimo.Kwa hivyo, nataka nimwambie Mhe. Waziri kwamba awapongeze sana wanawake, awasaidie sana wanawake na awaangalie sana wanawake katika suala zima la kilimo.Kwa sababu wao ndio wanaopoteza muda wao wote katika suala zima la kilimo. Vijana wetu ambao tulionao katika mji huu hawataki kazi, wanazurura katika miji, tatizo lao ni kuhangaika katika dawa za kulevya. Lakini wanawake mawazo yao yote yako katika kilimo.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa wakati wako ulionao na mimi umeshaanza kuniambia nianze kupumzika kwenye suala hili. Mhe. Naibu Spika, kwenye suala hili naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia kwa mia pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Konde, ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe, kwa michango yenu na tumebahatika asubuhi kuchangia wajumbe 10, na wajumbe 10 watachangia jioni.

Kwa hivyo, nawaomba walioleta majina hawajatajwa basi wafike mapema ili wapate kuchangia.Baada ya maneno hayo naakhirisha kikao hiki mpaka saa 11 jioni leo.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11.00 Jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, nashukuru na mimi jioni hii ya leo kunipatia nafasi ya kwanza kuchangia juu ya mswada ulio mbele yetu hapa. Pili nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii aidha napenda kumshukuru Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili,

kuteuliwa kwake kuwa Waziri wa Wizara hii na uanzishaji wake makini wa mswada huu, kwa hivyo nimpe pongezi za dhati na nimtakie kheri na mafanikio katika utendaji wake wa kazi katika kazi hii mpya aliyopewa.

Nafahamu kuwa kilimo ni moja katika Wizara muhimu za serikali yetu kwani ina mahitaji ya chakula kwa watu wetu, pindipo Wizara hii ikiwa makini ikajipinda kwa ufanisi kutekeleza majukumu yake, imani yangu iko siku itafika mapembe hatutoagizia tena.

Mhe. Spika, tunanzisha taasisi hii ya utafiti wa kilimo, utafiti ni jambo la msingi katika suala lolote lile ambalo linaanzishwa kwa sababu kuanza kitu bila ya utafiti ni kubahatisha, hivi sasa hatuko tena wakati huu kubahatisha lazima tufanye mambo yetu kwa uhakika na uhakika wake ni kufanya utafiti kwa masuala yetu yote.

Mhe. Spika, ardhi yetu tunayoitumia katika shughuli zetu za kilimo ni ndogo na sehemu hiyo hiyo ndio waliyokuwa wakitumia mababu, mababa ndio tunatumia sisi kwa hivyo kwa kima Fulani ardhi imezeeka na imechakaa, kwa hivyo kuna haja kabla ya kufanya utafiti wa haya mambo ya kilimo nah ii ardhi nayo pia inahitaji kufanyiwa utafiti ili tuweze kujua ni katika eneo gani, zao la aina gani litaweza kustawi na kuleta tija kama ile tunayoitarajia.

Hivi sasa wakulima wetu walio wengi zaidi vijijini wanalima kwa kubahatisha kwa sababu hakuna utafiti maalum uliofanywa juu ya sehemu ambayo wanalima, wala utafiti wa mbegu ambayo wanatumia. Kwa hivyo ipo haja tena kubwa ya kufanya utafiti juu ya ardhi, mbegu na aina gani ya mbegu inastahili pahala Fulani na n.k.

Mhe. Spika, Wizara ya kilimo hapa hapa imekusanya mambo kadhaa, imekusanya kilimo chenyewe, mazingira, tawala za mikoa hata Wizara ya Fedha nayo imo katika Wizara ya Kilimo, kwa hivyo hapa nije kwenye mazingira, mazingira yetu yatakapochafuka na yatakapoharibika ardhi yetu haitoweza kutupatia kama vile tulivyotarajia na hivi sasa tunashuhudia uchafuzi mkubwa na uharibifu mkubwa wa mazingira.

Mhe. Spika, uharibifu na uchafuzi ni mambo mawili tofauti, uchafuzi wa mazingira ni kuweka taka taka ambazo zinahamishika lakini ikawa zinalundikana bila ya kuchukuliwa hatua. Uharibifu ni uchimbaji ovyo wa kifusi, mchanga, ukataji ovyo wa misitu na mambo mengine hapa huwa tunaharibu mazingira, tunapokata misitu ovyo tunaifanya nchi yetu iwe nusu jangwa na ikiwa nusu jangwa mvua inapungua kilimo kinakuwa cha muda ambacho hakiaminiki. Kwa hivyo lazima wataalam wetu wafanye utafiti wa kutosha juu ya matumizi bora ya ardhi ili tusifike pahala ikawa hata muhogo haumei tena.

Mhe. Spika, kilimo ni uti wa mgogo wa taifa leto hivi sasa na kuna haja mazao yote ikiwa muhogo kufanyiwa utafiti ni mbegu gani inastawi vyema katika eneo Fulani, kwa sababu sisi tunafanya mambo yetu vizuri yakishaelekea tunayaacha tukiwacha wakishughulikia wananchi tunarudi pale pale, kuna kipindi tulifanya utafiti wa mbegu bora ya muhogo na ikawa tunapanda muhogo kitaalam na ilikuwa watu wanapata mazao mazuri ya mihogo. Lakini baadae suala hili halikuendelezwa watu wa kilimo hawakutilia mkazo utafiti huu wala uoteshaji huu wa mhogo, kule Kizimbani alikuweko Maalim Bena kwa kilimo ni mzuri tu akifanya utafiti wa vipando

mbali mbali sasa kwa kiasi Fulani yale aliyofanya nyuma yameachiwa sasa tumerudi tupp pahala ambapo tunaanza upya.

Uchafuzi wa mazingira baadhi ya wakati pia unasababisha uchafuzi wa vyanzo vya maji, lakini sasa tuna upungufu mkubwa wa maji katika sehemu zetu mbali mbali za visiwa vyetu kutokana na matumizi yetu mabaya kwa ardhi yetu, kwa hivyo iko haja ya makusudi watu wa utafiti wa mazingira waibadilishe jamii ili iweze kutumia ardhi kwa jinsi ambavyo ardhi inafaa kutumiwa.

Mhe. Spika, mazo ya kilimo ni mengi miti ya kilimo ni mingi lakini sasa hivi tumeshuhudia matunda mbali mbali yanaathiriwa na wadudu waharibifu wa matunda, hii pengine kutokana na kuwa hatuna udhibiti bora wa uingizaji wa vyakula au matunda kutoka nje ya Zanzibar, hivi sasa tunaagizia tungule kutoka Tanzania Bara, mara nyengine mananasi hata matikiti bila ya kufanya utafiti kwamba yale ni salama hayana maradhi ya aina yoyote.

Lakini tunaingiza kama hayana athari yoyote hatimae na sisi huku kwetu wakati tunaotesha matunda kama yale tunapata matatizo, zamani tungule zilikuwa zinatoka Mwambe kwa Mhe. Hija Hassan Hija ilikuwa zinatutosha wala zilikuwa hazia wadudu wowote waharibifu, lakini ulipoanza mtindo wa kuagizia tungule kutoka Tanzania Bara hata tungule sasa hivi nazo zina athari ya wadudu waharibifu, tungule, migomba, embe, mananazi, machungwa muhogo ndio kabisa ina wadudu weupe wale.

Kwa hivyo hiki kitengo cha utafiti ni muhimu kweli kweli na kifanya kazi yake kwa kujipinda barabara ili kuweza kutukwamua hapa tulipo, aidha wafanye utafiti wa hili zao kubwa la biashara za karafuu kwa kupandikiza miche mizuri, sehemu nyingi wakulima wa mikarafuu wana hiyari ile mikarafuu wanayong'oa mwituni kuliko ile inayotoka kilimo, wanadai hii ya kilimo umri wake ni mfupi sina uhakika lakini wakulima wanasema bora wang'oe kule porini wapandikize utaishi muda mrefu kuliko huu ambao umelelewa kitaalam. Kwa hivyo kama hoja hii ni kweli watu wa kilimo wangefanya utafiti itakuwaje ule wa porini uwe ni bora kuliko ule uliolelewa vizuri ukawa hauna ubora, kwa hivyo ni kazi ya watafiti kufanya utafiti huo itakuwaje kitu ambacho kimeengwa engwa, kimetunzwa kikakosa ubora lakini kilichoko porini kikawa bora zaidi.

Mhe. Spika, kuhusu mifugo tumekuwa nashirika mbali mbali kama PADEP wafugaji wengi walichukua ng'ombe, sasa ng'ombe walitoka maeneo ya Tanzania Bara sehemu ambazo zina baridi wakaletwa Unguja na Pemba maeneo ambayo ni joto sana zaidi ya asilimia 60 ya ng'ombe tulioagizia wamekufa, hapa ni kwa sababu hakuna utafiti wa kina uliofanywa na Wizara ya Kilimo kabla ya kuingiza ng'ombe hawa.

Mhe. Spika, mimi binafsi katika shehia yangu mradi huu wa *PACEP* uliingia na tulinunua ng'ombe 24 majike na dume moja, hivi sasa wamebakia ng'ombe tisa tu na wengine wote wamekufa kulingana na kutofanya utafiti wa kutosha, wataalam wenyewe wanasema aa lakini ni mradi ambao wananchi wenyewe wameupenda ndio, lakini nyinyi ndio wajuzi wa kuwashauri vyema kwa ule mradi ambao utaleta maendeleo.

Ingawaje mara nyengine wanakufa kwa kukosa matunzo bora, lakini pia na hali ya hewa inachangia kwa sababu hali ya hewa walikotoka na walipo haikubaliani. Kwa hivyo ipo haja

kabla ya kuingiza mambo ya namna hii Wizara ya Kilimo ikafanya utafiti ili wakulima na wafugaji wasipoteze nguvu zao bure, kwa sababu ng'ombe hawa wanalelewa kuliko mtu anavyomlea mwanawe.

Mhe. Spika, ng'ombe huyu umjengee banda, hafugwi mwituni huyu atafutiwe majani ale pale pale, atafutiwe vyakula vyengine vya kununua vya gharama, apigwe sindano hatimae asubuhi unaamka unamkuta amekufa, wakati umemnunua kwa pesa nyingi sana kwa hivyo tungewaomba watu wa kilimo wafanye utafiti wakati tunapoingiza hii mifugo ya ng'ombe, kuku na mbuzi.

Mhe. Spika, kuku wetu wa kienyeji kule Pemba kuna ugonjwa tunaita (magwa) sijui Unguja unaitwaje, huu unakuja mara kwa mara hasa siku za kiangazi kama hizi hakuna utafiti wa kina unaofanyika magonjwa haya sababu yake ni nini, sasa watu wanafuga baada ya muda mfupi kuku wote wanakufa wanabakia makoo mawili anza upya, wakati wa mago unapokuja atena wanakufa vile vile kwa sababu hakuna utafiti wa kina unaofanyika. Kwa hivyo ningeiomba Wizara hii chini ya kitengo hiki cha utafiti ambacho tunakianzisha kijitahidi kadri watakavyoweza kufanya utafiti wa kina juu ya mazao ya mifugo na mazao mengine ya kilimo na misitu.

Mhe. Spika, kama ingelikuwa kuna ufuatiliaji ulio barabara kwa wakulima wetu na wafugaji wetu leo ingelikuwa tunakunywa maziwa kwa wingi tena ya ng'ombe, tunakula matunda kwa wingi, tungekuwa tunakula nyama kwa wingi. Lakini matokeo yake kwa sababu ng'ombe tunaoagizia wanakufa kwa maradhi sasa hivyo tunakosa nyama, wanakosa matunzo mazuri tunakosa maziwa.

Mhe. Spika, katika bajeti ya mwaka 2012 ya Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mkoa wa Kusini Pemba hujipangia kulima ekari kadhaa za kula mbali mbali, kama ekari zile zingalilimwa kweli kweli zikashughulikiwa kitaalam basi nina hakika tungelikuwa hatuagizii mchele kutoka Mbeya, hatuchukui nanasi kutoka Tanzania Bara, hatuchukui kunde kutoka nje ya Mkoa wa Kusini Pemba. Lakini kwa ukosefu wa utafiti watu wanalima lakini matokeo yake mazao yanayopatikana ni kasoro ya yale yaliyotarajiwa. Kwa hivyo nasisitiza Mhe. Spika, umuhimu wa kitengo hiki cha utafiti ili uweze kufanya kazi yake kwa maslahi na manufaa ya wakulima na wafugaji wetu.

Kadhalika tuna mazao ya baharini samaki na mengineyo, haya bado yanahitaji kufanyiwa utafiti wa kutosha kwa sababu inasemakana kuna samaki ambao wanarundikana ambao bado hawajavuliwa, lakini tunakosa utaalam na zana bora za uvuvi. Mhe. Spika, hivi sasa maeneo mbali mbali yameanzisha ufugaji wa samaki sina hakika kuwa sehemu hizi watu wamejenga mabwawa ya samaki wamefanya utafiti wa kutosha mpaka kuwekeza hilo bwawa, vyovyote vile utafiti ni jambo la lazima.
Mhe. Spika, sisi tuna sheria nyingi na nzuri kama mtu aliyekuweko nje ya Zanzibar akisikia mambo yetu tunavyoyapanga basi mtu huyo ataona Wazanzibari wanaishi vizuri sana, kwa sababu tuna mipango mizuri lakini matokeo yake utendaji wake ni mdogo.

Kulikuwa na msemo mmoja wa zamani kidogo unasema " *Mipango yetu yote kama ingekuwa mizuri ikaenda mpaka utekelezaji basi kwa kweli tungelifarajika na tusingelitaka misada tena".* Wala kufadiliwa tena kama waombaji wangelikuwa ni farasi wanafarajika wanapanda na sisi

tungelifarajika kwa sheria zetu nzuri tunazozitunga lakini hatimae uwekezaji wake ukawa una kasoro kidogo na kila siku tunapanga hivi na vile.

Kwa hivyo Mhe. Spika, utafiti wa kilimo, Maliaisili na Mazingira unahitajika ili tuweze kutoka hapa kwenye kilimo tulichonacho na tuingie katika kilimo cha kisasa, mara zote tunapozungumza kilimo wakulima wetu walio wengi wanalima kwa kijembe kongoroka nikutie mbanio mabonde yaliyo mengi watu bado wanaendelea kulima kwa jembe la mkono. Kwa hivyo muda mwingi mkulima anautumia kwa kulima kuliko ule anaopumzika, jembe la mkono watu wetu wanahiliki kweli kweli kwasababu ni kazi nzito na ngumu lakini bado hatujafikia hatua ya kuona kuwa wakulima tunawapunguzia huu mzigo wa kijembe kongoroka, tunapata matreketa wakati mwengine maeneo hayendi sio mara nyengine lakini mara nyingi.

Mhe. Spika: Mheshimiwa zingatia muda.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Spika, ili tufike pahala pazuri nasisitiza kuwa Taasisi hii ya Utafiti ianzishwa na ifanye kazi zake kwa kuzingatia matakwa ya nchi. Baada ya kusema hayo machache Mhe. Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mhe. Asha Abdu Haji: Mhe. Spika, ahsante sana kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia na kutufikisha hapa jioni hii na kutupa afya njema. Pili napenda kumshukuru Waziri wetu kwa kutuletea mswada huu ili tuweze kupata mafanikio ya baadae.

Mhe. Spika, kwa kuwa uchunguzi ni muhimu ningeiomba Wizara hii ifanye maabara ya Sayansi ili kutupatia ufumbuzi wa vidudu vya maradhi ya miti hii, tukakapofanya uchunguzi tukachukua kidugu tukakipeleka maabara tutajua haya ni maradhi Fulani na tutafanya utafisi na kutafuta dawa yake, kwa kuwa wananchi wanajitahidi sana na kilimo lakini hawana soko na ningeiomba Wizara yako ijitahidi kutupatia viwanda ili mazao yale yanapokuwa mengi hususan siku za msimu tupate kushindika na yatufae baadae.

Mhe. Spika, kwa kuwa tumesema kwamba utafiti wa vidudu ni muhimu kutokana na kwamba hivi juzi juzi wilayani kwetu hususan ukanda wa pwani kulikuwa na matatizo na maradhi, yaani yakishafika maji kujaa watu wote wanawashwa mpaka kwenda pua na kwenye koo na watoto wadogo waliathirika na kufanya vidonda. Sijui wizara yako inayo habari na tatizo hili na ikiwa ina habari ilijiandaa vipi na imejua ni maradhi gani ambayo yametufika katika ukanda ule.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, na mimi nachukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipatia fursa hii ili niweze kutoa mchango wangu kwa ufupi kwenye mswada huu wa kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo.

Mhe. Spika, na mimi nimpongeze kabisa Mhe. Waziri kwa upande wa uteuzi kwa kuingia Wizara hii na vile vile nimpongeze Waziri aliyepita kwa sababu yeye aliondoka na kaulimbiu ya merika, na leo anaingia huyu na kauli mbiu ya kuanzisha utafiti.

Mhe. Spika, dhana ya kuanzisha jambo hili ni dhana nzuri na kwakweli imekuja kwa wakati ingawa tumechelewa kidogo lakini Wazanzibari wanahitaji, ni vuziri kwa sababu itaondosha kufanya kilimo kwa mazoea lakini vile vile Wazanzibari watapata hasa uwezo wa kuwatumia wataalam ambao tunao, wenzangu wamesema hapa kwamba Zanzibar na hasa Wizara ya kilimo tuna wataalam wengi lakini bahati mbaya hatuwatumii ipasavyo kuleta tija ndani ya mikono ya wazanzibari. Kwa hivyo na mimi nasema kuanzishwa kwa taasisi hii ni muhimu na Wazanzibari wanasubiri kwa furaha kubwa ili matunda ya taasisi hii yaweze kuwafikia Wazanzibari.

Mhe. Spika, kwenye sehemu ya ufafanuzi kuna tafsiri ya vitengo vya utafiti kwenye mswada huu ukurasa wa kumi na saba tumeelekezwa kwamba tafsiri hiyo itapatikana kwenye kifungu cha ishirini na mbili cha sheria hii nimejaribu kutafuta sijakiona. Sasa hapa Mhe. Waziri akija labda anisaidie tafsiri ya vitengo vya utafiti tumeambiwa kwamba viko kwenye ukurasa wa ishirini na mbili lakini kadiri ninavyoangalia sijaona maana ya neno hilo kwa hivyo Mhe. Waziri atusaidie pale atakapokuja kutoa ufafanuzi.

Mhe. Spika, jengine ni kifungu cha tano cha sheria hii kwenda suala zima la kazi na uwezo wa taasisi, Mhe. Spika, hapa kuna kazi kuanzia (a) hadi (m) mimi nashauri kwamba tuongeze na (n) kwa sababu tumeweka kazi nzuri, lakini nina wasi wasi kwamba pamoja na uzuri huu maafisa wetu watashindwa kufanya kazi kwa sababu hivi sasa tunao wataalam wengi hapa Zanzibar lakini kazi hazifanyiki kwa sababu hawana nyenzo. Kwa hivyo napendekeza Mhe. Spika, tuongeze (n) kuwapatia nyenzo wataalam husika vyenginevyo tutakuwa na kazi nzuri za maana lakini wataalam wanashindwa kufika vijijini kwa sababu hakuna nyenzo.

Kwa hivyo Mhe. Waziri nakuomba sana kwamba moja kazi ya tafsiri hii ni kuwapatia nyenzo wataalam wetu ili waweze kufika sehemu husika za vijijini, lakini vile vile kazi ya (l) ambayo inasema ni kuanzisha na kuendeleza kituo cha taarifa za utafiti Mhe. Waziri naomba unielimishe je kituo hiki kitakuwa na uwezo wa kuwasaidia wale watu walioko nje ya Zanzibar kuweza kuziona taarifa hizi, yaani kitakuwa kitakuwa na *access* ya kutoka kwamba wageni au Wazanzibari waliokuwepo nje ya nchi watakapohitaji kupata taarifa za utafiti huu hapa Zanzibar waweze kuzipata hata kabla ya kuja hapa Zanzibar. Nataka nielimishwe kwamba kituo hichi watu ambao wapo nje ya Zanzibar watakuwa na uwezo wa kupata taarifa hizi bila ya kufika hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, jengine ambalo nataka Mhe. Waziri anisaidie ni kifungu cha 6(b). Hapa kuna uongozi wa taasisi kifungu cha (a) Mwenyekiti ambaye anateuliwa na Rais, sina tatizo. Kifungu cha (b) na wajumbe wengine wanne ambao angalau wawili kati yao hao wawe wanawake watakaoteuliwa na Mhe. Waziri kuhusiana na taasisi.

Mhe. Spika, sina tatizo na wanawake, naunga mkono kwamba katika hao wanne na wanawake wawemo. Lakini ninaomba Mhe. Waziri azingatie kwamba sasa hivi ni wakati wa kutosha wa kuweka mjumbe mmoja lazima atoke Chuo Kikuu cha Taifa cha Suza.

Mhe. Spika duniani kote Chuo Kikuu cha Taifa, ndio chuo ambacho husaidia maendeleo ya nchi. Namshauri sana Mhe. Spika, kwamba lazima katika wajumbe wanne hawa tuseme kabisa kwamba mjumbe mmoja atoke Chuo Kikuu cha Taifa cha SUZA, ili chuo chetu kiweze kutoa mchango kwa maendeleo na tafiti hapa Zanzibar. Vyenginevyo haipendezi kwamba kila siku

tutumie Vyuo Vikuu vya Nje kufanya tafiti wakati SUZA tunayo hapa, na ni chuo kizuri na Wazanzibari wapo ambao wanaweza kufanya kazi hiyo.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningemshauri Mhe. Waziri ni suala zima kuhusu kifungu cha 6(2) cha Sheria hii kinasema kwamba, "mtu hatoweza kuteuliwa kuwa mwenyekiti isipokuwa awe angalau na shahada ya kwanza ya kilimo au masomo ya sayansi kutoka kwenye chuo kinachotambulikana na awe na uzoefu wa kazi usiopungua miaka mitano".

Mimi nashauri kwa hapa siyo tu mwenyekiti, lakini hata wajumbe. Napendekeza isomeke kwamba mtu hatoweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti na Mjumbe. Baraza hili la Taasisi ni lazima liwe na wataalamu. Ningeshauri kabisa tuache haya mazoea ya kuteua wajumbe wa Baraza kwa mazoea. Tumekuwa na wajumbe wa Baraza kwa mazoea. Tumekuwa na wajumbe wa Baraza ambao uwezo wao mdogo. Baraza hili ndilo ambalo litatoa muongozo kwa sekretarieti chini ya Mkurugenzi na watafiti. Kama Baraza halina uwezo litakuwa haliwezi kuwashauri vyema watendaji kwenye taasisi hii ya utafiti.

Kwa hivyo mimi napendekeza kwamba mwenyekiti na wajumbe wote basi wasipungue elimu ya shahada ya kwanza. Kwa sababu hawa ndio ambao watapanga mikakati, watapanga kazi kwa ule utafiti wetu. Leo kama mimi ukinichagua mjumbe wa Baraza hili nitamshauri vipi mtafiti au mtaalamu kufanya utafiti. Je, mimi kama mimi mfano nitatambuaje matakwa ya kitaalamu ya utafiti ikiwa sina uwezo. Napendekeza kwamba mwenyekiti wa Baraza hili na wajumbe wote wawe na elimu ambayo ya shahada angalau ya kwanza ili lugha yao iende sambamba na lugha ya utafiti.

Mhe. Spika, jengine ambalo napendekeza ni kifungu cha 7(1) (a) – (g) kazi za Baraza. Ukiangalia hizo kazi na kifungu cha 11 na 12 ni kazi za kitaalamu ambazo zitakuwa chini ya Baraza. Kwa hivyo najenga hoja kwamba Baraza lazima liwe na nguvu, liwe na watu wenye uwezo ili hizi kazi za kitaalamu waweze kuzisimamia ipasavyo, vyenginevyo Mhe. Spika, tukiacha sheria hivi hivi tukiteua Baraza ambalo halina uwezo, lugha ya wataalamu haitoeleweka na dhana nzima ya sheria hii itakuwa haina msaada.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningelishauri kwenye suala hili kuna suala zima la maana ya kilimo. Kilimo kwenye Sheria hii imejumuisha kilimo yenyewe, ufugaji, uvuvi na mazingira. Tumekuwa na mazoea hapa Zanzibar kwamba kila tafiti tunazofanya tumezoea kufanya tafiti za kilimo cha chini, kwa maana ya mabondeni kwa maana ya mpunga. Wananchi wetu wameshindwa kupata msaada wa kitaalamu kuhusu mazao ya juu hasa katika ukanda wa mashariki wa Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, lazima serikali itambue kwamba wakulima wa nchi hii sehemu kubwa wako vijijini, tena katika mashariki ya Unguja na Pemba, kwa hivyo hao ndio wanahitaji utafiti, wanahitaji maelekezo, wanahitaji kila msaada wa wataalamu kwa ajili ya kufikia kilimo ambacho kitaleta tija. Mimi napendekeza kwamba Mhe. Waziri sheria hii wazingatie sana wakulima wetu wa Mashariki ya Unguja na Pemba, ambayo ndio hasa wakulima wanaoleta bidhaa sokoni ndio wakulima wanaongeza pato la taifa kupitia kilimo, ndio wakulima wanaopunguza njaa kupitia kilimo. Vyenginevyo kuna sheria ambayo itawalenga tu watu wanaolima mpunga kwa nadharia ya nerika ambayo hatuioni faida yake nadhani itakuwa hatujafanya la maana.

Mhe. Spika, jengine ambalo ningelizungumza hapa ni suala zima la ufugaji wa samaki. Mimi nataka nimpongeze sana Mhe. Said Ali Mbarouk, Waziri aliyetoka Wizara ya Uvuvi kwa kufanya kazi ya ziada ya kuwashajihisha wananchi Zanzibar nzima kwa ajii ya ufugaji wa samaki.

Mhe. Said kwa kweli mimi alipoondoka katika Wizara hii nimepata mshtuko, kwa sababu kadiri utakavyoangalia Unguja na Pemba wavuvi aliwafikia na walimuelewa. Hivi sasa samaki wa kufugwa wameongezeka. Wasi wasi wangu kwamba kazi nzuri hii sijui kama itaendelezwa, Mwenyezi Mungu amjaalie huyo waziri aliyekuwepo aendeleze ili wafugaji wetu waweze kupata matunda haya.
Mhe. Said Ali Mbarouk amediriki kuwachukua Wazanzibari zaidi ya 12 kuwapeleka China kwa ajili ya kupata taaluma ya ufugaji wa samaki. Sheria hii pamoja na waziri aliyekuwepo ni lazima asimamie matunda yale, kwa ajili ya ufanisi wa ufugaji samaki Unguja na Pemba.

Nataka nimwambie Mhe.Waziri kwamba kama kuna eneo ambalo samaki wangefugika kwa maana ya kuwepo mabwawa ya kisasa, mabwawa ya kimaumbile ambayo hayakauki ni eneo la Muwambe, ningemuomba sana Mhe. Waziri, pengine baada ya sheria hii, akaja akajifunza akaona jinsi Mwenyezi Mungu alivyojaalia mabwawa kule ya kimaumbile ambayo hayakauki ili huo utafiti ukianza, basi ile taaluma ya ufugaji samaki itaweza kupatikana.

Mhe. Said Ali Mbarouk alipokuwa Waziri wa Uvuvi alikuwa tayari ameahidi kwamba kituo cha utafiti wa uvuvi kitajengwa kule jimbo la Kiwani hasa sehemu ya Muwambe. Kauli iliyotolewa na Mhe.Waziri, naye ni Waziri wa Serikali hii, basi kauli ile iendelezwe ili watu wapate kujenga kituo kile na kupata kujifunza.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo ningelizungumza haraka haraka ni yote haya yanahitaji fedha. Mimi nina wasi wasi kwamba sheria hii imeandikwa vizuri lakini kwa tabia yetu ya kudharau mambo, kutegemea wafadhili, dhana ya sheria hiyo ya utafiti itashindwa kutekelezwa.

Nimuombe sana Waziri wa Fedha kwamba asidhani kwamba utafiti unahitaji *ceiling*, utakapoweka *ceiling* ya utafiti basi ni kama mbingu na ardhi. Utafiti unahitaji fedha, kwa hivyo asidhani kwamba tunapitisha sheria hiyo ya utafiti baadae amwambie Mhe. Waziri basi njoo na *ceiling* yako. Utafiti hautegemei *ceiling* ya Wizara ya Fedha, bali unategemea fedha nyingi kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

Mhe. Spika, kama tunapitisha sheria kwa ajili ya utafiti wa kweli, basi ni lazima serikali ikubali kuwekeza fedha kwenye suala zima la utafiti, vyenginevyo tukitegemea wahisani, tukitegemea kuomba, basi dhana hiyo ya sheria hii itakuwa haina faida na kwa kweli Wazanzibari watatushangaa sana kuandaa sheria nzuri lakini haina faida kwao.

Mhe. Spika, mwisho kabisa niseme tu kwamba naomba sana Mhe.Waziri kwa busara zake akubali kwamba wajumbe wa Baraza zima, mjumbe mmoja awe ni kutoka Chuo Kikuu cha SUZA, ili na sisi Wazanzibari tupate matunda ya wataalamu wetu kutoka SUZA. Baada ya hayo akinikubalia nitaunga mkono Mswada huu mia kwa mia. Ahsante.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii ya kuchangia machache kuhusu uundwaji wa Taasisi ya Utafiti ya Kilimo.Awali ya yote Mhe. Spika, naomba unipe ruhusa nimshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma aliyetujaalia kufika hapa leo na kuwa na uwezo wa kuweza kuchangia maendeleo ya taifa letu.

Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nichukue fursa hii kuipongeza Wizara ya Kilimo kwa juhudi yao na upeo wao wa kuweza kuona kwamba, taasisi ya utafiti wa kilimo unahitajika sana hapa Zanzibar. Naamini kwamba tumeshakuwa na wasomi wengi sana ambao sasa wanaanza kuona umuhimu wa mambo mbali mbali ambayo wenzetu wameyatumia katika kuleta maendeleo ya taifa lao. Mimi niwapongeze Wizara pamoja na wataalamu wote ambao walikaa pamoja na wakaona umuhimu wa kuwa na taasisi hii.

Mhe. Spika, sote tunajua kwamba suala la kilimo limekuwa likitiliwa mkazo sana katika serikali yetu, na kilimo kimekuwa kinapewa maneno mengi sana, aidha “Kilimo ni uti wa mgongo”, “Kilimo ni uhai”, “Mapinduzi ya Kilimo”, “Kilimo kwanza”. Haya yote yanatokana na kutaka kuweka kilimo ni sekta ambayo ni muhimu katika nchi yetu. Kilimo hiki tumekuwa tukikitumia sisi hasa kwa kupatia chakula, lakini vile vile kilimo kimekuwa kikitumika kama ni nyenzo moja ya kutupatia fedha ambazo zinatusaidia katika kuendesha maisha yetu.

Kilimo chetu kimekuwa duni siku nyingi na kwa miaka mingi. Wazee wetu walikuwa wanalima kwa ajili ya kujikimu wao wenyewe na kufanya biashara ndogo ndogo.Sasa hivi dunia hiyo imepita, dunia iliyokuwepo sasa hivi kilimo kinaweza kukuletea manufaa au mafanikio katika nchi, hasa kwa kuweza kufanya kilimo kuwa ni kilimo cha biashara. Ikiwa kama tutafanya utafiti ulio mzuri na utafiti ambao utakuwa umeelekea katika kuleta tija ya kilimo basi kilimo kitatusaidia Zanzibar. Ardhi tunayo nzuri sana, Mhe. Asha Bakari alisema ukitia kijiti tu kinaota, ni kweli na hata yale maeneo ambayo yana mawe.

Mimi wakati nilipokuwa ZAYADESA tulikwenda kulima shamba la Tunguu ambalo linatusaidia katika kuwaelimisha vijana mbali mbali.Pale Tunguu mawe ni mengi sana, lakini kitu cha kushangaza kuna sehemu ya eneo la Tunguu tuliyaondoa mawe na ardhi tuliyoikuta chini udongo wake ni wa aina ya peke yake, unachokipanda kinaota.Haya mambo yanataka utafiti.

Hawa watakaohusika na taasisi hii wahakikishe kwamba wanafanya utafiti wa kina wa kujua ardhi za aina mbali mbali tulizokuwanazo hapa Zanzibar. Tuna ardhi nzuri sana na hata ardhi ya kichanga.Huu mchanga ambao tunasema sisi hauoteshi unaotesha. Mimi nilibahatika kwenda kusoma Israil nimekuta mpaka kwenye mchanga, kwa sababu wenzetu wao ni Jangwa.Kitu cha kushangaza ndizi zinaoteshwa kule za biashara zinapelekwa Europe, machungwa wanaotesha.

Nikasema kwa nini sisi tunao udongo mzuri lakini wao wanalima zaidi na wanafanya kilimo cha biashara kuliko sisi, wakati sisi tunao udongo mzuri. Lakini wao wamefanikiwa kutokana na utafiti ambao wameweza kuufanya na wameweza kujua ni kitu gani ambacho kinaweza kustawi kwao na ni kitu gani ambacho kinaweza kustawisha mazao katika maeneo hayo. Mimi nafikiria utafiti utakuwa ni kitu muhimu sana hasa katika kilimo.

Pili nilikuwa naomba kusema kwamba Zanzibar tumekuwa tuna mazao mengi sana hasa kwenye masuala ya mboga.Nasikitishwa sana mimi kila siku nalisema hili suala, wenzetu Kenya tayari

wameshaanza mradi maalum unaohusiana na kujaribu kuzipa kipaumbele mboga za kienyeji. Zile mboga zinasaidia sana katika lishe ya jamii.Zile mboga ndizo zilizowalea wazee wetu. Mimi naomba taasisi hii tuna aina ya mboga kwa Zanzibar zinafika 100 au mia mbili za zamani zilizokuwa zinatumiwa Zanzibar.

Leo hii tumebakia na mboga ambazo tumeletewa ngeni, mchicha sijui na nini, mboga nyengine hazitumiki. Lakini zile zote zinasaidia katika lishe.Leo hii watoto wetu wanakuwa na tatizo la utapia mlo kwa sababu hawajui zile lishe lakini mboga, ardhi zetu zinaweza kutoa aina mbali mbali, hebu tufanyeni utafiti, tuzitumie hizi mboga lakini sio tu kwa ajili ya kula sisi wenyewe, tuzifanye mboga ambazo tutaweza kuziuza nje.

Tuzitangaze katika masoko mbali mbali ya nje. Mimi naamini tukifanya utafiti tutaweza kuzijua *components* ambazo zimo ndani ya zile mboga, na tunaweza kuziuza nje lakini huu unatakiwa utafiti mkubwa. Mhe.Waziri tunaomba kwa hili hebu tutafutia sasa hivi miradi ambayo itashughulika na uzalishaji wa mboga mboga za asili hapa Zanzibar.

Mhe.Spika, mimi sitaki kuchukua muda wako mkubwa wa kuzungumza lakini tu nimefurahishwa sana na nasema hili suala la utafiti ni suala muhimu.Tumekosea pale zamani tulikuwa tunatafuta miti tu tunapanda, tunasema nchi fulani wanapanda na sisi tupande, kumbe ardhi yetu iko tofauti na wao, matokeo yake hakuna kilichotokea, ardhi tumeitumia vibaya.Makosa tumeshafanya sasa tujirekebishe.

Mhe.Spika, jengine ni kwamba ardhi yetu tunaitumia vibaya, na sisi chakula tunakihitaji na si kwa kula tu, tumesema hata kwa biashara. Sasa hivi siwalaumu wale watu ambao wanatumia yale maeneo ya kilimo kwenda kujenga.Kwa sababu hata na mimi nimefanya hivyo hivyo, lakini kwa sababu hakuna ardhi ya kujenga, hupati, kama hupati utakwenda kule kule kwa wazee wako ukajenge.Kwa sababu kule ndiko unakopata, utapewa pa kujenga lakini huku kwengine hupati ukiwa mnyonge.

Mimi nafikiria serikali sasa hivi ikae ijipange ipange maeneo, wengi wamesema tupange maeneo ya kilimo, tusiwaachie watu kule wakajenga yawe ni maeneo ya kilimo.Na huku kwengine ambako tunajua ni maeneo ya mawe watu wajenge.Lakini ikiwa tutakuwa tunakwenda hatuna mipango, matokeo yake tunaharibu maliasili zetu.

Mhe.Spika, katika hii sheria nimegundua kuna sehemu inasema katika ukurasa wa 20 kifungu cha 8 ambacho hapa kinazungumzia “Baraza litakuwa na katibu ambaye atakuwa mwanasheria wa taasisi, atakayefanya kazi zifuatazo”. Nikizitizama hizi kazi ambazo anatakiwa huyu Katibu azifanye, sioni kama hizi ni kazi za mwanasheria.

Hizi kazi ni za mtu ambaye ana sifa ya utawala. Mwanasheria kwa nini tunamuweka hapa au huyu tunae katika ofisi halafu tunataka kumuongezea kazi za utawala. Kama ni hivyo kama tunataka kumtumia huyu kwa kazi za utawala hivyo ni sawa, lakini ikiwa kama ni huyu tunampa kazi hii, hizi si kazi za Mwanasheria.

Naomba Waziri akija anifahamishe kwa nini hizi tunampa huyu, *unless* ikiwa huyu ni mwanasheria ana sifa nyengine, kwa sababu hapa kama atatafutwa mtu mpya mwanasheria ina

maana hapa huyu mwanasheria tunamuondoa katika *field* yake tunampeleke katika mambo mengine. Lakini ikiwa yupo tayari anawekwa anapewa kazi nyengine za nyongeza, basi hapo nitakubaliana na mapendekezo hayo.

Mhe. Spika, mimi nafikiri sitokuwa na mengi ya kusema zaidi ya hayo, lakini nasema kuwa ninaunga mkono huu Mswada 100 chini ya 100, na nawaombea kheri wale wote ambao watakuwa katika taasisi hii wafanye kazi kwa imani na kwa moyo, ili waweze kulijenga taifa letu ili waweze kutuletea mafanikio na maendeleo katika taifa letu. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante sana Mhe. Spika kwa kunipa fursa hii na mimi kuongeza machache katika Mswada huu ambao umewasilishwa kwetu.Kwanza nimshukuru Mhe.Waziri ambaye amewasilisha kwetu Mswada huu.Vile vile nisiwe mchache wa fadhila nimshukuru aliyetayarisha Mhe. Mansour Yussuf Himid, kwa hivyo na yeye nampongeza sana kwa kutayarisha Mswada huu na kuuleta kwetu.

Mhe. Spika, Mswada huu ni mzuri sana, na kwa sababu ulenga kwenye utafiti ambao wenzangu tokea asubuhi wamezungumza mambo mbali mbali kuhusu Mswada huu. Kwa hivyo na mimi nitasema machache ili nione nimeitumia ile fursa ambayo imenileta katika Baraza lako hili tukufu.

Mhe.Spika, kila siku zikienda mambo yanaongezeka na teknolojia inaongezeka. Kwenye suala hili la utafiti ni vizuri tukafanya utafiti wa kina kama walivyosema wenzangu kwamba, tufanye utafiti wa ardhi yenyewe tuweze kujua ni mazao gani yanamea kwenye ardhi ile. Si vizuri tukatumia fedha chungu nzima kwa kufanya tafiti mbali mbali, lakini *efficiency* inakuwa ni ndogo. Nimeona mimi mwenyewe kwamba serikali imetumia fedha karibuni bilioni moja kwa kupanda mboga mboga. Kuna ushirikiano wa Zanzibar pamoja na Misri. Lakini mpaka sasa hivi imetumika bilioni moja lakini bado mafanikio yake ni madogo. Hii ni kuonesha kwamba serikali inatumia fedha nyingi lakini ufanikishaji unakuwa mdogo.

Mhe. Spika, mimi ningesema bora tufanye miradi kidogo lakini iwe na mafanikio, kuliko kuwa na mambo mengi ambayo tunakuwa tunayaanzisha lakini yanakuwa si endelevu. Mimi ningeomba sana serikali sasa hivi tuelekeze nguvu zetu pahala pamoja.Kuna miradi imeshaanzishwa siku nyingi lakini faida zake hazionekani. Bilioni moja ile iliyotumika kwa mboga mboga wangesaidiwa wananchi wale wakulima wangefaidika kwa kiasi fulani.

Mhe. Spika, kuna wakulima wengi kama walivyosema wenzangu, kuna mabonde mengi kama Cheju na maeneo mengine. Ukienda sehemu za Pemba kuna maeneo mengi, lakini mazao hayapatikani, yanapopatikana unakuta hapana ufanisi, mazao yanakuja mara moja na yanaondoka mara moja. Au pengine mazao yanakuwa mengi katika msimu, lakini hatuna vya kuyafanya kwa sababu hatuna viwanda. Viwanda tulivyokuwa navyo kama wenzangu walivyosema asubuhi kulikuwa kuna viwanda vya maziwa, tulikuwa tunazalisha siagi hapa na ilikuwa ni nzuri, baadae vitu vinapotea.

Tokea juzi kuna masuala mbali mbali yamezungumzwa hapa, tunaanzisha vitu vizuri lakini baadae kuviendeleza tunashindwa.Tulikuwa tuna kiwanja cha watoto pale kizuri lakini kimekufa kabisa, pembea za watoto zilikufa na zikaoza kabisa. Sasa hivi tufanye kazi upya “Watu

wanasema kwamba tusipoziba ufa tutajenga ukuta." Kila siku baada ya kwenda mbele tunarudi nyuma. Mambo kama yale ni lazima tuyaangalie, tukianzisha jambo ni lazima baadae liwe endelevu.

Juzi tumekwenda na wageni wetu wale Wazee Arusha Club. Tumekwenda, lakini ukienda pale wewe mwenyewe unasikitika, sisi hatujaweka pale kwamba pawe ni sehemu ya utalii. Tuseme watu wa mazingira wangekwenda wakaona ni namna gani pale tutapata ufanisi. Kwa sababu pale tunapata *revenue* lakini ukienda kama pahala pametupwa. Tumekwenda na wageni pametupwa kabisa, angalau pale ingewasaidia wananchi wakawaelimishwa. Pale kuna miradi chungu nzima. Pale zimepatikana pesa za MACEMP, lakini kunakuwa hakuna uwajibikaji kwa zile taasisi zenyewe.Tunakuwa kila siku tupo nyuma tu, hatuna ufanikishaji. Nchi yetu ni ndogo kama ingelikuwa tupo *serious* basi tungelipata mafanikio mazuri, lakini hatupo *serious*.

Tunapewa miradi chungu nzima na wenzetu nje, lakini tunajikuta kila siku tupo nyuma. Pale panasikitisha sana kwani pale tunaweza hata kuwasaidia wananchi wetu ajira. Unapokwenda na wageni wewe mwenyewe unajihisi vibaya. Kwa hivyo haya ni mambo ya kukaa zile wizara husika, mazingira, wizara ya fedha hizi ndizo wizara mama, zibuni mambo ambayo tutakuwa tunakwenda nayo kwa uzuri na yatatuletea ufanisi.

Mhe. Spika, hili jambo linasemwa sana na wasanii wanalisema na hapa niko *serious*.Tunaambiwa mdudu ndani ya kokwa ya embe kaingiaje? Mheshimiwa ana watafiti chungu nzima atwambie hili suala la huyu mdudu kwenye kokwa kaingia kaanza kwenye ua, kaanza wapi na yeye anao wataalamu chungu nzima. Hili sio kwenye utani, maana wasanii watakuwa wana maana yao lakini mimi hapa nataka kujua huyu mdudu kwenye kokwa ya embe kaingiaje? Akija hapa kama kweli anao watafiti atwambie alianzia wapi.

Mhe. Spika, nije upande wa taasisi inasema kwamba itaweka vitabu vyake vya hesabu. Kwa sababu na mimi fani yangu ni mtu wa hesabu ni lazima viwepo vitabu vya hesabu na hasa *fixed asset register* ambayo kila tunapopita tunaona ni matatizo, serikali haijui mali zake. Kwa kweli hili ni tatizo kwa hivyo ni lazima hizi *assets* ziwepo na kitabu maalumu ambacho kinawekwa.

Mhe. Spika, kuna kifungu kinasema bila ya kujali masharti ya kijifungu cha kwanza kwenye ufanyaji wa utafiti wa taasisi kuanzia kifungu cha 14(1) "mtu yeyote anayefanya au atakayetaka kufanya utafiti wa kilimo Zanzibar atalazimika kwa gharama zake kutoa taarifa kwa taasisi inayohusiana na utafiti wao, na atalazimika kupeleka nakala ya utafiti kwa taasisi".

Hapa sina tatizo na kifungu hichi kwa sababu bila ya kufanya utafiti na kukawa na taasisi ambayo inahusika, ni mambo ambayo yatakuwa hayakupangika, na mwisho wa siku itakuwa hatujui nini tunakifanya. Hili ni suala la kulitilia maanani na kulihamasisha.

Nimeona kuanzishwa kwa uwezo wa taasisi. Mhe. Spika, kuna kifungu cha 5 kina namba 1(a) mpaka (m) lakini niende kwenye kifungu kinachosema "kufanya utafiti na kutumia utafiti wa kilimo kwenye mazao, mazingira, mifugo, misitu, uvuvi, ardhi, maji, wadudu, maradhi na aina zote zinazohusiana na mambo hayo" Ni kweli kuna vidudu vinaingia kwenye embe, mapera hapa ni lazima ufanywe utafiti na wajuulikane wadudu hawa wanatokana na nini. Mhe. Spika, pia

bahari ni sehemu ya kilimo vile vile kuna mambo mengi ambayo yanaingia kule baharini hivyo ni lazima tufanye utafiti tujue ni tatizo gani linaloleta usumbufu ndani ya maeneo yale.

Mhe. Spika, vile vile kuna kifungu cha (b) kinasema kufanya na kutumia utafiti wa kilimo utakaozidisha uzalishaji wa kutumia usimamizi wa kisayansi katika mazao, mazingira, wanyama, misitu, uvuvi, ardhi, maji na kuendeleza teknolojia inayofaa ikijumuisha aina mpya ya udhibiti wa wadudu wa maradhi.

Mhe. Spika, pia nataka niipongeze hii taasisi kwa kufanya utafiti wa kuweka sheria hizi ili sasa tuone kwamba ni ukombozi na ni wajibu wetu kufanya hizo kazi kiudhati wa roho zetu ili tupate mafanikio, isiwe kwamba mtu hawajibiki ila tufuate ile ile misingi kama inavyosema tuwe wawajibikaji, tuwe na uwazi ndani yake kwani Mwenyezi Mungu unapokuwa muwazi na ukawa muajibikaji basi Mungu anakuongozea njia. Kwa hivyo, mimi nasema naunga mkono hoja hii na niwapongeze sana watendaji ambao wameleta sheria hii wakaumiza vichwa wakaona watuletee mswada huu. Kwa hivyo, ningewaomba wawakilishi wenzangu tuupitishe mswada huu mia juu ya mia.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Allah Subhana Wataala na kumtakia rehma Mtume wetu Muhammad (S.A.W). Pia nitoe shukurani zangu za dhati kwako jioni hii na mimi nikapata nafasi ya kutoa mawazo yangu katika mswada huu wa sheria uliopo mbele yetu.

Mhe. Spika, kwa kweli tukiuangalia huu mswada tutaona kwamba toka kupata uhuru Zanzibar mwaka 1964 hadi leo hii ndio tunaanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na mambo mbali mbali, tutaona kama tumechelewa. Lakini niseme kwamba mambo hayo ya utafiti yalikuwa yapo, lakini yalikuwa bado hayajapewa nguvu lakini nitoe shukurani zangu za dhati kwa serikali kuona kwamba kuna umuhimu kuwa na chombo hiki kinachoweza kujigemea. Kwa hivyo, sina budi kuipongeza serikali kwa hilo.

Mhe. Spika, kuwa na chombo cha utafiti ningaliiomba sana serikali isiweke chombo bila ya kuwawekea maeneo ya shughuli zao za utafiti, kwa sababu nahisi kwamba hadi muda huu tulionao ndugu zetu wa utafiti hawana ofisi ambayo inashughulikia hasa kama ofisi hii ni ya utafiti Zanzibar bado wamepachikwa katika Wizara ya Kilimo. Kwa hivyo, kwanza niitake serikali wawajengee hawa utafiti ofisi yao maalum ili iweze kutosheleza katika masuala yote ya utafiti hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, tatizo hili la kuwaenzi hawa watafiti ndio ilipofikia kwamba watafiti wetu wengi huihama nchi na kuhamia katika maeneo mengine. Tukiangalia kuna mtaalamu mmoja Dk. Kassim Omar na wengine walikuwa ni watafiti wazuri na wataalamu wakubwa hasa sehemu za mifugo, lakini wengi wametutoka katika nchi yetu. Kwa hivyo, kutokwa na watu kama hawa kwa kweli ni kurudi nyuma kimaendeleo ya nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Spika, nikianza kutoa mchangio wangu nataka nianze katika kifungu cha 5 kazi na uwezo wa taasisi. Mhe. Spika, hii inasema kufanya utafiti na kutumia utafiti wa kilimo kwenye mazao, mazingira, mifugo, misitu, uvuvi, ardhi, maji, wadudu, maradhi na aina zote zinazohusiana na mambo hayo na mfumo wa viumbe na mazingira. Mhe. Spika, hapa pamewekwa mambo mengi

sana na tukisema tulichambue moja moja, basi muda pia utakuwa hauturuhusu. Lakini niseme kwamba suala zima la mazingira kwanza tuhakikishe watafiti wetu yale mazingira yao ya kazi yamekuwa tumeyaboresha, tutakapowaweka katika mazingira mazuri naamini kwamba shughuli zao za utafiti zitakuwa zinakwenda vizuri. Lakini kama mazingira yao yatakuwa ni mabovu, basi itakuwa tumewanyima na watakuwa hawana uwezo wa kufanya kazi.

Mhe. Spika, lakini tukitoka katika mazingira hayo pia tuwe na mazingira yakuwafanyia kwamba safari zao za kwenda kwa walengwa kama kwenda kwa wakulima, basi wawe wanakwenda kwa uharaka. Lakini inawezekana pengine watafiti wote hawa tulionao wana gari moja, hii kazi itakwenda vipi Mhe. Spika? Hivyo itakuwa hatujafika katika malengo yaliyokusudiwa. Kwa hivyo, ningeliishauri sana serikali kwamba wawezeshe watafiti wetu, wawe na nyumba nzuri, wawe na magari ya kutosha ili kufuatilia kule ambako tumekulenga kuunyanyua uchumi wa nchi.

Mhe. Spika, tukija katika misitu tukiangalia sasa hivi Zanzibar misitu yetu mingi inapotea. Kwanza kwa kutumia kuni kwa ajili ya kupikia, miti kwa kujengea na mambo mengine mbali mbali. Kama watafiti wetu watakuja vijijini maeneo ambayo yana misitu wakato taaluma basi kuna uwezekano wa wananchi kuweza kuwafahamu, na wananchi wakapata mbinu mbadala ili kuinusuru misitu na ili kuifanya nchi yetu iwe inapata mvua za mara kwa mara na kuweza kurudi rutba katika ardhi tuliyonayo ili wananchi wakaweza kupata kilimo na mbolea mbali mbali.

Mhe. Spika, kuhusu suala zima la uvuvi tukiangalia Zanzibar kwamba ni visiwa na visiwa vyetu vimezingirwa na bahari, Mashariki, Magharibi, Kusini na Kaskazini. Kwa hivyo, tunasema kwamba njia moja ya maisha ya wananchi wetu wa Zanzibar wengi wanatumia bahari, na uvuvi unaovuliwa haukukidhi maisha ya wananchi wetu. Kutokana na kwamba serikali imeona umuhimu wa bahari wana mpango wa kuwawezesha wananchi wetu kufikia bahari kuu kuvua, lakini Mhe. Spika, mimi bado naona hii ni ndoto hatutofikia.

Mhe. Spika, wavuvi wetu wote wanaovua wanavua vile walivyorithi kwa wazazi wao, hakuna taaluma yoyote. Kwa hivyo, ningeliishauri serikali kwa hatua tuliyofikia sasa ni vyema tukaanzisha mpango wa kuwafundisha wanafunzi namna gani ya kuweza kuvua na kufikia katika bahari ambazo wataweza kukidhi maisha yao.

Lakini pia tutakuja sema hapa, itakuja sera ya uvuvi waje wafaidike watu wa nchi nyengine Wazanzibari wabaki kuambiwa kwamba Wazanzibari hawataki kazi, haliyakuwa inayokosekana ni taaaluma. Kwa hivyo, wakati tunatayarisha haya basi tusitayarishe na tuwatayarishe na vijana wetu kwa kutoa elimu ili litakapofanikisha hili iwe tayari Wazanzibari wana taaluma yakuweza kufikia katika bahari kuu.

Mhe. Spika, suala zima la maji, maji ni uhai na kitu chochote hakiwezi kuishi bila ya maji, lakini tumesikia hapa juzi Wizara ya Ardhi ilisema kwamba maji mpaka huko duniani hayapatikani. Kwa hivyo, inasemekana kwamba Zanzibar ina maji mengi yakuweza kutosheleza mambo mbali mbali hapa nchini kwetu. Lakini kutokana na miundombinu ambayo ni mibovu imekuwa ni tatizo hakuna maji kila mmoja analilia maji.

Kwa hivyo, ili tufikie chombo hiki cha utafiti ni vyema kikawezeshwa tukaondosha tatizo hili ili wananchi wetu waweze kupata maji ili kuweza kujenga afya zao na hali zao. Kwa hivyo, ningelishauri sana serikali unapoweka taasisi hii ya utafiti unajua kwamba itakuwa inafanya tafiti sehemu mbali mbali, maeneo kwa maeneo, hivyo ili wafikie ni kuhakikisha kwamba tumewawezesha.

Mhe. Spika, nikiendelea kifungu cha (f) kinasema kwamba kuanzisha vituo maalum vya utafiti, vituo vidogo maeneo ya miradi na mashamba kwenye maeneo tofauti ya mahusiano ya viumbe na mazingira ya nchi yakufanyiwa utafiti kwenye maeneo ya kilimo yenye matatizo.

Mhe. Spika, hili ni kweli wananchi wetu wengi hawana taaluma yakutayarisha mashamba yao kwa ajili ya kilimo, mkulima wa vijijini anapotaarisha shamba yake kama hajachoma moto magugu anaona mwaka huu yeye havuni. Kwa hivyo, kama tutakitumia kweli hiki chombo tunachotaka kukiweka kwanza kuwataalamisha hawa wananchi ambao wanapotayarisha mashamba mpaka wapige moto tukawataka sasa wasitumie tena moto watumie mbinu nyengine mbadala, basi naamini kwamba tunaweza tukauhisha viumbe vyengine tunavyoviona kwa macho na vile tusivyoviona.

Mhe. Spika, kwa sababu mashamba mengi yana wadudu mbali mbali wenye kuruka na wale ambao wanatambaa, na wadudu wale husababisha ardhi ile kupata rutba, lakini mkulima anawapiga moto. Kwa kweli hili ni tatizo kwa hivyo kama tutawatumia ipasavyo watafiti wetu na kuwawezesha kufika katika maeneo ya wakulima, basi upo uwezekano wa wananchi wetu kupata tija zaidi kuliko hiki kilimo walichokizoea cha kijembe kongoroka.

Mhe. Spika, nikiendelea katika kifungu (h) kinasema kwamba kutayarisha semina, midahalo na warsha kwenye maeneo yenye matatizo ambayo yanahitaji wataalamu kutokana kwenye taasisi mbali mbali za utafiti na kutoa fursa na kubadilishana mawazo na kujipatia maendeleo ya kisiasa katika kilimo.

Mhe. Spika, hapa pana tatizo kubwa, mara nyingi tunaweka sheria kama hizi lakini utekelezaji unakuwa haupo, na hili linakuwa ni tatizo. Kwa nini? Kwa sababu wananchi wetu wengi taaluma hawana, lakini sisi tumeshasema kwamba wapewe semina, lakini tatizo la semina watu wengi wanaangalia semina ni nini, hanaangalia semina ni kupata lile posho.

Kwa hivyo, hapa watu wanajipanga na nani aende kwenye semina, inawezekana wale walengwa wakulima hata mmoja hayuko katika semina ile, watu wanalokwenda ili apate shilingi kumi au ishirini aweze kuhuisha maisha yake. Kwa hivyo, hapa naomba sana pafanywe utafiti wa kweli je hawa tunaowalenga kwenye semina hii ndio wahusika.

Mhe. Spika, tukiendelea tunasema kwamba tuna Masheha katika shehia lakini hawa masheha wanahitaji kufanyiwa utafiti, watu wanachukuana kifamilia, wanachukuana kiukoo hatima yake elimu inayotoka pale haifiki kwa walengwa. Kwa hivyo, ni vyema tukawa na mabadiliko na kuufanya utafiti kweli tunaowataka ndio wanaoingia katika semina ile na pia hii midahalo ipatikane. Mhe. Spika, wakati tumekiweka hiki chombo basi ni vyema kuhakikisha fursa hizi wananchi zimewafikia na tumeona kweli kumetokea mabadiliko ya wakulima wetu ili kuweza kupata maendeleo katika suala zima la kilimo.

Mhe. Spika, tukiangalia mwaka mzima huu nusu ya mwaka Mhe. Rais amefanya ziara mbali mbali katika kukiendeleza kilimo, ikiwa kilimo cha mikarafuu, kilimo cha mpunga. Lakini tulidhani mwaka huu kwamba serikali kwa vile Rais alivyofanya ziara nyingi katika kuhimiza suala hili na Wizara hii ya Kilimo itajikaza ili kuhakikisha kwamba wananchi wamelima kwa wingi na wamevurugiwa mashamba yao.

Mhe. Spika, jambo la kusikitisha ni kwamba wananchi wengi wamelimiwa jembe la mwanzo, lakini suala la kuvurugiwa mashamba maeneo mengi yamekosekana. Mhe. Spika, inawezekana kwamba vyombo vilizidiwa na kazi au ufuatiliaji ukawa mgumu kwa wananchi na kwa wizara husika. Kwa hivyo, tungeliishauri sana serikali kutayarisha zana za kilimo mapema ili wananchi wetu wapungue ile kuisema sana serikali, kwa sababu hivi sasa maeneo mengi mvua zimeshaanza kunyesha na kunyesha kwa mvua mashamba yale hayalimiki tena, na kukosa kulimika kwa magari haya ya trekta inakuwa ni dhiki kutokana na mvua na vile walivyolima watu wa kilimo wananchi wanashindwa kuendeleza kilimo kile.

Kwa hivo, kama serikali inawahimiza wananchi kulima ili tupunguze ugumu wa maisha tuweze kujitegemea kwa kilimo, basi ni vyema wataalamu wetu hawa wakaanza kuwafikia wakulima na mapema na kuwa karibu na mabwana shamba na mabibi shamba ili kuhakikisha kilimo hiki wananchi wetu wameweza kupata kwa ule wakati uliowekwa. Mhe. Spika, kutokana na muda na kuna wenzangu wengi wanahitaji kuchangia na mimi ni miongoni mwa kamati hii kwa hivyo nakuombeni sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu mshirikiane na sisi ili tuiunge mkono hoja hii ili watafiti wetu waweze kufanya kazi za haraka ili nchi yetu iweze kupata mabadiliko. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, na mimi nashukuru sana kabisa kwa kupata nafasi hii ya kuchangia kidogo katika Mswada huu wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Lakini kwanza Mhe. Spika, kabla sijaanza kuchangia hicho kidogo nilichokusudia niungane na wenzangu kwa kutoa mkono wa pole kwa mwenzetu somo yangu aliyetangulia mbele ya haki Sheikh Salim Amour Mtondoo. Mhe. Spika, huyu mtu tulikuwa jirani ni somo yangu lakini ndio amekwenda mbele ya haki Mwenyezi Mungu amsamehe makosa yake yote na amuweke mahala pema peponi.

Mhe. Spika, la pili sina budi kutoa pongezi zangu za dhati kwa uchaguzi mdogo uliopita na kumpata mtaalamu wetu mpya katika Baraza hili Sheikh Mohammedraza Hasanali Mohammedali. Na mwisho kabisa tena kwa furaha iliyomo moyoni mwangu nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar kwa mabadiliko aliyoyafanya hivi karibuni na kwa makusudi kabisa Mwenyezi Mungu akatujaalia tukampata mheshimiwa mpya katika Wizara hii ya Kilimo, wizara inayogusa uhai wa wananchi Mhe. Suleiman Othman Nyanga na huyu kama tunavyojua Mhe. Spika, ni mtaalamu amepita wizara nyingi na alhamdulilah tunaona namna anavyojibu maswali naamini tutafaidika kwa hali ya juu kabisa.

Baada ya hayo Mhe. Spika, naomba sasa kuchangia katika mswada huu mfupi kwanza kwa kupata ufafanuzi kidogo.

Mhe. Spika, katika mswada huu ukurasa wa 23 kifungu cha 13 (d) ambacho kinahusiana na kamati na kazi itakazozifanya pia imeeleza kuwa kamati itakuwa na kazi ya kufanya kazi nyengine zozote zitakazotolewa na Baraza. Kwa hivyo, hii kazi nyengine zozote naona inafika mbali sana kwa hivyo ningeliomba iwekwe katika hali ambayo hizo kazi nyengine zozote zinazohusiana na yote yaliyomo katika mswada huu. Hilo ni moja.

Mhe. Spika, jengine katika ukurasa huu huu wa 23 kifungu cha 14 (1) kinaeleza hapa kuwa mtu yeyote atafanya au anayetaka kufanya utafiti wa kilimo Zanzibar atalazimika kwa gharama zake kutoa taarifa kwa taasisi inayohusika na kuendelea. Mhe. Spika, wakati mwengine tunajua kwamba tunaweza tukatokewa na matatizo ya maradhi hapa yawe ya miti, yawe ya wanyama na kadhalika, na pengine uwezo sisi wenyewe hatuna na tunahitaji wataalamu kutoka nje ili kuja kusaidia katika utafiti wa yale matatizo ambayo hatujayajua ni matatizo gani.

Kwa hivyo, tukisema kuwa watafanya kazi kwa kutumia gharama zake mimi hapa sikufahamu vizuri kwa hiyo naomba nielekezwe zaidi, tukitilia maanani yametokea matatizo mengi hapa. Kulitokea matatizo ya nzi wa embe na tulipata tabu kubwa sana mpaka kukatokea mitego kidogo ndio haijambo, tulipata maradhi ya migomba yaliuwa migomba muda mrefu sana mpaka tukaona majani tuyapige moto na migomba wenyewe sijui kama ndio udawa au si kweli.

Kwa hivyo, mimi nahisi kwa vile mambo yako juu ya uwezo wetu pamoja na taaluma tuliyonayo tunapohitaji wasaidizi kutoka nje kutufanyia utafiti kwa sababu huwezi kutibu kitu bila ya kukijua kilivyo kwa kufanya utafiti, tusiseme kuwa wajigharamie wenyewe lakini ama tuombe kwa njia ya ufadhili au ikiwa kuna msaada wa aina yoyote tuwape ili kuweza kuokoa janga ambalo Mwenyezi Mungu asijaalie ikatokezea hivyo.
Mhe. Spika, tukija katika ukurasa wa 22 kifungu cha 9 (2b) na kifungu cha 11 (1) kwa hao wataalamu pamoja na uwezo wao wa kitaaluma lakini wametakiwa katika vifungu hivi tofauti kila mmoja awe na uzoefu usiopungua miaka 10. Nahisi Mhe. Spika, miaka 10 ni miaka mingi sana na utaalamu pamoja na kuwa uzoefu unasaidia, lakini na utaalamu ni kitu cha kupewa kipaumbele.

Mimi ningelihisi tungelifanya kama tulivyofanya katika miswada mengine kiasi kipindi cha mitano, miaka sita na kadhalika tusiweke miaka hii ikaja ikasababisha tukakosa wataalamu na tunaanzisha suala hili kwa madhumuni ya kuwa tuepukane na mashaka tuliyonayo.

Mhe. Spika, la mwisho ambalo nikitaka ufafanuzi ni kuwa tunazo wizara hizi, ambazo wizara hizi kwa makusudi zimejumuisha hizo wizara zinazohusika katika kilimo. Wizara zilizopo ni 9 na kila moja inajionesha wazi wazi ukija Wizara ya Uvuvi, Mifugo, Mazingira, Maji, Fedha na kadhalika. Lakini isipokuwa hii wizara yenye dhamana ya Tawala za Mikoa nikitaka kujua katika jumla ya wizara hizi zenye dhamana mbali mbali hii yenye dhamana ya Mikoa ina umuhimu gani wa kuingizwa katika shughuli hii.

Mhe. Spika, jengine katika kuendelea na kuchangia ni kuwa kwanza nashukuru kuwa serikali imeona kuweko na taasisi hii ya utafiti kwa sababu tunapotaka kufanya jambo lolote kama hapajafanywa utafiti wa kina tukajua matatizo yake yakarekebishwa mapema tukaingia tu, basi siku zote tunafeli na suala kama hili la kilimo linalogusa moja kwa moja uhai wa wananchi huwa tunajiingiza katika matatizo.

Mhe. Spika, kwa mfano tumeanza zamani sana tu kufuga ng'ombe wa maziwa na ng'ombe wa nyama tokea kopa ng'ombe ulipe ng'ombe mpaka leo, mpaka hapa kati kati ikawa wanatoka watu kwa makundi kwenda Tanzania Bara iliyokuwa ikiitwa Tanganyika kabla ya Muungano kuchukua ng'ombe na kuwaleta hapa. Tumejitahidi sana kuleta kuku kutoka nchi za nje tena wengi sana na hivi sasa tunaingia kwenye samaki.

Mhe. Spika, kama ingelikuwa kuna utafiti wa kina kabla ya kufanya jambo halafu ndio tukaendelea baada ya kujua kuwa hili linafaa, hili halifai naamini ile dhamira ya serikali yakuwa tujikwamue kiuchumi na tujiondowe katika umasikini ingalikuwa ishapatikana zamani. Lakini kwa sababu yakutokuwa na chombo hiki cha utafiti ikawa sisi tunaangalia tu machoni kuwa mpunga huu miezi mitatu unavuna unaletwa unalimwa ikitimia mwaka mmoja hakuna tena mbegu, ng'ombe huyu ni mkubwa sana tunapata nyama anachukuliwa na ng'ombe wetu wa kienyeji wanazaliwa watoto hawazai tena wanapotea. Na sasa hivi tunawatoa samaki baharini tunawatia katika mashimo wengine wanakufa.
Kwa hivyo, tunafanya kazi nyingi tujikwamue kiuchumi lakini siku zote tunajiongezea umasikini kwa sababu ya kutokuwa na utafiti mwanzo kabla ya kufanya jambo lolote. Kwa hivyo, mimi niipongeze serikali kwa makusudi kwa kuona haja ya kuwepo chombo hiki ambacho kitafanya kazi katika sehemu zote ukizungumza kilimo humu katika mambo chungunzima; ufugaji, ukulima, misitu na kadhalika yote hayo yanamgusa mwananchi. Sasa basi, ili tuendelee Mhe. Spika, ninaloomba suala la utafiti tusilifanye *experiment and error* kwa kuona tu machoni tukaamua ikawa siku zote tunafeli.

Mhe. Spika nitakupa mfano, wenzetu hapa na mpaka sasa hivi *Alhamdulillah* tuna utajiri wa *liquid nitrogen*, lakini zamani ilikuwa tukiagizia kutoka nje kwa gharama kubwa na tukachukua mbegu za ng'ombe waliokuwa wakubwa na wengine wenye maziwa mengi, tukaja tukafanya hapa *selective breeding* kwa kuona kuwa kitakachozaliwa kitazaa tena na hizi sifa mwisho wake tutazifika. Lakini kumbe hatukufanya utafiti kuwa haya mazingira ya hapa Zanzibar yalivyo na hizi mbegu zinakotoka yalivyo, hapo kila mmoja ndio maumbile yake tokea enzi na enzi Mwenyezi Mungu alivyojaalia zinaoana au vipi, na matokeo yake pesa nyingi zimepotea lakini mpaka leo umasikini wa wanyama tunao tunaagizia nyama kutoka Bara.

Mhe. Spika, watu wamefuga kuku wengi tu. Juzi tulikwenda kule Ubago tuliambiwa hao kuku ndio tena wanamalizika, lakini walikuwa wengi sana lakini mfugaji kasema mimi naomba Mwenyezi Mungu wamalizike kwa sababu gani? Hakufanya utafiti, walipokuja hapa hatuna taaluma isipokuwa ya kuwapa chakula lakini mambo mengine hayakushughulikiwa wamekufa, wamekufa mpaka wamebakia kidogo sana. Hii ni hasara kubwa sana tunatumia fedha nyingi halafu tunaambukia patupu.

Mhe. Spika la kusikitisha, na hili ni la kusikitisha kweli kweli, hatufanyi utafiti hata namna watu kuweza kuitumia bahari yao vilivyo. Ilitokea hivi karibuni *MACEMP* ikatoa mashua zikaenea katika majimbo yote tena nyingi sana, lakini nyengine zikapigwa moto, nyengine sheha akazifanya zake na nyengine hazijulikani zilipo hatukufanya utafiti. Sasa naomba tusifanye mambo yetu kwa kushitukia tufanye utafiti wa kina, hayo ni upande wa mazingira.

Lakini pia kuna na utaalamu wa kufanya utafiti wa *genetic make up* wale...hasa wanaohusiana na hawa kimaumbile kweli wanaweza wakaendelea? Ambapo hii kazi ni nzito hii si kazi ya kubahatisha tu, hii ni kazi lazima iwe na pahala maalumu ifanywe hii inafaa hii haifai ndio *selective* maana yake mpaka aa, hawa watatusaidia ndio tuendelee. Vyenginevyo Mhe. Spika, tutatumia pesa nyingi itakuwa tunaingia katika hasara.

Jengine Mhe. Spika, ni mazingira, bila ya kuhuisha mazingira na bila ya kutilia maanani mazingira, lolote tutalolifanya mwisho wake itakuwa ni hasara tu. Kwa sababu mazingira yatakuwa yanachafuliwa na mazingira yatachafuliwa vipi? Uchafuzi wa mazingira unatokana na kazi za binadamu zenye kumletea tija yeye lakini *by product* zinazotoka zinaharibu mazingira. Kwa hivyo, kuna uharibifu wa mazingira katika hewa, katika maji na vile vile kwenye ardhi.

Kwa mfano Mhe. Spika, umasikini na kulazimisha kupata maisha, watu wanalima kama siku hizi lakini mtu anafanya kazi ile iliyo rahisi mtema mkubwa sana kweli kweli anapiga moto tu, watu wa kilimo wapo wanawaachia tu halafu wanasia wanapata mpunga, lakini baada ya mara mbili tatu ile sehemu inakuwa jangwa haioti chochote maji yanakimbia, mbegu haioti kwa sababu ya moto aliyotia na kuua kila kitu, *micro organs* wote walikufa. Kwa hivyo, suala kama hili ili mtu kabla ya kulima kilimo chake ni lazima watu wa mazingira wawe macho wamwambie hapa ukifanya hivi hasara yake inayotokea ni hii kwa hivyo tutaweza kuendelea.

Jengine kuna watu lazima watafute maisha hivi sasa, wanaharibu mazingira lakini hawana njia nyengine na tushukuru Wazanzibari huku hatupigani risasi katika kutafuta maisha kila mtu anakwenda mpaka mwisho wa uhodari wake.Ukiwa na msumeno wa moto unatumia na miti inakatwa ovyo, watu wanafanya kwa kujipatia maisha lakini matokeo yake ni kuwa nchi inageuka jangwa.

Miti inapokufa rutuba katika ardhi inaondoka, mvua inakimbia, joto linakuwa kali, na joto linapokuwa kali sana vile vile vipando haviwezi kumea. Serikali iweze kumudu mazingira haya ya kuweka misitu lakini wakati ule ule na wananchi waelekezwe katika kufanya kilimo bora ili kutokana na kutafuta maisha kwa umasikini kule waweze kufaidika katika kilimo.

Halafu jengine Mhe. Spika, kuna rahisi nyingi hatuzichukui, tuna mambo humu tukichanganyisha tunaweza tukapata mawazo mazuri sana, lakini watu wetu hatuwaelimishi mwisho inasababisha kuharibika kwa mazingira. Kwa mfano, kuna mashamba siku zote yatalimwa muhogo hayo hayo siku zote, ile ardhi inachoka na ardhi ikichoka na mazingira yashaharibika hapana kinachoota. Watafiti wafanye kazi ya kuelimisha wale watu jamani kuwa safari hii mmelima muhogo kesho hebu limeni choko, kunde na kadhalika ile *legumenous plants* inatia rutuba katika nchi, au wafanye *mixed farming*, wachanganyishe yale mambo lakini tunawaachia kila mtu analima anavyotaka mwenyewe.

La mwisho kwa sababu ya utafiti Mhe. Spika, kuna mambo yanatuharibikia. Mimi nasikitika sana Mhe. Spika, tunaiga na mwisho tunaharibikiwa. Mhe. Spika, hutokea matatizo ya maradhi katika miti, hutokea matatizo katika wanyama, wakati ni viumbe ni lazima watapata matatizo ya maradhi, wajibu wetu sisi ni kutibu, lakini tujue kile unachokikuta katika dunia ndio Mwenyezi Mungu keshakijaalia kile kishaweza kupambana na mazingira kinaweza kikaishi na kuzaa na kuzaana, lakini sisi tukiona hivyo tunabadilisha.

Juzi tulikuwa na mbegu zetu hapa mimi nakumbuka za mpunga, kulikuwa na mpunga wa juu na wa kwenye vuli na kadhalika. Mbegu za muhogo zilikuweko za muda mrefu, wa kati sasa kuna muhogo unaitwa *Sepideh* kwa sababu kuliingia maradhi ya muhogo miezi mitatu hukuula unaharibika unabakia na njaa na muhogo uko shambani. Hatukufanya utafiti kabisa na ni jambo la kusikitisha, yale yetu ya asili tunayadharau tunaiga mambo bila ya kuyafanyia utafiti. Ingelikuwa tunafanya *experiment* kwanza tunaweka mpaka tukaona aa hapa hakuna tatizo ndio tukaweza kuhamisha.

Hivyo hivyo Mhe. Spika, mpaka hivi sasa tujue kuwa hii kazi inayokwenda ya ufugaji wa ng'ombe hii tunayo kama alivyosema *liquid nitrogen* tunayo na mbegu tunasambaza, lakini naomba tena wakati mrefu umepita watu wetu wanalalamika.

Tulikwenda katika kijiji kimoja Shehia ya Mwambe kule kuna mama mmoja alisema mimi sina ng'ombe nina nyumbu, kwa sababu hazai, anamghasi kwa chakula anaomba afe, *Wallahi* anaomba Mwenyezi Mungu afe, tukenda Konde kule ng'ombe 23 waliokwenda kuchukuliwa wote ni tasa na walizaa watatu tu na hao watatu na wao watoto wakafa na huyo mmoja hakamiki kwa kutofanya utafiti. Kwa hivyo Mhe. Spika, tunapotafuta hizi mbegu pia tujue jamani hawa wenzetu wanatuuzia kwa nia safi au ni pesa za serikali tukachukue tulete tu tukitiana balaa?
Kwa hivyo, la mwisho ninaloomba ni kuwa tunajadili mswada huu na mimi naomba Mwenyezi Mungu atujaalie tuupitishe kwa kura zote. Lakini hii ni hatua ya mwanzo, hatua ya pili ni utekelezaji, wataalamu wote wale waliotajwa hapa ninaloomba wafanye kazi ya ziada ili mafanikio yaweze kupatikana. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu (*S.W*) aliyetujaalia uhai, uzima tukawepo hapa jioni hii kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu. Lakini pia nikushukuru na wewe Mhe. Spika, kwa kunipatia nafasi hii kutoa mchango wangu mdogo kuhusu mswada huu ulioko mezani wakati huu.

Mhe. Spika, kwa kweli mswada huu uliopo mezani ni muhimu sana kwa maendeleo ya taifa hili, ukizingatia kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa taifa. Wananchi wengi wa taifa hili wamejiajiri kupitia katika sekta ya kilimo, humo ndimo wanamotafuta rizki zao na kujikimu kimaisha. Kwa msingi huo na umuhimu Mhe. Rais wa Zanzibar mara tu baada ya uchaguzi wakati alipokuja kulifungua Baraza lako hili tukufu katika hotuba yake ya Mpango Kazi wa miaka mitano basi nayo pia alisema kuwa, "ni lazima yapatikane mapinduzi ya kilimo".

Mhe. Spika, wananchi walijenga matumaini makubwa baada ya kupata taarifa ile ya Mapinduzi ya Kilimo. Mhe. Spika, mambo hayakuwa kama walivyotaraji, kulipangwa mpango kazi zipatikane pembejeo, mbegu za nerika na kificho nazo hizo hazikupatikana kwa muda wote wa mwaka huu mmoja na nusu. Kumbe kulikuwa na jambo jengine ambalo pia lilikuwa ni kikwazo ni hili la sheria ya utafiti wa mambo haya ya kilimo nalo kumbe halikuwepo. Kwa kweli tumechelewa lakini kawia ufike, tumechelewa lakini niseme kwamba tafiti ni muhimu sana kabisa katika masuala yote ya uzalishaji wa mazao kwa wakulima.

Wakulima wetu wengi wanajikita katika shughuli mbali mbali za kilimo bila ya kuwa na taaluma maalum au kuzitumia ardhi hizo bila ya kujua ni zao lipi ambalo linashamiri au kustawi katika eneo husika. Waliendelea kulima hivyo siku hadi siku, na mavuno yakawa ni madogo na hali zao kuendelea kuwa duni, pamoja na kwamba mara nyingi serikali ilikuwa ikipigia kelele juu ya hicho kilimo na kuona kwamba tunawakwamua kiuchumi. Lakini kimsingi sheria hii sasa ifanye utafiti, umefika wakati wake tunamuomba Mwenyezi Mungu ajaalie ipite na ipate watu wazuri wa kuisimamia sheria hii.

Mhe. Spika, ni lazima sasa tafiti zetu zioneshe ni zao gani linashamiri katika ardhi gain, iwe tofauti na wakulima wetu walivyozoea madhali ni shamba lake apande chochote anachokitaka, nadhani tukiwa tutatumia tafiti hizi kwa ajili ya mipango kazi yetu katika shughuli za kilimo naamini tutafika pale tunapokwenda. Pia tafiti hizi ziingie katika mbegu kama ilivyokusudiwa kuona watumie mbegu gani ili waweze kufaidika na kilimo hicho.

Mhe. Spika, hata mbolea nazo matumizi yake wakulima wetu hawaelewi kabisa utaratibu wa kutumia mbolea hii ya kemikali na hata hiyo mboji ya kiasili nayo pia hawajui namna ya kuihifadhi.

Mwenzangu aliyemaliza kuchangia alisema kwamba wanapotayarisha mashamba basi hutumia moto zaidi kwa kuunguza, pengine kitaalamu kuchoma moto ni kuondoa wale wadudu wengine ambao Mwenyezi Mungu amewajaalia pale kuwa ndio hifadhi ya hiyo miti mingine ambayo inapandwa, lakini bila kuelewa hilo wao huanza na hali hiyo. Nina imani kubwa wakulima kwa wakati huu ambapo inapitishwa sheria hii watajenga matumaini. Kiukweli utafiti ni moja katika nyezo ya maendeleo ya taifa, jambo lolote lile litakapoanzishwa bila ya kulifanyia tafiti ya kina ili kuweza kuona utekelezaji wake unaweza kufanyika vipi sidhani kwamba linaweza likatoa majibu mazuri.

Mhe. Spika, utakuwa shahidi, wewe mwenyewe tuliyekuweka kwenye kiti hicho tumefanya uchambuzi wa kina hadi tukaona kwamba unafaa kutuongoza kukalia kiti hicho huu ndio utaratibu, lazima tufanye haya na tuone sasa tuchague yale ambayo yametokana na tafiti zetu yanatekelezeka basi yatekelezwe.

Mhe. Spika, kuna suala la kuwatumia wataalamu wetu katika hizi tafiti za kilimo. Wataalamu wapo wengi lakini tatizo limekuwa nyenzo za kufanyia kazi zao. Mara nyingi inaonekana kwamba hata wale mabwana shamba tulionao huko vijijini ambao wanatakiwa wawasaidie wakulima wetu basi mara nyingi wanakuwa hawafiki na hubakia katika maofisi na kushindwa kuzifanya kazi zao ipasavyo na wakulima kukosa taaluma hiyo, na pia kupelekea mavuno kuwa madogo na wakulima kutopata manufaa kwa kilimo hicho wanachojituma.

Mhe. Spika, katika tafiti hizi ningependa katika ile nafasi ya wajumbe basi pia tutumie Chuo chetu Kikuu cha *SUZA,* nacho kiwe na mjumbe ambaye anashiriki katika utaratibu wa tafiti zetu hapa nchini. Kwani chuo kile ni chetu na kina wataalamu wa kutosha, naamini wanaweza kabisa kutusaidia katika tafiti zetu.

Mhe. Spika, pia ningeishauri serikali baada ya tafiti hizi kufanyika, ni vizuri basi yale matokeo ya tafiti zetu yatumike ipasavyo. Mara nyingi tafiti zikishafanyika basi matokeo yake huwa ni

kubezwa na kumalizia kwamba ilifanyika tafiti tu. Hivyo basi, kubaki hali ile ile bila ya kutumiwa, hili ni tatizo na nadhani tafiti hizo kama zingetumika ipasavyo katika sekta husika basi wananchi wangepata maslahi katika yale mambo ambayo hutumiwa kwa kutumiwa fedha nyingi za serikali.

Mhe. Spika, nadhani sasa umefika ule wakati wa serikali yetu kutumia lile agizo la Abuja la Umoja wa Mataifa la kutumia asilimia 10 ya bajeti ya serikali kwa ajili ya kilimo. Hili ni agizo ambalo nadhani kama na sisi tungejipanga katika mpango kazi kwa ajili ya kulitekeleza hili kutumia asilimia 10 ya bajeti yetu kuu ya serikali, kwa ajili ya nguvu kazi hiyo kuielekeza katika kilimo, nadhani tungeweza kufanikiwa na kupiga hatua.

Mhe. Spika, tuna wakulima wengi wa mazao mbali mbali lakini mazao hayo hulimwa na hatimae hukatika njiani na wakulima hukata tamaa. Kama tunavyoelewa nchi yetu hii ni kisiwa, ardhi yetu ni ndogo, lakini pia katika tafiti hizi sheria hii imegusa sana katika sekta sita.

Sheria hii imekwenda kwenye uvuvi, mifugo, maji, na nyenginezo na ni kweli nakubaliana nayo. Kilimo peke yake kisingewezekana bila ya maji, nadhani umefika wakati sasa tukiwa tunajielewa Wazanzibari kwamba chakula chetu kikuu ni wali lakini hapa kwetu sasa hivi mchele tunaagiza kutoka nje. Naamini kwamba sheria hii itakapofanya kazi sawasawa na tafiti zikafanyika ikiwemo hii ya maji kwa umwagiliaji ninaamini wananchi wataweza kujikimu kimaisha lakini pia wanaweza kuzalisha mazao ya ziada, ambayo yataweza kuwapatia fedha kwa ajili ya shughuli zao nyengine.

Mhe. Spika, tuna bahari ambayo imetuzunguka, wengi walilizungumza hili, lakini kwa kweli bahari yetu bado kabisa haijafanyiwa tafiti za kina kuonesha kwamba rasilimali zilizomo katika bahari ile zinaweza zikapatikana kwa maslahi ya Wazanzibari. Bado uvuvi unaoendelea ni ule ule wa mazoea waliokuwa wakivua mababu na mabibi zetu, na hadi hii leo ambapo tumefikiwa na karne ya sayansi na teknolojia bado sisi tuko nyuma. Naamini kwamba rasilimali ile kama itatumiwa vizuri basi tutaondokana na hii hali duni tuliyonayo.

Mhe. Spika, hapa pamezungumzwa wizara husika na mambo haya ya kilimo.Mhe. Spika, wenzangu nao waligusa kuhusu mifugo, tulianzisha vikundi vingi vya ushirika, watu wakahamasika, wengi wao wanawake walikuwemo humo wakapata mbuzi wa mifugo, lakini kwa sababu tafiti hazikufanywa na utaratibu mzuri haukuwepo wakaanza ufugaji huo na hatimae mbuzi hao wamefariki mmoja baada ya mwengine na wananchi wakaingia kwenye hasara.

Mhe. Spika, hata ukiwatajia wakati mwengine kuhusu habari hizi za mifugo wanaweza wakakwambia msituletee mambo yasiyokuwa na maana. Kwa maana mbuzi wao waliowazoea wa asili basi wanahimili yale mazingira ambayo yapo, hivyo kwa vile sisi tumeshaanzisha kitu kigeni ipo haja ya kuangalia hata mazingira na hali ya hewa yetu kwa wanyama ambao tunataka kuwafuga katika mazingira yetu, ni vizuri zaidi tujikite katika hali hiyo.

Mhe. Spika, mimi sitokuwa na mchango mkubwa kwani wenzangu wengi wameligusa hilo. Sasa nije hapa katika mswada wenyewe kwenye sehemu ya pili kuanzishwa na kazi na uwezo wa taasisi. Hapa Mhe. Spika, kunasema kwamba kuanzishwa hiyo taasisi yenyewe.

Ningependa kusema kwamba ni lazima wajielewe wale ambao watapewa nafasi hii katika taasisi hii kwamba si ya mtu binafsi, hii ni taasisi ambayo inahitaji kutoa huduma kwa wananchi wote ifanywe kwa uzalendo, kwa juhudi na maarifa na kutumia utaalamu wao ipasavyo, vyenginevyo lengo na dhamira ya kupitisha sheria hii kuipitisha hapa haitozaa matunda. Naamini kwamba sheria hii itakapopitishwa hapa itaweza kufuatwa na kufanya kazi zake kama ilivyopaswa, basi nina imani kwamba baada ya mwaka mmoja basi mabadiliko makubwa yatatokea.

Wananchi wengi hawana kazi za kufanya, vijana wetu hawana ajira lakini nao pia wanashindwa kuingiza mkono wao katika shughuli za kilimo wakiona kuwa kilimo hicho hakikuwa na kishiko ndani yake. Wataalamu waliishia maofisini na hao waliotaka kwenda huko kulikuwa na ugumu wa kutosha kwa kukosa usafiri wa kuwapeleka kule ambako kuna walengwa waliokusudiwa.

Mhe. Spika, kama alivyosema mwenyewe Mhe. Rais ni lazima tufanye haya mapinduzi ya kilimo na hayatokuja tu mapinduzi haya bila ya kuwa na sheria inayosimamia. Leo tumefika pahala tunaweka sheria hii ili iweze kutumika, nina imani kwamba tafiti hizo zitakapofanyika zikaonesha maeneo maalum ambayo yanahusika na mazao maalum kile kilichojitokeza kwa wakati huu kwamba, vijana wetu ni wafanyabiashara ambao wanatoa matunda mengi kutoka Tanzania Bara kumbe wana uwezo wa kutosha wa kuzalisha hapa kwetu endapo tafiti za maji nazo pia zingefanyika na kujulikana kuwa kwa mwezi fulani pengine na ardhi fulani inaweza ikapandwa kipando fulani kwa ajili ya maslahi na kuwapatia tija vijana wetu.

Leo Mhe. Spika, tunaagizia tungule kutoka Tanzania Bara, tunaagizia karoti na kadhalika hali ambayo kama kweli tungetumia ipasavyo tafiti zetu basi naamini kwamba yangekuwa yanazalishwa hapa hapa kwetu Zanzibar. Zanzibar dhiki ya maji ni miundombinu yenyewe ya maji tu lakini sio kwamba Zanzibar hakuna maji. Zanzibar kuna maji ya kutosha tunahitaji tafiti za kina ili tuone kwamba tunanasuka katika suala hili la kilimo, ambalo limewaajiri wananchi wetu wengi, huo ni ukweli usiofichika.

Mhe. Spika, hapa niende katika kifungu cha 4 Muhuri wa Taasisi. Huu nao usije ukageuka hadithi utumike kwa yule ambaye amepewa dhamana kweli ya jambo lile. Tumeshuhudia watu wengi wanatumia mihuri hii, dhamana hizi kwa ajili ya kujinufaisha wenyewe bila ya kujali, bila ya kujua. Kwa sababu chombo hiki ni chombo ambacho kitahitaji fedha za kutosha nina imani kwamba serikali kuu itafanya hilo kwa sababu bila ya fedha tafiti hazitoweza kufanyika *asilani abadani.* Fedha hizi na mihuri hii itumike ipasavyo.

Mhe. Spika, kwenye kifungu cha 5 Kazi na Uwezo wa Taasisi, kutafanyika tafiti kwa kutumia utafiti wa kilimo kwenye mazao, mazingira, mifugo, misitu, uvuvi, ardhi, maji na wadudu na kadhalika kama inavyoendelea. Mhe. Spika, huu ndio msingi mkuu kwamba yafanyike haya, tunalima mazao mengi na tumeshuhudia sote kwamba tuliwahi kuona hapa maembe yalitokewa na balaa kubwa ya wadudu na wakati ilikuwa ni zao moja ambalo wananchi walianza kulisafirisha kulipeleka Arabuni. Lakini ghafla lilivamiwa na wadudu na baada ya kupelekwa kule wenzetu wakalikataa.

Kwa hivyo, kama tujuavyo kwamba Zanzibar tumefikwa na balaa kubwa la kuvamiwa na wadudu katika mazao yetu mbali mbali. Chanzo chake hatukijui kuna nini, ni sababu zipi na matunda ni muhimu sana kwa maisha ya mwanadamu. Sisi wenyewe wacha biashara lakini

matunda yote hadi yale mapera yanayopatikana huko misituni basi nayo pia yana athari za wadudu. Nini kimesababisha mpaka leo sidhani kwamba kutakuwa na mtaalam ambaye amesema labda aliwahi kufanya tafiti na kuonesha kwamba kuna sababu moja, mbili, tatu ambayo imesababisha matatizo haya ya uharibifu wa matunda yetu. Mhe. Spika, nadhani kwa kuanzisha sheria hii nina imani kwamba sasa italinda, itasimamia na itaendeleza, haitokuwa sheria yenye kuanzishwa bali itakuwa yenye kuendeleza tafiti katika kilimo chetu. Mhe. Spika, kwa hayo machache napenda kuunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, nakushukuru na mimi kunipatia nafasi hii ili niweze kusema machache tena haraka haraka. Mhe. Spika, kwanza naipongeza serikali kwa kufikiria kitu hichi cha utafiti, ni kitu muhimu sana kwa sababu jambo lolote la maendeleo huwezi kulifanya bila ya kuwa na utafiti kwanza. Kwa hivyo, naipongeza sana serikali kwa kuweza kufikiria namna ya kuunda taasisi ya utafiti huu ambao tunauzungumza leo.

Mhe. Spika, nilikuwa napenda niseme kitu kimoja. Unajua tuna wataalam wa kila aina katika nchi yetu na wanafanya kazi nzuri. Lakini mara nyengine tunakuwa tunashindwa kutekeleza ule ushauri waliotupa wa kitaalam na mara nyengine inaweza ikaudhi kwa sababu wataalam na wanasiasa mara nyengine wanakuwa hawaendi vizuri sana, inaweza ikaudhi na baadae yule mtaalam akajuta kwa nini akatoa ushauri wa aina ile.

Hata ukisoma kitabu cha Shaaban Robert Kusadikika mambo kama yale yamo mle. Pia hapa katika miaka ya 80 kuna mtafiti mmoja wa mambo ya uchumi aliwahi kutoa makala yake wakati ule kule Mwanyanya watu hawajajenga kuna mipera mingi sana. Akasema pera lililoko Zanzibar kama serikali italishughulikia lile pera basi lingetosha kuongoza uchumi wa Zanzibar. Lakini mtaalam huyo akaonekana mshenzi kweli kweli na nadhani dola ilikuwa inamtafuta imshikishe adabu. Lakini maneno aliyoyasema yalikuwa mazuri yalikuwa yapaswa tukae chini tuyazingatie na pengine yalikuwa na ukweli ndani yake. Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana ushauri ambao utakuwa ni wa wataalam wetu tumewasomesha wenyewe kwa pesa zetu wenyewe tuuzingatie usipite na hewa.
Mhe. Spika, tunahitaji kufanya utafiti hasa huu wa kilimo kwa sababu tuna changamoto nyingi. Inawezekana karibu asilimia 70 ya Wazanzibari wanategemea kilimo ama kwa kujikimu kwa chakula au hata kwa kujikimu kiuchumi. Kwa hivyo, jambo ambalo lina asilimia karibu 70 ya Wazanzibari si jambo la kuliachia tu liende hivi hivi linahitaji kweli utafiti. Lakini tukiwa na wataalam wa utafiti tunaweza kujua ni aina gani ya udongo inakubali mazao ya aina gani. Ni jambo muhimu sana kujua hilo kwa sababu kuwekeza katika kilimo ni gharama, sasa kama hujui *tendency* ya udongo ule ambao unataka kuotesha kitu unaweza ukajishtukia siku moja umepoteza gharama kubwa lakini hatimaye huna ulichokivuna.

Mhe. Spika, mimi siku moja nilikurupuka nikapanda migomba kwa gharama kubwa kidogo lakini ilinawiri kwa kipindi kifupi sana mwaka haukufika hakuna mgomba tena pale nikajua kosa langu. Maana yake niliwafuata watu wa kilimo wakanambia bwana hukuja kwetu tukakushauri kama udongo huo unaotaka kuotesha migomba unakubali au vipi. Kwa hivyo, nikaona umuhimu mkubwa sana wa kufanya utafiti kwanza. Lakini tunahitaji pia kujua ni kilimo cha aina gani kwa mazingira ya kwetu Zanzibar kinaweza kikausaidia zaidi uchumi wetu. Ni jambo muhimu sana na hilo hatuwezi kulipata mpaka tufanye utafiti.

Mhe. Spika, wenzangu wengi wamesema hapa tumetokewa n maradhi ya aina kwa aina ya mazao hapa na kwa bahati mbaya pamoja na wataalam tuliokuwa nao lakini tuliyaacha yale maradhi mpaka yakatuathiri sana. Mfano mzuri ni maradhi ya migomba ambapo ilikuwa inakauka ovyo ovyo hata ikiwa kwenye sehemu za maji lakini unaikuta inakauka majani. Lakini tulichukua muda mrefu bila ya kufanya utafiti tukajua migomba hii inaathirika kwa kitu gani.

Tuna wadudu wa maembe wale tulichukua muda mrefu kweli kweli tokea walikuwa katika maeneo madogo madogo tu katika nchi yetu lakini hatukufanya utafiti namna ya kuwadhibiti mpaka wadudu wale wakaenea nchi nzima sasa hivi ni gharama kubwa ambazo wataalam wanasema ni kazi kubwa kweli kweli kuweza kuwadhibiti wale wadudu. Sasa hii ni kuonesha kwamba kwa kweli ni muhimu sana kufanya utafiti.

Lakini pia Mhe. Spiaka, tunahitaji kufanya utafiti wa soko ambalo ni jambo moja muhimu sana katika mambo ya kilimo, sio mtu akurupuke alime tu lakini hajui soko liko wapi mimi nikishakulima mazao yangu nitauza wapi. Kwa hivyo, bila shaka soko nalo linahitaji utafiti wa kina ni kilimo gani tukilima tutapata soko na soko hili liko wapi ni mambo yanayohitaji kushughulikiwa vizuri.

Mhe. Spika, wakulima wetu wana changamoto nyingi moja ikiwa ni uwezo wa kulima, pembejeo, madawa ya wadudu haya, lakini pia tatizo la maji. Kwa hivyo, nakubaliana na huu mswada kwamba wameweka pale mwisho kwenye jadweli namba moja wizara nyingi ambazo zitahusika katika kulishughulikia suala la kilimo.

Mhe. Spika, kama nilivyosema nitasema haraka haraka kwa sababu muda unakimbia sana, nataka nije kwenye mambo mawili tu katika huu mswada. Jambo la kwanza ni kifungu cha 1 ambacho kinataja jina la sheria yenyewe. Mhe. Spika, naomba kunukuu kifungu cha 1 “Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ya Mwaka 2012 na itaanza kutumika mara itakapotiwa saini na Rais.”
Lakini ukiangalia jina hili halafu ukenda kwenye ukurasa wa 27 ukisoma madhumuni na sababu ya mswada huu unakuta kuna kitu tofauti kidogo. Mswada tunaanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, lakini ukija kwenye madhumuni na sababu utakuta pale baada ya ile (a) na hata hiyo (a) yenyewe inasema sababu zifuatazo: “Kutambua na kuweka mfumo utakaowezesha kusimamia na kuratibu tafiti zote za kilimo na maliasili. Ukisoma (b) “Kuipa taasisi uwezo wa kisheria na kiutendaji katika kutoa huduma za utafiti wa mazao ya kilimo na maliasili.”

Sasa hili neno maliasili halimo katika jina la huu mswada na maliasili ni neno pana kidogo. Kwa sababu hata mafuta ni maliasili lakini ninahakika mswada huu sio madhumuni yake kufanya utafiti wa mafuta. Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana wanasheria warekebishe kidogo maana yake ikiwa ni maliasili za baharini basi waainishe kama maliasili za baharini lakini ionekane kama katika maliasili yenyewe mafuta hayahusiki na taasisi hii.

Mhe. Spika, jambo jengine ambalo pengine litakuwa la mwisho ni kifungu cha 6 nafikiri kuanzisha muundo wa Baraza hili la Taasisi ya Utafiti wa Kilimo. Ukisoma *sub-section* 3 na hata *sub-section 4* pia inasema “Mtu hatoweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti isipokuwa awe na angalau shahada ya kwanza ya kilimo au masomo ya sayansi kutoka kwenye chuo kinachotambulika. *Sub-section 3* inasema “Isipokuwa kwa Mkurugenzi na Wakurugenzi wa

Wizara zilizotajwa." Kwenye jadweli namba moja hiyo bila shaka. Sifa za Wajumbe wa Baraza zitakuwa angalau shahada ya kwanza haikuambiwa shahada ya kwanza ya nini, tuseme ni ya kilimo nayo pia.

Lakini mimi nilikuwa nahisi kilimo kinachukua sehemu kubwa sana ya uchumi wa nchi yetu. Sasa ni muhimu katika hili Baraza hasa kwa sababu tunashughulikia mambo ya utafiti kuwe na watu wenye sifa za uchumi kwa sababu kilimo kinakwenda na uchumi wa nchi. Kwa hivyo, yule mtu wa uchumi atakapokuwemo katika Baraza hili basi ushauri wake pia utakuwa unalenga kwenye mambo ya kuimarisha uchumi.

Kwa sababu unaweza ukalima Mhe. Spika, lakini kilimo chako kikawa cha mahitaji ya kujikimu kwa chakula kuliko kuimarisha uchumi na malengo ya kilimo pia ni kuimarisha uchumi. Sasa nilikuwa nahisi kuna haja ya kuwa na mtu mwenye sifa za kiuchumi hizi *degree* nyengine ziwe za uchumi. Nafikiri tukifanya hivyo tutakuwa tumeboresha hili Baraza letu na litakuwa linalenga hasa kwenye yale malengo ambayo tumeyakusudia.

Mhe. Spika, mswada huu ni mzuri na kwa kifupi hauna makosa na mimi binafsi naukubali kwa asilimia mia moja na nawaomba sana na wenzangu waukubali. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakushukuru sana kupata wasaa huu mdogo kuchangia machache tu mswada huu wa Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili juu ya Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwa kweli tunampongeza sana Mhe. Waziri na amekuja wakati ndipo, maana yake kaja na mswada mpya na mswada wenyewe ni mswada muhimu sana. Mhe. Spika, maendeleo kama walivyosema waheshimiwa walionitangulia ya kitu chochote au maendeleo ya nchi yoyote yanategemea sana msingi wa utafiti. Kwa sababu utafiti ndio unafuatilia mwenendo wa kila kitu, matatizo yanayotokezea na halafu unafanya huo utafiti kushauri kupata ufumbuzi wa yale matatizo yaliyopo.

Mhe. Spika, kuna waheshimiwa waliuliza utafiti huu unatusaidiaje. Nafikiri unatusaidia sana katika kuondoa migogoro mfano katika matumizi ya ardhi, kuleta maendeleo kama nilivyosema, kuongeza tija ya uzalishaji, kupunguza umaskini, hata kuangamiza maradhi na wadudu waharibifu. Mhe. Spika, mambo mengi kama nilivyosema kwa kweli kama una matatizo suala la msingi kwanza jiulize kwa nini linatokea tatizo hili ndio utafiti, halafu tazama wenzako huko nyuma wamefanya nini, kama kiko kilichofanywa basi ndio uwe msingi wa wewe uanzie pale ndio utafiti *(research)* unazidi kutafuta.

Sasa mimi nampongeza sana Mhe. Waziri na Wizara kwa ujumla kutwambia kwamba kwa mswada huu kwenye ukurasa wa 17 kwamba maana ya kilimo kwa mswada ni uoteshaji wa mazao ya kilimo, misitu, ufugaji wa wanyama na samaki na kwa kuzingatia uhifadhi wa mazingira.

Nafikiri hii ni *definition* nzuri sana na inayotuongoza hasa katika suala zima la utafiti. Hii Mhe. Spika, inaturejesha nyuma kule tulikotoka zamani katika vituo vyetu vya utafiti hasa hichi kituo

kikuu cha utafiti tunachokirejesha hadhi yake Kituo cha Kizimbani. Kituo hichi ndio ilikuwa Makao Makuu ya Utafiti wote kama ilikuwa utafiti wa wanyama, wa mifugo, wa mazao, wa udongo, yote yalikuwa pale na kuna vituo vidogo vidogo lakini hichi ndio kilikuwa kituo mama.

Sasa Mhe. Spika, mimi napongeza sana Wizara kwa kuona kwamba aaa kwa kweli lazima turudi katika mtazamo wa zamani, si vya zamani vyote vilikuwa vibaya. Mtazamo ule mzuri pale ndio itakuwa kama ni *coordinating centre* au kama nilivyosema ndio makao makuu ya utafiti wote na mambo yataanzia pale yatapangwa pale. Pia kuna vituo vidogo vidogo vingi nafikiri vyengine vimeanza kufa lakini sasa navyo kwa ule mtandao vitaanza kufufuka. Kwa mfano, kituo kile cha Chamanangwe, Matangatuani, Weni, Makunduchi, Mkwajuni, Bungi, Wesha, vyote hivi vilikuwa vinatumainia Kizimbani kama ndio baba. Bado tunaendelea navyo katika uzalishaji mbegu lakini utafiti kwa kiwango kikubwa ukiacha Matangatuani kwa kweli naweza kusema kwamba umepunguka sana.

Kwa hivyo, kwa mswada huu kwa mantiki yake Mhe. Spika, ni imani yangu kwamba vituo hivi navyo vitafufuka. Ni muhimu kwa sababu utafiti hasa wa mbegu, mbegu utakayopendekeza kwamba hii itafaa labda kwa maeneo ya mvua nyingi kama ya Kizimbani si lazima kwamba itafanya vizuri mbegu ile katika eneo la Bungi au katika eneo la Mkwajuni au la Matangatuani. Kwa hivyo, kuna umuhimu wa kufanya wenyewe watafiti wanaita *on farm research* au utafiti wa shambani ambako kwa kweli utaona hasa zinafanya vipi hizo mbegu kazi huko shambani.

Mhe. Spika, mimi napongeza katika *approach* hii ambayo Wizara imeichukua na tunapozungumzia utafiti basi na hizi *section* tulizozitaja za mazao ya kilimo, misitu najua kuna aina nyingi za utafiti, wa maji, wa umwagiliaji, uvuvi, mifugo, mazingira, udongo, wadudu, hata uzalishaji wa maziwa.

Mhe. Spika, lazima nipongeze Wizara kwa kweli kwa kazi kubwa sana waliyoifanya hasa pale Kizimbani kwa sababu haya mambo nataka kusema kwamba hapo kati kati kidogo yalipotea potea. Sasa wamejipanga vizuri, wamejigawa, wametafuta wataalam wamewaweka pale, waheshimiwa walisema Wizara hii ina wataalam wengi, kweli ina wataalam wengi lakini kazi zake bado ni nyingi sana na zinahitaji watu waliobobea katika *section* mbali mbali. Kuna watu wa *profession* kuanzia *degree* na kwenda juu, lakini kuna wale *technicians* kuanzia diploma labda mpaka *certificate* wale watu nao pia wanahitajika, wale ndio wanaofanya kazi za msingi za shambani zile.
Sasa ni kweli kuna wataalam wengi lakini hili Mhe. Juma Duni Haji huwa analiita dudu, hili dudu kubwa yale mambo yake ni mengi sana na yanahitaji watu ambao kwa kweli wanajitolea. Kwa sababu utafiti ni kujitolea unatupa muda wako mwingi sana kwa hiyo unahitaji motisha ya hali ya juu kabisa.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi naipongeza sana Wizara kwa mtazamo huu mpya na naamini kama walivyosema Waheshimiwa Wajumbe wenzangu tukiwa pamoja tukifanya kazi pamoja kwa mashirikiano kati yao wenyewe na kwa kutumia ile *approach* ya siku hizi ya multi-*sectoral approach* au *inter disciplinarity.* Yaani tukae pamoja tusifanye kazi kwa mtu peke yake tu, utafiti wa siku hizi watafiti wanafanya kazi kwa pamoja. Hili ni suala la msingi sana kwa hiyo naamini wakiwa kama ilivyoelezwa katika ile kamati ya wataalam ambayo kazi yake kubwa itakuwa kuchambua miradi ili tuone kwamba kazi za utafiti hazijirejei.

Leo Mhe. Abubakar Khamis Bakary kafanya utafiti labda wa mfumo wa kilimo, mimi kesho nafanya utafiti huo huo, hata miaka mitano haijafika. Kwa hivyo, nafikiri kazi zilizowekwa za kamati ya wataalam katika ukurasa wa 23 zitasaidia sana na zitaongoza na kuepusha migongano au marudio ya utafiti pasi na kupita muda mkubwa.

Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 24 kulielezwa fedha za taasisi vipi utafiti unaweza ukajiendesha wenyewe. Kwanza wamesema fedha zote zitakazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa matumizi ya taasisi. Hili tunakubali hii ni chanzo kimojawapo lakini kwa kweli kwa utafiti kutegemea fedha za serikali ni kidogo mno. Kama nilivyosema kazi za utafiti zinahitaji muda mwingi, zinahitaji rasilimali nyingi, kwa hivyo lazima kuwe na mbinu za kutafuta pesa zaidi. Wapi utazipata hizo pesa zaidi.

Mhe. Spika, kama nilivyosema utafiti siku hizi ni kama *joint project* inakwenda kilimwengu. Kuna taasisi za kimataifa ambazo zimejitolea zinapata mapesa maalum kwa kufanya utafiti. Kwa mfano, Philippines kule kuna kituo kinaitwa *IRRI (International Rice Research Institute)* wao wamebobea kwenye utafiti wa mpunga tu kuusarifu wali na mambo yake hayo yote na sisi watu wa Unguja tunapenda sana wali. Kwa hivyo, kwa kweli hawa ni marafiki zetu wakubwa sana tulileta mbegu nyingi sana za mpunga hapa tukazijaribu mpunga wa juu na mpunga wa umwagiliaji na tumepata baadhi ya mbegu mpaka leo tunaendelea nazo.

Kwa hivyo, hawa ni watu wa kuwa karibu nao sana Mhe. Spika, kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri na hii taasisi ambayo tunaiunda basi wawe karibu sana na vituo hivi vya utafiti, utafiti wa kilimwengu wanapata mapesa mengi na wao wako tayari kushirikiana na nchi zetu ndogo ndogo ambazo tunafanya utafiti. Vituo hivi ninavyokumbuka baadae labda Mhe. Waziri ataweza kunisaidia, mimi nakumbuka mwisho niliviacha 13 kabla sijaja kujiunga na Baraza lako Mhe. Spika, sijui leo viko vingapi.

Lakini kama nilivyosema kiko hicho kinachoshughulika na mpunga na huo mpunga pia uko *IRRI* au Philippines lakini katika Bara letu la Afrika kuna taasisi moja inaitwa *WARDA (West African Research Development Association)* iko Ivory Coast na hiyo ndio iliyoizalisha ile mbegu tunayoita *nerika* ambayo ni kama muokozi kwetu. Mbegu ile ningeomba sana Waheshimiwa Wawakilishi tusiitupe msimu huu tuijaribu kwenye shamba zetu.

Mhe. Spika, najua mkulima wewe na utakuwa mstari wa mbele kutuongoza, mbegu hii haina mazonge mengi, kama unavyopanda muhogo na mbegu hii inakubali. Tumeona wewe huwezi kuamini leo useme Bambi ukazalishe mpunga, maana yake mtu ukimuhadithia hawezi kuamini, lakini tumekwenda mwaka jana tumeona kazi nzuri sana iliyofanywa na kilimo *nerika* imeota Bambi nchi ya ukame na ni mbegu fupi na ndio imetolewa huku *WARDA.*

Mhe. Spika, kituo chengine ni vituo vinavyofanya utafiti wa mihogo na mazao ya mizizi kama vile *IITA* kule Nigeria, lakini pia Columbia hawa ndio hasa watafiti wanajishughulisha zaidi na mazao haya ya mizizi. Lakini pia kuna kituo kinajishughulisha na mazao ya ndizi *INIBAB* wao wame-*specialize* utafiti wa migomba tu, mgombe wewe unauona majani yake labda yamenyauka lakini ujiulize kwa nini, kuna tatizo pale.

Sasa hawa *INIBAB* na sisi kama tulivyosema tulikuwa na uhusiano nao hapa na ni imani yangu kwamba Wizara ya Kilimo na Maliasili bado mahusiano yale wanaendelea. Kama nilivyosema mambo mengi wanayafanya tunaweza tukayachukua tukayajaribu na kwetu.

Lakini pia jirani yetu tu hapa Kenya kuna kituo kikubwa sana kinaitwa *ICIPE (International Centre for Insect Physiology and Ecology)* wale ndio wataalam wa utafiti wote wa wadudu waharibifu. Waheshimiwa Wajumbe wengi sana walizungumza juu ya matatizo ya wadudu waharibifu kama mafunza kwenye maembe, mafunza kwenye mahindi na mengineyo. Sasa hawa wenzetu wa Kenya wana kituo hichi na hivi vituo vinatambulika kimataifa sio kama urafiki wa nchi kwa nchi tu na wana mapesa mengi sana wanapatiwa hawa kutoka kwa watu wa biashara na wengineo. Kwa hivyo, ni vyema sana Mhe. Spika, hili suala zima la sera za kuendesha utafiti lazima tuandike miradi, tutafute, tuhangaike na wao wako tayari kabisa. Mhe. Spika, ningemuomba sana Mhe. Waziri tujitahidi katika suala hili, tuwe watundu wa kuandika miradi, tuwe watundu wa kutafuta, kwa kweli hizi pesa ni nyingi tutazitafuta.

Mhe. Spika, mfano kuna kituo chengine kinaitwa *IFRESAT* ambao hawa wanajishughulisha na mazao yanayostahamili ukame, lakini kuna kituo chengine Mexico kile kinaitwa *SIMIT* hawa ni utafiti wa mahindi tu. Hii yote Mhe. Spika, nilitaka kusisitiza kwamba kuna vituo vya kilimwengu wana mapesa mengi sana na hatutegemei bajeti yetu tu ya SMZ kwa utafiti. Tukitegemea bajeti yetu tu wataalam hawa kama nilivyosema watakuwa hawana motisha na watadumaa tu, lakini lazima tuwahangaikie waandike miradi kwa wingi sana.

Mhe. Spika, hata *COSTEC* hii iliyoko Tanzania Bara wana pesa nyingi sana na ni wajibu wetu na ningewaomba sana wataalam wa utafiti tulionao Wizara ya Kilimo na Maliasili watumie huduma hizi za *COSTEC* katika kupata pesa za kuendesha utafiti.

Mhe. Spika, ukurasa wa 21 kifungu cha 25 lilielezwa suala zima la taarifa ya mwaka kwamba itengenezwe, iwasilishwe, halafu inasema Mkurugenzi ataandaa kila mwisho wa mwaka wa fedha taarifa za kazi za taasisi kwa mwaka huu na kuziwasilisha kwa Baraza, na baada ya kuidhinishwa atawasilishiwa Mhe. Waziri.

Suala hili ni zuri Mhe. Spika, na mimi nalipongeza sana kwamba lazima mtafiti kila mwaka aoneshe kafanya kitu gani. Haiwezekani mtafiti mwaka mzima hana hata ripoti moja, kwa kweli itakuwa haina maana. Isiishie hapo tu, lakini lazima tuwe na utundu au tuwe na ubunifu wa kuandika kwenye *International Journal*, kuna ma-*journal* ya kimataifa haya na pale ndipo unapojulikana kwamba mwaka fulani Mhe. Dk. Said Ali Mbarouk kafanya hivi na hivi na kaona hivi na hivi. Sasa *journal* lile linaonekana kimataifa.

Kwa hivyo, haya maandishi aliyoyazungumza Mhe. Waziri kwenye kifungu cha 21 yasiishie kwenye ripoti zetu hapa hapa tu, hapana, tuandike kwenye ma-*journal* tuchapishe, tufanye makongamano. Kuna watu wanaletewa tiketi tu. Kwa mfano, leo ukatoe *paper* London au kwengineko kwa *paper* yako baada ya kuiona na utafiti ule. Kwa hivyo, suala hili nataka kusisitiza sana kwamba lazima mtafiti kila mwaka aandike. Hii Mhe. Waziri ningekuomba au ningesema kwamba ndio *criteria* ya kupata *increment* basi ingekuwa hii. Mtafiti mwaka mzima asipoandika akachapisha basi huyo hafai utafiti, kwa hivyo hii ndio *criteria* moja wapo ya kuwapima na kuwapa nyongeza.

Mhe. Spika, kama ma-*professor* wa Chuo Kikuu ambao kupanda cheo kwako basi ni kufanya utafiti, na hapa nataka niunganishe Mhe. Spika, kuomba sana hiki kituo chetu cha utafiti, lazima kiwe karibu sana na vyuo vikuu. Waheshimiwa Wajumbe walizungumza hapa kwamba hawawezi kujiweka peke yao, lazima kuwe na *link* na vyuo vikuu. *Alhamdulillah* Chuo Kikuu chetu cha SUZA tayari kina kitivo cha *science* na wako watafiti wazuri tu kule. Kwa hivyo ningeomba sana tusiwe mbali na vyuo vikuu, kwa sababu zile *project* za wanafunzi nazo ni sehemu ya utafiti na zitasaidia maendeleo ya nchi. Kwa hivyo, Mhe. Spika, nilikuwa nasisitiza sana suala la uchapishaji.

Mhe. Spika, katika zile kazi za wataalamu wamezungumza kwamba watatayarisha mpango kazi wa utafiti wa taasisi na kuwasilisha kwenye Baraza kama nilivyosema, ili ziweze kupitiwa. Kuna kitu kimoja ambacho niipongeze wizara kwa kiwango wameanza kukishughulikia, *bio technology.*

Mhe. Spika, hatuwezi kuepukana na *speed* ya haraka sana ya kuendeleza utafiti hasa wa mazao bila ya kutumia *bio technology*. Tunawashukuru wizara kwa kiwango fulani wameanza pale Kizimbani kwa *tissue culture* na hili waendelee, wasomeshe watu na tuende zaidi na zaidi. Kuna nchi kidogo wanapingana, wanasema hapana, *bio technology* hatuitaki kwa sababu wanaogopa uchafuzi wa mazingira. Lakini pia wana matatizo ya kile kitakachozalishwa kitakuwaje. Lakini wengine wana wasi wasi kwamba labda kile kitakachokuja kwa usalama wa binadamu. Kama mahindi yale tunayokula mengi sana yanatoka Marekani, matokeo yake ni hayo hayo.

Kwa hivyo, ningeomba sisi tusiwe na wasi wasi lakini tujaribu, kwa sababu kuna mambo mengine tunaweza kujaribu wenyewe hapa hapa, lakini kuna mambo mengine tunaweza tukachukua mawazo yao tu na kuyaona. Kwa hivyo, muhimu tusiachwe nyuma, suala la *bio technology* ni suala mkombozi, ni suala la kimaendeleo na ni suala la kisasa. Mhe. Spika, niliona nilitilie mkazo sana hili.

Suala la mwisho Mhe. Spika, ni kwamba kuna Waheshimiwa Wajumbe wengi walizungumza sana kwamba hatuko *serious*, mambo mengi sana yamefanywa lakini yamewekwa tu. Kwa kweli mimi niseme sio tatizo, lakini tatizo, na sio hili la nchi hii tu, ni nchi nyingi sana. Hivyo tatizo ni ile *link,* yaani unafanya kazi vipi kati ya utafiti na wale wanaoeneza matokeo ya utafiti. Hawa watu ni lazima wawe pamoja, kuwe na *strong link* kati ya watafiti na hawa wanaoeneza matokeo ya utafiti.

Mhe. Spika, nashukuru siku hizi kuna *technology,* wizara wameipata na kwengineko wanatumia, kutumia hizi *pharmacy trading school,* yaani mashamba darasa, kule watafiti wanaeneza elimu kwa wakulima na wanafanya kazi pamoja. Hili ni suala zuri sana na naomba tuliendeleze, kwa sababu kumbabili mkulima kwenye mambo aliyozowea kuyafanya sio rahisi, pale ana rizki na maisha yake, akiukosa msimu mmoja tu atakufa njaa yule.

Kwa hivyo, kumkabili mkulima yule Mhe. Spika, lazima kweli uende na kitu cha kumshauri. Kwa hivyo, uende naye taratibu, usiende kwa papara hatokubali. Mhe. Spika, niliona nisisitize hili kuwa tatizo kubwa la matokeo ya utafiti kuwafika wale wakulima, hilo ndio suala la msingi. Sasa suala hili tushirikiane sote hasa sisi wanasiasa pia tuna jukumu letu.

Mimi ningemuomba sana Mhe. Waziri, nilikuwa nanong'ona hapa na mwenzangu jirani yangu, Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria kuwa ingekuwa vizuri Mhe. Waziri angetuandalia *study tour* tukaenda Kizimbani pale, tukaona mambo yaliyokuwepo pale, nafikiri wengi sana tungefunguka muono wetu na mtizamo wetu. Wengi wameukubali mswada tunashukuru, lakini mambo wangeyaona pale wangekwenda labda na *vetenary* pale Maruhubi wakaona mitambo ile ya AI na mengineyo, basi najua ni kamati moja au mbili tu ambazo zinakwenda *field* kule.

Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri hasa Kizimbani pale wakaenda wakaona mbegu za mpunga zilizokusanywa, wakaona waheshimiwa aina mbali mbali za udongo uliokusanywa pale na vipi unasarifiwa na vipi utafiti unavyofanywa. Nafikiri itatusaidia sana kupata muono zaidi katika suala zima la utafiti. Mhe. Spika, niliona nigusie hayo tu. Niseme naunga mkono hoja hii ya Mhe. Waziri kwa asilimia mia moja, ahsante sana.

TANGAZO

Mhe. Spika: Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame tunakushukuru, hapana shaka muda uliobaki ni mdogo hautatosha kwa kufanya majumuisho leo, inabidi kazi hii ifanyike kesho baada ya kipindi cha maswali.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla ya kusitisha shughuli zetu kuna tangazo moja. Kwanza tumshukuru Mhe. Waziri wa Afya, ametupa taarifa kupitia madaktari wake kwamba ile kazi ya kupima afya kwa Waheshimiwa Wajumbe itafanyika kuanzia kesho asubuhi mapema, mnamo saa 1:00 madaktari wetu watakuwepo hapa kuanza kufanya shughuli hiyo.

Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe tunashauriwa usiku wa leo, kikomo chetu cha kula kifikie saa 6:00 za usiku, kula na kunywa. Baada ya hapo tujizuie kula ili kesho tukija mambo yale ya *digestion* na mengineyo yawe tayari yameshakaa sawa na tukabiliane na madaktari wetu kwa ajili ya kupima afya.

Kwa hivyo, tunategemea Waheshimiwa Wajumbe tutashiriki vya kutosha kabisa na mimi nitaongoza upimaji huo. Tutapima mambo mengi kwa ridhaa ya mjumbe. Baada ya hayo machache Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni na sasa naakhirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 11/04/2012, saa 3:00 asubuhi barabara.

(Saa 1:38 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka
tarehe 11/04/2012 saa 3:00 za asubuhi)